Kikao cha Ishirini na Saba - Tarehe 21 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe.Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2014/2015
Wizara ya Kilimo na Maliasili

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea. Nafasi ya kwanza kwa leo hii inakwenda kwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, baadae Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, wakati Mhe. Salma Mussa Bilali anajitayarisha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuwa mchangiaji wa mwanzo siku hii ya leo ya Jumamosi. Nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Vile vile nimshukuru Kaimu Waziri wa Wizara hii na nimpe pole sana kwa majukumu ya wizara nzito hizi mbili alizokuwa nazo, ukiwachia yake mwenyewe ingawa zinafanana kwa kiasi fulani.

Vile vile nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili katika shughuli za Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Kwenye Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, kuwa mstari wa mbele kuongoza kamati hii, ikiwa mvua au ikiwa jua kwa hivyo nikushukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa utendaji wako huo, ikiwa mimi ni mmoja wa wajumbe wa kamati hii ninayoizungumza.

Pia nitakuwa sikumfanyia haki Katibu Mkuu wa Wizara hii, ndugu Affan kwa jitihada anazozichukua, pamoja na kuwa wizara hii imetupwa kwa kiasi fulani au naweza kuthubutu kusema ni wizara nzima nayo, tukiiwacha Wizara ya Afya na hii imetupwa na kutokushughulikiwa.

Mhe. Spika, cha kusikitisha leo kamati kwa mara nne au mara tano inataka kukutana na waziri, lakini hayupo, kazi zitafanyika vipi. Sijui Naibu Waziri kama anafika BLM. Leo tuna mawaziri watatu wasiokuwa na wizara maalum, ni kitu cha aibu! Kuna Mhe. Machano Othman Said, pana Mhe. Shawana Bukheit Hassan, na Mhe. Haji Faki Shaali. Leo kubadilisha kumchukua Mhe. Suleiman Othman Nyanga kumpa wizara maalum na kumpeleka mjumbe mwengine pale, lipi la aibu.

Vile vile nimshukuru Mhe. Saidi Ali Mbarouk, mwisho aliitwa akakaimu wizara hii lakini nafikiri sheria haziruhusu. Akasema mimi niko tayari kujitolea, kumtafuta waziri kukaimu Waziri wa Kilimo kwa muda mrefu, sisi tunashindwa. Huu ni ushauri kama watendaji wapo wa serikali, tukimpeleka Mhe. Machano Othman Said au Mhe. Shawana Bukheit Hassan kukaimu wizara ile, Mhe. Suleiman Othman Nyanga akaja kukaa huku kwa wizara isiyo maalum kuna ubaya gani. Hayo ni mawazo yangu na fikra zangu; kama zitatendewakazi sawa, na kama hazikutendewa kazi sawa. Lakini itaendelea wizara hii kuteseka.

Mhe. Spika, ndugu Affan Othman Maalim, Katibu Mkuu anakwenda mpaka viatu vinalika kwa kwenda, tunafanya nini!

Mhe. Spika, nije na kilio cha kamati ambacho nilikikuta mimi, kuhusu deni la wakulima wa mbegu. Leo ni aibu serikali kuwa inadaiwa na wakulima, baada ya serikali kuwasaidia wakulima, kitu hicho hakielekei. Hapa nitahitaji maelezo ya Mhe. Waziri, naomba kulitaja deni sasa na kuliandika. Wakulima wa Cheju wanadai milioni 69,212,971, wakulima wa Mwera milioni 7,300,888, Kisongoni milioni 13,422, Upenja milioni 16,264, jumla shilingi milioni 106. Leo serikali kweli inafanya haki kwa wakulima hawa.

Hapa pana kazi nzito kama serikali itashindwa kuwalipa kweli shilingi milioni 106. Tuna nia kweli ya kuwasaidia wananchi hawa na wanafanyakazi katika mazingira magumu watu hawa. Kuna wakulima wanne walifika katika Bonde la Mtwango kuja kulia katika kamati na mimi nimo shahidi katika kamati hiyo.

Kwa hivyo, kama serikali itashindwa kuwapatia fedha zao shilingi milioni 106, mimi mwisho niliomba ile mbegu nilikuwa nayo ya akiba na kamati shahidi, wasije wakategemea tutahangaika na hizi kama zitapatikana. Kwa suala hili nitaiomba serikali itowe maelezo kamili kama itashindwa kweli kulipa deni la milioni 106. Tuna nia ya kuwasaidia wakulima kweli!

Baada ya hapo Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 200 kuhusu Idara ya Misitu. Mwaka jana nilichangia eneo hili nikasema misitu inazidi kuteketea na mito yetu inaanza kupotea. Kama mto wa Bububu na mto wa Mwera hadhi yake inaanza kupotea na kuna hatari pengine hata maji tukajakuunga kutoka Bagamoyo, tukapitisha bomba baharini mpaka huku. Kwa hivyo vitu hivi ni vya kuangaliwa sana.

Eneo jengine Mhe. Spika, ambalo nitahitaji maelezo ni lini ukulima wa umwagiliaji maji katika kijiji cha Muyuni utaanza baada ya harakati ya Mhe. Mbunge na Mhe. Mwakilishi kuhangaika na kupata msaada. Nataka kujua.

Mhe. Spika, jengine ambalo wizara hii imetupwa kuhusu kuingiziwa pesa. Wizara hii imekuwa na migogoro sana ya kuingiziwa pesa na tunaambiwa kilimo mwanzo, lakini naona kama itakuwa kilimo mwisho, sio mwanzo tena. Wizara hii naona bado uingizwaji wa pesa zake hauridhishi.

Kazi nyengine iliyofanywa ya kujenga mtaro wa mita 500 na *pump* mbili kwa bonde la Bumbwisudi - Kibokwa kupitia mradi wa *KOICA*. Hili ni jambo la kupongezwa sana. Tuwapongeze kwa jitihada walizofanya wizara hiyo.

Mhe. Spika, suala jengine ni kutokufika mbolea kwa wakati kwa wakulima na dawa ya kuulia magugu. Mhe. Spika, kilimo kinakwenda na wakati. Unaweza kwenda kuwapelekea wakulima trekta kwenda kuchimba, ikawa ardhi haikubali kuchimbika, atalima nini? Kwa sababu unampelekea mbegu wakati sio.

Mhe. Spika, nafikiri hapa panatosha kwa mchango wangu huo. Kwa hivyo nitahitaji maelezo katika maeneo hayo ya madeni, na ukulima wa Jimbo la Muyuni wa umwagiliaji maji ni lini utaanza baada ya mkataba kusainiwa. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mohammed Mbwana Hamad na Mhe. Salma Mussa Bilali ajitayarishe.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kukutana hapa katika kuendeleza majukumu yetu ya kitaifa.
Pili nichukuwe nafasi ya kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu japo kwa muhutasari juu ya hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili ya mwaka 2014/2015.

Aidha, nachukuwa nafasi hii kumpongeza Kaimu Waziri wa wizara hii iliyokosa bahati kwa muda mrefu, kupata waziri mtendaji wa moja kwa moja. Pia nimpongeze Naibu Waziri kutokana na juhudi zake za kupambana na maswali mbali mbali yakiwa hayana msaidizi wazi katika kipindi chote cha mwaka huu.

Baada ya utangulizi wangu huo Mhe. Spika, nianze mchango wangu katika ukurasa wa 10 wa kitabu kilichopo mbele yetu. Mhe. Spika, katika ukurasa wa 10, naomba ninukuu;

Kifungu cha 2.5 katika kitabu cha waziri;

> " Jumla ya miche 941,176 ya mikarafuu, Unguja 309,640 na Pemba 631,536 sawa na asilimia 94 ya lengo, imeoteshwa na kusambazwa kwa wakulima bila ya malipo, pamoja na kuwapatia wakulima mafunzo ya mbinu bora za uoteshaji wa miche ya mikarafuu, utunzaji na uoteshaji kwa wakulima 300, Unguja 100 na Pemba 200. Aidha, skuli 21 za wakulima wa karafuu, Unguja 8 na Pemba 13 zilianzishwa na zimepatiwa mafunzo".

Mhe. Spika, hili ni jambo jema la kwamba Wizara ya Kilimo na Maliasili imeotesha miche ya mikarafuu yenye idadi hiyo niliyoitaja na ikasambaza kwa wakulima wa mikarafuu. Lakini serikali katika kipindi cha miaka miwili au mitatu iliyopita nyuma iliwatangazia wananchi wanaohusiana na ukulima wa karafuu, waoteshe miche na badala yake serikali itainunua miche hiyo kupitia kwa wakulima hawa wa karafuu.

Mhe. Spika, jimboni kwangu Chamani pale kuna waoteshaji wa miche ya mikarafuu vikundi vingi sana, wameuza ng'ombe zao kwa ajili ya kujiimarisha, wameendelea kuimarisha miche hii ya mikarafuu, lakini hadi leo hii serikali imeshindwa kuinunua miche hii ya wananchi hawa ambao hivi sasa wamekuwa wakisikiliza wito wa serikali. Je ni lini watainunua miche hii?

Wananchi hawa wamepata tabu, wanabeba ndoo za miche ya mikarafuu, wanawake wanabeba mabeseni ya miche ya mikarafuu kwa ajili ya kuatika, lakini matokeo yake serikali imeshindwa kuinunua miche hii. Kwa hivyo, naiomba serikali ituambie ni lini itainunua miche hiyo ya mikarafuu, ili wananchi hawa wajisikie na wao kwamba ile azma ya serikali ya kuendeleza zao la mikarafuu, basi linapitia kwao na kupata tija ya maisha yao ya kila siku.

Mhe. Spika, nikiendelea hapo kuna skuli 21 za wakulima wa mikarafuu zilianzishwa na zimepewa mafunzo Unguja 8 na Pemba 13. Naomba kumuuliza Mhe. Waziri, skuli hizi zilikuwa katika maeneo gani. Mbali ya kuambiwa Pemba na Unguja, lakini tunataka tuambiwe kwamba skuli hizi zilikuwa Chake Chake kwa kule Pemba na walikuwa ni wanafunzi wangapi ambao waliingia katika skuli ile, na ni vigezo gani ambavyo vilitumika kuwapata wanafunzi wa skuli hizi na walisomeshwa wangapi. Pia ni faida gani iliyopatikana katika mafunzo hayo ya wanafunzi wa skuli 21 za wakulima wa zao la karafuu.

Vile vile Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu, niende katika idara ya uendeshaji na utumishi katika ukurasa wa 17. Mhe. Spika, katika malengo ya mwaka 2013/2014, Mhe. Waziri amesema hivi;

"Kuendelea na uhakiki wa mali za serikali zilizokatika wizara na kuzipatia hatimiliki".

Mhe. Spika, hili ni jambo jema na ni jambo zuri kabisa, kwa sababu mali nyingi za serikali zinapotea kwa kukosa udhibiti. Kwa kweli Wizara ya Kilimo na Maliasili katika suala hili nichukuwe nafasi ya kulipongeza sana, lakini wahakikishe kwamba suala hili hawalicheleweshi, kwa sababu Wizara ya Kilimo na Maliasili iko miaka mingi, sasa isiwe tena kila siku inaleta taarifa hii ya kufanya uhakiki wa mali za serikali na kuzipatia hatimiliki.

Mhe. Spika, pia hatimiliki imekuwa ni kikwazo sana katika taasisi zetu za serikali. Sasa mimi najiuliza kwani hizi hatimiliki zinatolewa na nani na kuna kuwa na uzito gani wa kupatikana katika taasisi zetu za serikali.

Kwa hivyo, Mhe. Kaimu Waziri wewe pia ni Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, tunakuomba suala hili la uhakiki wa mali na kuzipatia hatimiliki; suala hili kwa kweli ulipe nafasi ili mali za serikali zijulikane na ziepukane na kuvamiwa na wavamizi ambao kazi yao ni kuzitafuta mali za serikali na kuzifanya mali zao binafsi.

Mhe. Spika, nikiendelea na malengo hayo niende katika nukta moja, mbili, tatu, nne ya tano inazungumza kwamba kuratibu ukusanyaji wa mapato ambayo yanakadiriwa kuwa ni shilingi milioni 748. Hapa ningemuomba Mhe. Waziri anieleze vyanzo vyao vya mapato ni vipi, fedha hizi watazikusanya kupitia wapi na wapi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niendelee na mchango wangu katika ukurasa wa 40, kuhusu Idara ya Umwagiliaji maji. Mhe. Spika, kwa kweli idara hii ni muhimu sana, kwa sababu tumetangaza kilimo kwanza sasa ni lazima tuhakikishe kwamba kilimo kwanza kinafanyakazi, ili wakulima wetu wapewe nyenzo za kutosha pamoja na visaidizi, vyote vinavyofaa katika kuliendeleza suala zima la kilimo.

Mhe. Spika, inasikitisha sana kwamba tumetangaza kilimo kwanza, tumetangaza mapinduzi ya kilimo, lakini bado hatujaona mabadiliko ya mapinduzi ya kilimo, tunaona bado ukulima uko vile vile. Hatuna mazao yoyote yanayoonekana kuongezeka mwaka hadi mwaka, isipokuwa tunachokiona ni ongezeko la maelezo yaliomo katika kitabu. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri katika suala zima la umwagiliaji maji kuna mabonde mengi ambayo yametajwa katika kitabu hiki, kwamba kunatafutwa miundombinu, tunachimba visima vya maji katika mabonde haya. Mimi ningemuomba Mhe. Waziri aangalie vipaumbele vya mabonde mangapi, japo mabonde manne, Pemba mabonde mawili na Unguja mabonde mawili yawezeshwe katika ukulima huu wa umwagiliaji maji, ili wakulima wetu wa maeneo hayo wawe wamekomboka kwa kiasi kikubwa sana na mwaka mwengine tuelekee katika maeneo mengine.

Mhe. Spika, tunapoelezea maendeleo ya kilimo, katika mabonde 10 au 15 kwa wakati mmoja tunashindwa, kwa sababu kila pahali tunafanya kidogo, mradi hauendelei na kilimo kinasita. Mhe. Spika, suala hili namuomba

Mhe. Waziri alipe nafasi kubwa, kwa sababu tunachohitaji sisi sasa hivi ni kujikomboa kweli katika suala zima la kilimo na kwa sababu ya hali ya hewa kuwa na kilimo cha umwagiliaji maji ni jambo zuri na jema. Kwa sababu tunayo mabonde makubwa, yenye maji mengi basi yanataka visaidizi tu endelevu, ili kilimo hiki kiwe hakitajwi tu kwa maneno, bali kiwe kinatajwa kwa kuonekana maendeleo yake.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika changamoto za wizara kwenye ukurasa wa 46. Mhe. Spika, changamoto ya kwanza inasema mabadiliko ya hali ya hewa ni moja ya changamoto kubwa zinazo athiri kilimo; hasa cha mpunga wa kutegemea mvua, kutokana nakutokuwa na miongo isiyotabirika.

Mhe. Spika, huu ni ukweli, lakini wizara hapa inatakiwa ijipange, ili kuwawezesha wakulima hawa mapema. Kwa mfano, kuna baadhi ya maeneo watu wanavuna mapema mpunga ambao unategemea mvua, lakini wizara inachelewa kwenda kuwalimia watu hawa.

Kwa hivyo, naiomba wizara katika suala zima la kushughulikia kilimo kinachotegemea mvua wajipange vyema, ili maeneo haya likiwemo na eneo la Chambani, watu wakimaliza kuvuna tu, wapeleke matrekta, ili watu hawa walimiwe mapema, kwa nini? Kwa sababu watu wanaotegemea mvua ikinyesha mvua wanaendelea kupanda, lakini wanakwenda kulimiwa watu wakati mvua zimeshapita wanapanda na mpunga unaota na baadae unashambuliwa na jua kali na upepo na mavuno yanakuwa hayapatikani.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri ajipange vizuri na watendaji wake, ili kuhakikisha kwamba unapofika msimu wa kilimo wapeleke matrekta watu walimiwe mapema, ili wasubiri mvua ikinyesha wapande.

Mwaka huu wakulima wengi wa maeneo mbali mbali walipata tabu sana kwa kusubiri gari za serikali, kwa sababu gari ni mbovu, wakulima wanasubiri gari hakuna, hali ikiwa hivyo hivyo twende rudi na wakalima katika hali hiyo na waliuwahi msimu wa mvua mapema na mavuno kwa kiasi fulani yanatia moyo, kwa sababu hivi sasa watu wanaendelea kuvuna na mvua zimepita hivi juzi tu, mpunga umechanua katika kipindi cha mvua haukuathirika na upepo wala jua kali.

Kwa hiyo, suala hili namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho, ajitahidi sana katika suala zima la kuwapelekea wakulima wetu matrekta mapema, ili wawahi msimu wa upandaji mapema kuliko kuchelewa.

Mhe. Spika, ameelezea hapa Mhe. Waziri njia za kukabiliana na changamoto hizi ambazo amezitaja hapa. Moja katika njia ya kukabiliana kwake ni mabadiliko ya hali ya hewa, anasema kwamba, ili kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa wizara inatoa msisitizo juu ya kilimo cha umwagiliaji maji wa mpunga na mazao mengine ya juu pamoja na kuendelea kuhamasisha wakulima kuvuna maji ya mvua. Aidha, hatua za uibuwaji wa teknolojia za kilimo na misitu zitaendelea na kuelekezwa katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa. Kwa kweli hili ni jambo zuri na wizara inalitegemea kulitekeleza. Lakini kuna tamko hili ambalo linalosema hivi, pamoja na kuendelea kuhamasisha wakulima kuvuna maji ya mvua.

Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri wakulima hawa amewaandalia miundombinu gani ya kuvuna maji ya mvua, kwa sababu maji ya mvua yanahitaji mahodhi makubwa pamoja na gharama kubwa kwa ajili ya kuyakusanya. Hivyo, mkulima wa Chambani au Kangani ama Mjimbini unamwambia ahifadhi maji ya mvua atayahifadhi wapi ndani ya ndoo kwa ajili ya kukoga, kuwakogesha watoto pamoja na kufulia nguo anao uwezo wa kuhifadhi, lakini maji ya mvua atayavuna vipi kwa ajili ya kilimo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atupe ufafanuzi wa azma hii ya serikali kuwahamasisha wananchi kuyavuna maji ya mvua, ambayo yatawasaidia kwa ajili ya kilimo.

Mhe. Spika, pamoja na maelezo hayo, nasema kwamba siungi mkono hoja hii mpaka Mhe. Waziri atakaponieleza jinsi gani alivyojipanga kuwalimia wakulima kwa wakati unaofaa. Vile vile namna gani alivyojipanga kuwaimarisha wakulima wetu kuvuna maji ya mvua; mvua zinanyesha *Alhamdulillah* kipindi cha mwaka huu, kama kungekuwa na miundombinu endelevu ya kuyavuna maji ya mvua, hivi sasa mabwawa makubwa yangekuwa yamejaa maji na wakulima kwa kipindi kizima hiki, kwa sababu mvua zilikuwa ni nyingi na bila ya shaka maji yangekuwa ni mengi ya kutosha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa mchango wangu huo naomba kutoa shukurani zangu kwa kunipa nafasi hii na ahsante sana, nitaunga mkono baada ya kupata majibu yangu. *(Makofi)*

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia katika Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili. Vile vile nitoe shukurani zangu kwa Mhe. Kaimu Waziri wa wizara hii pamoja na watendaji wote wa wizara hii kwa jitihada wanazozifanya katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inaingia kwenye yale mabadiliko makubwa ya kilimo.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu hautakuwa mkubwa sana lakini nina mambo mawili matatu ambayo nimeyaona kidogo nilikuwa nahitaji niweze kupata ufafanuzi. Kwanza nianze na kitabu hiki ukurasa wa 8, taarifa ya utekelezaji wa mwaka kwenye mapato na matumizi. Mimi nilikuwa naangalia pale kwenye makusanyo ambapo wanasema, "Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka fedha 2013/2014 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 748 milioni", lakini ilikusanya zaidi kama shilingi 856,180,640 sawa na asilimia 114. Sasa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie yale makisio ambayo tuliyakisia na mpaka tukaweza kuvuka tukafika huku labda yalichangiwa na kitu gani. kwamba tumejikisia hiki na Baraza liliidhinisha makisio haya ya makusanyo lakini wizara tuseme kwa jitihada zao, sasa tunaomba ule ufafanuzi wa namna ambavyo walifanya.

Ukiangalia kwenye makusanyo ambayo wanayatarajia kuyakusanya katika kipindi hiki cha mwaka 2014/2015 ni shilingi 845 milioni. Kimahesabu hapo ukiangalia makusanyo ambayo waliyatarajia mwaka jana walivuka lengo, lakini mara hii inaonekana wamejipangia kidogo zaidi ili waweze kuvuka lile lengo tena. Kwa sababu hizi shilingi 845 milioni wameshazivuka mwaka huu uliopita, sasa hebu wanipe kigezo wanachotumia katika kupanga au kujiwekea haya makadirio. Maana kama umeshavuka bila shaka utahitaji wende mbele zaidi, lakini naona wao kama wanarudi nyuma. Sasa hii kidogo imenipa wasiwasi.

Baada ya hapo nisogee mbele kwenye kitabu chake hiki ukurasa wa 17 kwenye Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Nikiangalia kwenye yale malengo ya mwaka uliopita niende kwenye utekelezaji, kuna kifungu cha mafunzo kwa Bodi ya Zabuni na Kitengo cha Manunuzi hayakufanyika.

Mhe. spika, nilikuwa nataka kujua ni kwa nini mafunzo haya hayakufanyika na mafunzo haya ni muhimu sana. Kwa sababu moja kati ya matatizo ambayo tunayapata katika taasisi zetu hizi ni namna ya bodi hizi au kitengo hiki cha manunuzi kinapokuwa kiko *weak*. Hapa ukiangalia katika Wizara ya Kilimo na Maliasili kuna manunuzi mengi ya mbolea, pembejeo na vitu vyengine, kama itakuwa mafunzo hayafanyiki maana yake zile shughuli hazifanyiki kwa ufanisi.

Kwa hivyo, nataka kujua ni nini tatizo lake wakashindwa kutoa mafunzo kwa bodi hizi ili iweze kufanya kazi zake vizuri, kwa sababu tulishakwenda pale kukagua na tukakuta kuna tatizo hili. Sasa kama hawakufanya haya ina maana lile tatizo litakuwa linaendelea.

Mhe. Spika, ukiangalia katika taasisi nyingi hata katika michango yetu ya bajeti ya mwaka jana katika wizara hii tuligusia juu ya kuweko na mali nyingi sana chakavu na vitu vyengine, na tukaiagiza wizara kwamba iziorodheshe na kuweza kuhakikisha kwamba ndani ya mwaka ule wanaziondosha.

Sasa kitengo hiki ni kazi yake moja hiyo, lakini inaonekana hapa kama hakikuweza kuwezeshwa kitengo hiki maana yake hiyo kazi haikutendeka. Pia nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja atuambie katika lile zoezi zima la kuorodhesha zile mali na kuziandikia kuwapelekea watu wa uhakiki mali, ili waweze kuziondosha kwa utaratibu lilifikia wapi.

Mhe. Spika, nizungumzie kwenye suala la upimaji wa mashamba. Mwaka jana tulilizungumza sana hapa namna ya mashamba ya wizara hii yanavyopotea; yanapotea kutokana na kutokuwa na hatimiliki wizara yenyewe. Tulilipigia kelele sana na tukaiagiza wizara kuhakikisha kwamba inafanya jitihada kuhakikisha mashamba yote inayapima na zile nyumba ambazo wanazo, maana wizara hii inazo nyumba pia tuliiagiza iziwekee hatimiliki.

Nadhani ni vyema atakapokuja Mhe. Waziri, atusaidie katika lile zoezi zima la kuyapima mashamba, ingawa hapa wameandika lakini mimi sikuridhika na haya maelezo, mashamba ni mengi mno lakini hapa yameorodheshwa kama mashamba mawili matatu, wanasema na la Cheju linaendelea kupimwa lakini haya yako mengi sana.

Sasa tunataka kujua lile zoezi hasa wameshapima mashamba mangapi na hayo ambayo hayajapimwa kwa nini mpaka sasa hivi, wakati yeye waziri ambae anakaimu wizara hii ndiye yeye Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na

Nishati ambae hati za mashamba zinatoka kwake. Mimi nafikiri ingekuwa kitu chepesi sana akilikusudia hasa hawezi kutumia hata miezi miwili kwa zoezi hili kwa sababu anapiga ngoma zote mbili yeye mwenyewe.

Kwa hivyo, anapiga na huku anacheza, sasa ilikuwa ni rahisi kwake kuwaagiza watendaji wake kutoka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwenda kupima na kutoa zile hati, lakini kama mpaka leo wanakwama waziri mmoja ambae anakaimu wizara hii na huku ndiye Waziri wa Ardhi, kipi kinamshinda mpaka leo kuhakikisha mashamba haya wanayapima na yanapata hatimiliki.

Jengine nije kwenye ukurasa wa 20 wa kitabu cha Mhe. Waziri kwenye Idara ya Kilimo. Kwenye idara hii nimepata mashaka kidogo, nimejaribu kuangalia kwenye kitabu kikubwa hiki cha makadirio, nikiangalia fungu 1501 la Idara ya Kilimo kuna fungu la ruzuku 263167 ambapo ni Huduma za Kilimo Mikoani au Mkoa wameandika lakini najua wamekusudia mikoani. Hapa ndio penye bajeti ya wakulima wetu maana serikali hapa ndipo inapoingiza fedha kwa ajili ya wakulima wetu ikiwa ni matrekta na mbolea na vitu vyengine.

Mhe. Spika, bajeti ya mwaka jana ilikuwa ni shilingi 3.4 bilioni hivi, lakini kwa mwaka huu imeshuka sana mpaka shilingi 2.2 bilioni na huku ndio tunaiona serikali inasema inaweka mkazo au kipaumbele kwenye kilimo ili wananchi wetu waweze kujikomboa. Sasa mimi nilikuwa nataka kujua tu kwa bajeti hii Mhe. Waziri aliyotuwekea hapa hivyo ndio tutakuwa tunakiendeleza mbele hicho kilimo au tunarudi nyuma.

Naomba atakapokuja Mhe. Waziri kufanya majumuisho hapa anisaidie maelezo ya kutosha, ili niweze kuridhia *otherwise* nitaondosha fungu jengine huko nije nichomekee hapa angalau wakulima wetu waweze kupata zaidi.

Kwa kweli tuna tatizo la wakulima wetu kutokupata matrekta kwa wakati na wakati mwengine matrekta yapo unaambiwa mafuta hamna, wakati mwengine trekta lipo lakini unaambiwa limeharibika kuna kipuri kinatakiwa, hakuna fedha. Hapa kuna tatizo kwa hiyo, bajeti hii sijaridhika nayo Mhe. Waziri, nataka maelezo ya ziada maana hizi fedha ambazo zimekatwa hapa ni nyingi mno. Sasa tuone namna ambavyo mwaka jana tulikuwa na 3.4 bilioni na mwaka huu kuna 2.2, sijui kwa sababu gani tukazipunguza kiasi hiki.

Mhe. Spika, mwisho niingie kwenye vifungu kidogo, ambapo baadhi ya vifungu ninahitaji maelezo nianze kwenye kifungu cha Idara ya Uendeshaji na Utumishi fungu 1301, niende kwenye vifungu vidogo vya 211100 malipo ya likizo, 211104 posho maalum, 211110 posho la vikao na kamati 211116 na posho la baiskeli 211117, naomba maelezo juu ya matumizi ya mafungu haya naona kidogo hayako sawa.

Vile vile nisogee kwenye gharama za safari, yaani safari za ndani na nje 220301 na 220302 pia na hapa ninaomba maelezo mazuri ya matumizi haya, kwa sababu haya mafungu ya safari yako mengi mno humu na kila idara imeekewa mafungu ya safari mengi wakati hapa pia yapo mengi sana.

Hata hivyo, kwenye matengenezo ya ofisi 220700 hapa naomba maelezo kwenye matengenezo madogo ya ofisi kifungu 220701 na matengenezo makubwa ya majengo 220702, maana haya yote ni matengenezo, lakini yote yameekewa fedha. Sasa kama kuna haya matengenezo makubwa, haya madogo ya kazi gani! Kwa sababu unapofanya matengenezo makubwa hakuna haja ya kufanya matengenezo madogo ndio umeshayafanya, kwani hayo makubwa ndio yanayochukua na hayo madogo ndio yamo kwenye hayo makubwa.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atusaidie kidogo kutupa ufafanuzi katika hili.

Baada ya hayo, Mhe. Spika nimalizie hapo na ninakushukuru na wala sitaweza kuunga mkono bajeti hii kwanza nipate maelezo na baadae nafikiri Mhe. Waziri baada ya kuniridhisha kuhusu wakulima wangu namna ya fungu hili lilivyo, naweza kumuachia bajeti yake. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa nimkaribishe Mhe. Salim Abdalla Hamad na baadae Mhe. Mohmmed Haji Khalid.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kidogo katika bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, kwanza kwa sababu ya uzito wa bajeti hii na wizara yenyewe ilivyo, namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili apone haraka, awe na afya njema na aweze kutekeleza majukumu yake vilivyo, kwa sababu ni wizara inayogusa moja kwa moja uhai wa wananchi. *(Makofi)*

Nianze mchango kuhusu mwelekeo wa bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili mwaka 2014/2015 kwenye ukurasa wa 6 kifungu 1.18. Mhe. Spika, kifungu hiki kinaeleza kuwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili itaendelea kusimamia na kutekeleza malengo ya Dira ya 2020, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010/2015 Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA II), malengo ya *millennium MDG*, Mipango na Mikakati ya Kisekta pamoja na Mipango ya Mageuzi ya Sekta ya Kilimo (*ATI*).

Mheshimiwa haya ni mambo mengi na yote yameelekezwa kuwa wizara hii itasimamia na kutekeleza shughuli zake kwa kufuata misimamo hii, ni mengi na ninaamini kila mmoja ina maelekezo yako ndio ikawekwa mingi hapa.

Kwa hivyo, ningelimuomba Mhe. Waziri anieleze kwa urefu hasa wala asione tabu ni vipi wizara yake kwa kupitia serikali, itaendelea kusimamia na kutekeleza malengo yake kwa dira ya 2020, ni vipi hiyo ilani ya chama ya uchaguzi ya CCM 2010/2015, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini na malengo ya *millennium* pamoja na mpango wa mkakati wa kisekta pamoja na mambo ya mageuzi ya kisekta ya kilimo kama ilivyoelekezwa yatatekelezwa. Naomba kila moja aniambie inaeleza nini, kwa sababu naona ni mambo yanatajwa tu lakini mimi nimeshindwa kuyaunganisha. Hilo ni moja.

La pili, Mhe. Spika, niende kwenye changamoto inazozikabili wizara hii na imeeleza kuwa ingawa sekta ya kilimo imeendelea kukua hata hivyo ukuaji huo umekuwa mdogo kufikia kiwango kilichowekwa katika MKUZA II cha asilimia 6. Mhe. Spika, miongoni mwa changamoto zinazoikabili sekta hii ni pamoja na utegemezi mkubwa wa kilimo cha kutegemea mvua. Kwa hivyo, kabla sijenda katika nyengine ni kwamba tunajua tokea zamani wakulima wetu wanalima kilimo hiki cha kutegemea mvua na sasa ikiwa ni changamoto iliyoikabili wizara hii. Kilimo hiki cha kutegemea mvua tukiangalia ukurasa wa 10 wa kitabu hiki, inaeleza kuwa Wizara ya Kilimo na Maliasili imeongeza zana za kisasa kwa lengo la kuimarisha ukulima wa mpunga wa kutegemea mvua, na jumla ya matrekta 20 mapya yamenunuliwa kwa kuweza kusaidia kazi za uzalishaji wa mpunga.

Sasa huku ni changamoto halafu huku anasema kuwa wanaimarisha. Kwa hiyo, Mhe. Spika, kwa nini mahala tumeshaona kuwa ni changamoto ambalo halimo katika uwezo wetu, tusitafute njia mbadala ya kuona kilimo kinaendelea bila ya kujali kuwa kuna changamoto na sisi tukatafuta njia nyengine, badala yake tukaja tukasema kuwa tutazidisha kilimo kule kule tuliko-*fail*. Kwa hivyo, na hili naliombea maelezo.

Mhe. Spika, halafu tukifungua ukurasa wa 46 huku kuna changamoto za wizara na moja ni mabadiliko ya hali ya hewa ikiwa ni moja ya changamoto kubwa ya kilimo, hasa cha mpunga wa kutegemea mvua kutokana na kutokuwa na miongo inayotabirika. Sasa ikiwa mambo yenyewe ni haya kwa hiyo huu mpango wa kukuza kilimo hiki una faida gani badala ya kutafuta njia mbadala, ili tuone kuwa watu wetu wanapata kilimo cha kutosha, wanavuna, tunauza nje na mashaka ya njaa yanaondoka na tunaingiza fedha za kitaifa za nchi kwa kupunguza uagizaji wa chakula kutoka nje ya nchi.

Mhe. Spika, nikiendelea jengine ambalo linaathiri sana au ni changamoto kwa wizara ni mabadiliko ya hali ya hewa, hili hatuna mamlaka nalo lakini kuna hii miripuko ya maradhi, wadudu waharibifu wa mazao na upungufu wa rutuba katika maeneo ya kilimo na uwekezaji mdogo wa sekta binafsi. Sasa Mhe. Spika, mimi hapa ninaloomba kuelezwa ni kuwa moja kati ya kazi kubwa ya wizara hii tunajua kwamba kuna maradhi, sasa ikiwa kuna uharibifu mkubwa sana wa kilimo chetu kutokana na maradhi, ningeliomba kujua hayo ni maradhi ya aina gani kati ya yale mbali ya asili tuliyonayo na wizara imechukua hatua gani kuona kuwa maradhi haya yameondoka na hayarudi tena.

Halafu ni wadudu gani ambao ni waharibifu wa mazao na upungufu wa rutuba. Sasa kuhusu rutuba Mheshimiwa sisi tunajua tunalima na serikali inajitahidi kutoa mbolea ya bure na ikiwa kuna upungufu wa rutuba hii, mbolea inasaidia nini kwa sababu mbolea inapotumiwa ndio inatia rutuba katika ardhi. Watu wanaendelea na kilimo chao vizuri. Kwa hiyo, ikiwa kuna upungufu wa rutuba upungufu huu ni wa maumbile, au unasababishwa na ukulima mbovu wa watu au kuna kitu gani. Naomba tupate maelezo ya rutuba ikiwa ndio muhimu katika kilimo, vipi wizara imejipanga kukabiliana na upungufu huo.

Jengine Mheshimiwa ninalopenda kuzungumza ni kuhusu kilimo cha maweni; katika fahamu zangu hapo zamani kilimo cha maweni kilikuwa kinaimarika sana. Kweli kweli kulikuwa na uwele wa kutosha, kulikuwa na viazi vikuu vya kutosha, pilipili hoho zilikuwa zikiuzwa nchi za nje, pamoja na mengi yanayohusiana na hayo.

Lakini kwa mujibu wa maelezo haya ni kuwa wizara inaeleza kwamba pamoja na jitihada nyingi ilizochukua wizara bado kilimo cha maweni hakijapiga hatua yakuridhisha. Nimeeleza kuwa wakulima wengi wa ukanda huu wana uzoefu mkubwa katika uzalishaji wa mazao ya mbaazi, mtama, uwele, viazi vikuu, ndimu, pilipili hoho na kadhalika kama mazao ya chakula na biashara.

Sasa ni kwa vipi mpaka sasa hivi kuwa kilimo hiki hakijaimarika au hakijapiga hatua ya kutosha. Je, tunaamini maweni ni kwahala kwenye ukame wakati haya ni mazao ambayo yanastahamili ukame. Kwa hiyo mpango mbovu wa wizara katika kusimamia wananchi au kuna lipi lilojitokeza mpaka ikawa kilimo cha maweni hakijaweza kupiga hatua inayoridhisha hasa kutokana na hatari tuliyonayo katika kisiwa chetu watu wanaongezeka, ardhi ya kulima inajengwa, na hatimae sehemu ya kulimia inapunguzwa.

Kwa hivyo, ili kuweka mambo sawa ni lazima tuwekeze zaidi katika upande wa kilimo cha maweni. Sasa ikiwa kuna hili tunaomba kujua ni sababu gani na wizara hasa imejipanga vipi katika kulishughulikia suala hili.

Pia wizara inasema kuwa itaendelea na utafiti wa kilimo cha maweni kwa kushajihisha kilimo mseto na kuhamasisha utunzaji wa mazingira. Kilimo mseto hiki ni kwa aina hii hii ya kilimo au katika utafiti wao wana kilimo chengine kitakachofaa kulima maweni, ili zao la chakula liweze kuongezeka, na hilo pia naomba nipate maelezo.

Pia wizara inasema kuwa juhudi za kuwaendeleza wakulima wa maweni kwa kuwapatia kazi mbadala za kiuchumi hasa ufugaji wa nyuki zitaendelea zaidi. Kazi mbadala maana yake ni kubwa badala ya kilimo sasa wafuge nyuki. Je, hiyo asali ndio itatutosha sisi kuweza kupata chakula cha kutosha? Maana Mhe. Waziri ukiweka mbadala maana yake ni kuwa kile sasa kikiondoka kitakuwa kinawakilishwa na hiki. Sasa hiyo asali tuseme ipatikane iwe nyingi na kadhalika itatusaidia nini, sisi tunataka kula, tunataka kuuza nje lakini mimi ushauri wangu sipingi kuwa wasijikite katika hili, lakini pia wahakikishe kuwa kilimo cha maweni kimeshughulikiwa vilivyo na tija inapatikana.

Jengine Mheshimiwa ni kuhusu maliasili. Mhe. Spika, wizara imeeleza kuwa kwa upande wa maliasili wizara inaendelea kushajihisha jamii katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili katika maeneo ya hifadhi na ya wananchi. Pia inathamini mchango mkubwa unaotolewa na jumuiya hizo kwa kuhifadhi maliasili na kubuni mbinu mbadala za kupunguza uharibufu wa rasilimali za misitu. Naipongeza wizara kwa hili lakini itilie mkazo sana ijue umuhimu wa misitu iliyokuwa ni ya asili na pengine hata japokuwa si asili, wakati inaweza kumea hapa haileti athari yoyote inasaidia rutuba katika nchi, inasaidia kusafisha mazingira, kuondoa gesi ukaa na pia palipo na miti hapakosi mvua itarutubisha nchi yetu, hiyo naunga mkono sana.

Mhe. Mwenyekiti, lakini haya maelezo aliyoyaeleza huku mwisho kubuni mbinu mbadala za kupunguza uharibu wa rasilimali za misitu. Mbinu mbadala mimi nahisi ilibidi nipate maelezo kwa sababu ninavyojua moja katika njia inayosababisha misitu yetu kupungua ni kwa sababu ya uchongaji, upigaji mkaa mkaa, kutafuta kuni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na hii kutokana na hali ya umasikini ya jamii ilivyo naona ni kitu cha muda mrefu. Sasa ni mbinu gani mbadala wao wataifanya na hii nayo Mheshimiwa naomba maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ninalopenda kuzungumza ni kwamba kilimo ndio uti wa mgongo na ndio tegemeo la maisha yetu, na kilimo kadri ya siku zinavyokwenda mbele kuna mabadiliko ya tabianchi, tunahitaji kupata mabadiliko ya mbegu ambazo zitaenda na wakati unaohusika; haya ni mambo ya kitaaluma. Kama mbegu fulani haiwezi kumea kwa sababu ya mabadiliko ni kazi ya wizara kutumia wataalamu wake kuona kuwa tupande mbegu gani mbadala, ili wananchi waweze kupata chakula wasipoteze nguvu zao bure.

Kwa hivyo, hii kuagizia mbegu kutoka Bara na sehemu nyengine zikaja zikapandwa tu hapa na tunajua siku zote unaweza ukachukua kitu ukaona kwamba sasa hapa tutapata faida ukaweza kupata kwa mazao ya mara ya kwanza na mara ya pili, halafu tena unapoendelea ikawa ni mashaka matupu. Kwa hivyo, naomba kujua wizara imefanya utafiti gani wa mbegu watakazoziingiza kuwa hapa zitakuwa endelevu kutokana na hali ya mabadiliko yalivyo na huko zinakotoka, na hapa zinapoletwa ni sehemu yenye ardhi tofauti.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu tumezoea kusifu mbegu hapa na kuzipigia debe lakini ikifika siku mbili tatu si kwenye wanyama wala kwenye kipando, mbegu zile haziwezi zikaendelea kuzaa. Mfano, tulikuwa na mpunga wa *nerika* ulisifiwa sana kweli kweli kupita kiasi, tena tukaona sisi ishakuwa mkombozi, lakini kwa bahati mbaya tumeona athari yake ni sehemu chache zinaoota na masharti yake ni makubwa na sehemu nyengine masharti haya hayawezi kutimizwa maana yake ni kukosa mazao.

Jengine Mheshimiwa naomba nifungue kiambatanisho Nam. 1 ambacho kiko ukurasa wa 51…

Mhe. Spika: Una dakika tano.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kutokana na kiambatanisho hiki kinachoelezwa takwimu za uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa tani kuanzia mwaka tokea 2008 mpaka 2013, naomba kupata maelezo yafuatayo, kwa sababu hapa tuna wataalamu wanipe sababu.

Tuangalie kama kilimo cha mtama mwaka 2008 tulianzia kwa tani 610 tu, lakini 2009 zikapungua mpaka tani 457, nataka kujua ilikuwa ni sababu gani badala ya kuongezeka ikawa zinapungua. Lakini ilikwenda mpaka mwaka 2012 zilikuwa tani 484, mwaka huu ambao tunaambiwa kuwa kilimo kimekuwa 2013 ni tani 225.53. Naomba nipate maelezo hasa hii wizara kama inafuatilia kweli mambo ya kilimo mabadiliko haya yanatokana na nini na wanajipanga vipi kuona watu wanaolima mazao haya yanaendelea kukua.

Mhe. Spika, jengine ni mpunga ambao ni zao letu muhimu sana; hii nashukuru tukiangalia mwaka 2008 kulikuwa na tani 20.8 zikaja 26, zikaja 21, zikaja 23 mpaka 2012 zikawa 6 tu. Kwa hivyo, tani 6000 kutoka 23 mwaka 2011 mpaka zikafika 6 zilisababishwa na nini tupate sababu na walijirekebisha vipi mpaka tukapata tani 33,655 katika mwaka huu 2013.

Mhe. Spika, zao jengine ambalo ni muhimu sana ni zao la muhogo, muhogo ndio chakula chetu kikubwa; ndio chakula cha kimasikini hakina gharama kubwa ya ushughulikiaji, lakini nacho mwaka 2012 kulikuwa na tani 192,00072.68 lakini mwaka 2013 kulikuwa na tani 164,000 ilipungua sana, hata huu muhogo nataka kujua ni sababu gani.

Vile vile Mhe. Spika, jengine ni ndizi ambacho tunajua ndio chakula chetu kikubwa. Vile vile kwa kupunguza wakati tulianzia kwa tani 1,8300 kwa mwaka 2008 mpaka tukamalizia tani 68,357.6 kwa mwaka 2013, nataka kuelewa ni sababu gani? Kwa maana haya pamoja na mengine nayaacha kutokana na wakati. Mheshimiwa kama wizara ambayo ina Idara ya Utafiti ikiona kuwa zao muhimu linapungua, hawakujua sababu ikawa wakaweka sawa katika hali ilivyo. Hii inaonesha kuwa utafiti uliomo humu ni wa kitabu tu, si wakuhusika katika mashamba moja kwa moja. Kwa hivyo, naomba nipate maelezo hayo ili niridhike kama kweli wizara inafuatilia takwimu zake.

Mhe. Spika, mwisho namalizia kwa kusema kuwa tunao watalii wengi na sisi wenyewe tunayo mahitaji ya lazima, katika uzoefu wangu mboga mboga zinaota wala hakuna aina ya mboga mboga zilizokuwa hazioti. Lakini tukiangalia mboga mboga pamoja na tungule, nyanya chungu na kadhalika tunaagizia sana kutoka nje, wakati kwetu zinaota. Kwa hivyo, ningelimuomba Mhe. Waziri zaidi ya malekezo aliyoyaweka hapa atwambie kwa nini wakati mazao haya yanaota na yatasaidia sana kukuza soko katika nchi yetu, ikawa haishughulikii na badala yake tunaagizia kutoka nje. Mheshimiwa nashukuru.

Mhe. Spika: Nimuombe radhi kidogo Mhe. Mohammed Haji Khalid nilimruka Mhe. Mgeni Hassa Juma kwa hiyo aanze yeye Mhe. Mgeni na baada ya hapo Mhe. Mohammed Haji Khalid ambapo atafuata Mhe. Salma Mussa Bilali.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii yakuweza kuchangia hotuba ya Wizara ya Kilimo na Maliasili. Awali ya yote Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia kufika hapa leo tukiwa wazima wa afya.

Mhe. Spika, nitakuomba radhi kidogo sauti yangu haiko sawa kwa sababu ninaumwa na mafua, kwa hiyo na hata katika uchangiaji wangu hautokuwa mkubwa kwa sababu ya hali yangu ya kiafya.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Kaimu Waziri ambae ametuwasilishia hotuba hii, lakini nimpongeze vile vile Naibu Waziri mwanamke mwenzangu ambae kwa kweli kwa uhodari wake na umahiri wake tumemuona uwezo wake mzuri, anavyochapa kazi ambayo amekabidhiwa. kwa hiyo nimpongeze sana. Vile vile niwapongeze watendaji wakuu akiwemo Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi na Maafisa mbali mbali kwa kazi waliyoifanya katika kipindi cha 2013/2014.

Mhe. Spika, mimi nitazungumzia ukurasa wa 4 ambao unazungumzia suala zima la hali ya uzalishaji. Mhe. Spika, nimeona kwamba inasema kuwa kutokana na kiwango ambacho kilichokuwa kinatarajiwa kutoka kwa MKUZA II kwamba kilimo kitakuwa kwa kasi kubwa, lakini sasa tatizo limejitokeza kwamba wanasema hapa

wakulima wengi wanategemea kilimo cha mvua na kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na miripuko ya maradhi mbali mbali. Lakini katika kurasa mbali mbali Mhe. Spika, nimeona kwamba Wizara inajitahidi katika kuelimisha pamoja na kuajiri vijana kwa ajili ya kuweza kuwasaidia wakulima katika maeneo mbali mbali.

Sasa Mhe. Spika, mimi nilikuwa ninajiuliza suala la kwanza ambalo ninajiuliza na Mhe. Waziri nitamuomba sana anisaidie kunijibu, nataka kujua hivi umeshafanyika utafiti wa kujua kwamba idadi ya mashamba yote katika kila Wilaya. Hilo nilikuwa naomba sana nipate kujua ni aina ya kilimo katika mashamba hayo, hilo vile vile nilikuwa naomba Mhe. Spika, nilijuwe.

Nasema hivyo kwa sababu Maafisa tunao katika Wilaya lakini sasa maafisa wale unaona muda mwingi wanakuwa hawana la kufanya. Sasa laiti ingelikuwa kwamba wanajua kazi yao na wanajua wapi wende wakulima gani wanawahitaji, wana ratiba maalum kwa ajili ya kutembelea, mimi ninaamini kwamba kwa hakika kilimo chetu kingekua maradufu. Hili amelizungumzia hata Mhe. Mohammed kwamba leo tunasema kwamba mvua inakuja lakini na kuna suala zima la elimu ya *water harvesting* ile ya kuvuna maji.

Sasa kwa bahati mbaya wakulima hawajui na hatuwezi ku-*assume* tunaandika tu kwenye vitabu lakini hatuwezi kufikiria kwamba wakulima elimu hii wataipata tu. Kuna elimu chungunzima ambayo wakulima wanaihitaji, kwa kweli tunaona bado haijawafikia kwa sababu wataalam na watendaji wa Wizara bado hawajaweza kuwafikia wakulima na kuweza kuwaelimisha ndani ya maeneo yao. Kwa hivyo hilo ninaliuliza ni muhimu sana.

Vile vile ninauliza hawa maofisa wa kilimo kweli wanapewa uwezo wa kuwafikia wakulima, kwa sababu wapo ndani ya wilaya lakini kama hawana uwezo, kama hawatapewa vipando, kama hawatapewa miongozo ya kazi zao ambazo wanazifanya Mhe. Spika, tutakuwa tunadanganyana hapa. Elimu ni muhimu sana kwa wakulima wetu. Lakini wakulima sio wao wawafuate, kwa sababu mimi ninashukuru *alhamdu lillahi* kidogo ninajua. Kwa sababu na mimi kidogo ninalima ni mkulima vile vile ingawa ni mtu wa mjini.

Mara nyingi sana sisi ndio tunaowafuata Maafisa kwenye masuala ya ufugaji, lakini kwenye masuala ya kilimo unamtafuta. Lakini yeye kumtafuta mkulima hicho kitu hakifanyiki au ni mara chache sana. Labda wana mashamba yao maalum wanafanyia kazi, lakini katika maeneo mengine hawafiki. Mhe. Waziri hilo ninakwambia.

Nikimaliza hapo Mheshimiwa kama nilivyosema michango yangu sio mingi sana nakwenda katika ukurasa unaozungumzia masuala ya misitu na maliasili. Mhe. Spika, mimi ninafahamu misitu na mali ya asili, maliasili ni pamoja na wanyama wetu ambao wamo ndani ya misitu ile. Humu sikuona chochote kilichozungumzia kuhusu suala la wanyama wetu ambao tulionao ndani ya misitu. Mhe. Spika, ninasikitika kwa hilo, tuna wanyama ambao na tumekua na misitu ambayo tunaitumia katika utalii lakini inavyoonesha kwamba hawa wanyama hatujawatia kwenye hesabu ya mali ya asili. Sasa mimi ninajiuliza hivi hawa wanyama tulionao kama kimapunju, tuna paa nunga, tuna maguruguru, tuna ziwarde, kuna ndege aina ya minana na wengineo, hawa hesabu yao nani anawashughulikia? Kama ikiwa humu kwenye kitabu hiki hawamo na ni masuala ya misitu, hawa wanakaa misituni jamani.

Mhe. Spika, mimi imenisikitisha sana kilichojitokeza hapa ni kwamba ni suala zima la ile mitego ya kunguru zaidi ya hapo sijaona kitu chochote. Sasa Mhe. Spika, mimi ninaiomba Wizara hii au kwa ujumla serikali ijipange katika kuhakikisha kwamba hawa wanyama ambao wamo ndani ya misitu yetu wanahifadhiwa na wanatiwa katika hesabu ya mali ya asili.

Mhe. Spika, wenzetu nchi nyengine wanafufua wanyama ambao wamo ndani ya asili kwa ajili ya kusaidia katika kuendeleza masula ya uchumi wa nchi zao. Tuna wanyama chungunzima, tuna ndege wengi lakini leo wamepotea hakuna anayejali. Mhe. Spika, mimi ningeomba sana na ninafikiria Wizara hii inaweza sana kushirikiana na Wizara ya Utalii kwa ajili ya kuangalia viumbe hivi ambavyo vitaweza kutusaidia katika kukuza uchumi. Tunataka leo watalii wakija hapa licha ya kuja tu kwenye masuala ya fukwe zetu, lakini waje watizame wanyama wenye asili tofauti ambao huko kwao hawapo. Mara moja atakuja atakaa kwenye *beach* na mara nyengine ili tuwarudishe watalii wetu. Leo tunalia kwamba watalii hawaji kama tunavyotegemea kwa sababu hiyo hakuna *diversity.* Lakini wanyama wa asili ni muhimu, sasa ikiwa humu ndani ya kitabu hawamo ina maana kabisa hawa hawana maana; kimapunjua hawana maana kweli. Mhe. waziri naomba hilo uje unijibu kwa nini wanyama wa asili hawajaorodheshwa, kama sio idadi lakini hata hawajazungumziwa namna gani wanahifadhiwa katika Wizara hii.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache maomba niseme tu kwamba Mhe. Waziri, anijibu masuala yangu na baada ya kunijibu nitaunga mkono hotuba hii. Mhe. Spika, ninakushukuru sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kutoa mawazo yangu mafupi kuhusu Wizara hii ya Kilimo na Maliasili. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha asubuhi kufika hapa kuendelea na kazi zetu za kawaida. Kadhalika nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi na nimpongeze Kaimu Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri kweli kweli, kwa sababu mpaka sasa hivi hajatokea Waziri aliyeweza kuwasilisha hotuba yake kwa kasoro ya saa moja.

Kwa hivyo kafanya vizuri sana Kaimu Waziri, lakini huyu Kaimu Waziri ni Kaimu wa Wizara au ni Kaimu wa kitabu cha bajeti. Kama Kaimu wa Wizara ningeomba anieleze ni mara ngapi kenda Wizara ya Kilimo kuzungumza na Maofisa wa Kilimo kule Wizarani au popote pale. Kama ni kaimu wa bajeti ni sawa sawa, kama ni wa Wizara ningeomba maelezo yake.

Mhe. Spika, mimi nianze mchango wangu kama nilivyosema mfupi kwa hali ya uzalishaji, humu imezungumzwa kuwa kumekuwa na ongezeko la uzalishaji kwa baadhi ya mazao kwa mwaka huu unaomalizika ukilinganisha na mwka uliopita kwa baadhi ya mazao. Pia kulikuwa na upungufu kwa baadhi ya mazao mengine. Kwa kuwa Mhe. Spika, mazao yote haya yanategemea hali ya hewa ya aina moja, ningependa kujua yale yaliyoongezeka ni kwa sababu ipi iliyopelekea iongezeke na yale yaliyopungua ni sababu zipi za msingi zilizofanya yapunguwe.

Halafu hivi vipimo Mhe. Spika, kuwa kuna tani kadhaa ukiacha karafuu ambazo tunapeleka sokoni kuuzwa lakini muhogo, viazi na mpunga mimi ninalima mpunga na nimepakana na bibi Fatma Ali, tunapovuna mpunga wetu tunapeleka nyumbani wala hakuna ofisa yeyote anayepita kuupima. Sasa haya makisio Wizara ya Kilimo wanayapata wapi ya kujua muhogo ni tani kadhaa, mpunga tani kadhaa, viazi tani kadhaa au wanakisia mara hii mavuno mazuri tufanye hivi, mavuno kidogo tufanye hivi, ingawaje haya ni makisio, lakini ule utaratibu wanaoupata ni upi.

Halafu Mhe. Spika, wanapima wanataja kwa tani, nadhani vizazi vipya hilo neno tani hawalijui. Kwa sababu hivi ni vipimo vya *british system* ambao sasa watu wanakwenda kwenye *metric system*. Je, hawa watu wanajua kuwa tani moja ni kilo ngapi kwa sababu mimi ninajua tani ni ratili ngapi. Je, hawa watu wanaofanya hivi wanajua kuwa tani moja ni kilo ngapi? Kwa sababu tani si kipimo cha kilo ni kipimo cha ratili.

Mhe. Spika, mimi nianze kwa Idara ya Umwagiliaji Maji na hapa nina jambo moja tu dogo; katika jimbo la Mtambile liko bonde Kwa Machigi ambalo ni la umwagiliaji maji na Mhe. Spika, ukiacha bajeti ya mwanzo ya Baraza hili linaloendelea ya mwaka 2011/2012 bajeti zote zilizobakia 2014/2013, 2013/2014, 2014/2015 zinataja kuingizwa umeme katika kisima. Bajeti zote tatu zinataja, lakini hizi mbili za nyuma hakuna kilichotendeka mpaka katika malengo ilikuwa inaingizwa kuwa itajumuishwa. Mwaka 2012/2013 iliingizwa kuwa utawekwa umeme kimya, 2013/2014 imemalizika hii sidhani kwa siku 10 zilizobakia kuwa watakwenda kuweka kimya kimya. Mwaka 2014/2015 wameingiza. Kwa hivyo hapa Mhe. Spika, nitakuwa mgumu kweli kweli kwa Wizara hii hadi wanithibitishie kweli kweli, ni lini umeme utawekwa pale ili bonde lile lianze kutumika.

Kwa sababu miundombinu takriban yote imekamilika na pesa nyingi sana za serikali pamoja na wafadhili mimi nimekwenda mara moja pale. Wamekuja watu kutoka Umoja wa Mataifa wamesaidia bonde lile.

Mwaka jana ilikuwa wakulima walipanga hasira ile misingi iliyochimbwa wakaifukia wapate shamba zao, tukazuia zuia. Kwa hivyo mara hii ningeomba Mhe. Spika, nipate habari ya kutosha kweli kweli nitakayoiamini kweli kweli kwa kaimu Waziri wa Kilimo na Kaimu wa bajeti kilimo, juu ya suala hili la uwekwaji wa umeme katika bonde lile kwenye kile kisima.

Pia Mhe. Spika, wakati wa kujenga miundombinu hii ya mambo haya kuna mazao ya wakulima ambayo yanaathiriwa. Kwa mfano mimi huwa ninatembea tembea sana, Makombeni liko bonde kama hili la Mtambile; wao walijenga barabara kutoka Kipitacho hadi gari ya Makombeni kwa ajili ya haya mambo ya umwagiliaji. Barabara hii ilipojengwa na watu wa kilimo kuna mazao kadhaa ya wakulima ambayo yaliathiriwa lakini hadi hii leo hakuna fidia yoyote iliyotolewa. Sasa ningeomba Mhe. Kaimu Waziri anieleze ni lini wakulima walioharibiwa mazao yao watalipwa fidia wa yale mazao yaliyoathirika.

Mhe. Spika, nizungumzie kidogo katika Idara ya Kilimo mpaka sasa Mhe. Spika, kilimo chetu tumekitegemeza katika misimu ya mvua ya kawaida kama vile ilivyokuwa katika miaka ya 1960, 1970 kwa mahesabu haya ya miongo Mhe. Spika, yalifanywa mahesabu ni muda mrefu sasa uliopita kwa Machi/Mei ni Masika, Juni, Julai, Agosti ni kipupwe. Septemba, Oktoba, Novemba ni Vuli, Disemba, Januari, Februari ni Kaskazi, kwa sasa miongo hii imepitwa na wakati.

Bado ndio tunasafiria katika kilimo chetu, sasa wataalam wa leo kwa nini hawajakaa wakaanza kufikiria kuandaa takwimu nyengine au misimu hii wakaipanga upya kulingana na hali ilivyo leo, tunategemea misimu ambayo ilikuwa *calculated so many years back* mpaka leo tunabakia hapo hapo tu kuwa 21 Machi mvua inaanza ya Masika. Imeganda hapo hapo tukijua kuwa kuna mabadiliko makubwa sana. Kwa nini mahesabu hayajachukuliwa ili tukaenda na hali halisi ilivyo leo.

Jana mwanamapinduzi hapa alichangia kuhusu kilimo na alitaja matrekta yale ambayo yalikuwa na mnyororo, lakini alisema pia matrekta ya nyuma zaidi, yeye kasahau yalikuwa yana dereva na *turnboy*, dereva alikuwa anaendesha trekta tu, majembe yanakwa *controlled* na mtu mwengine nyuma huku.

Mhe. Spika, wakati ule ilikuwa mkulima haombi kulimiwa. Mtu anaweza kwenye shamba lake akakutia shamba tayari limechimbuliwa. Leo mabadiliko, lakini pia unaweza ukaomba ukaambiwa umechelewa, unaweza ukaomba ukakosa ingawa ndio desturi ya kuomba; ukiomba si lazima upate. Lakini Mhe. Spika, kuna mambo unapoomba ni lazima upate. *(Makofi)*

Mojawapo ni haya matrekta ya kulimia...

Mhe. Spika: Mheshimiwa inategemea unachoomba. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Nimesema mojawapo ambacho ukiomba upewe ni haya matrekta kwa sababu unaomba kitu ambacho ni cha kukiendeleza kilimo mbele. Mhe. Spika, tulipofika ukulima wa kijembe kongoroka kutia kibanio umepitwa na wakati. Ili kilimo kiweze kutosheleza kwa Zanzibar ni lazima kibadilike na hili ongezeko Mhe. Spika, liko wapi? Kwa sababu mazao ya kilimo kama mpunga umeongezeka lakini huu uagiziaji wa mchele kwa nini haipungui na tunasema kwamba mpunga uzalishaji wake umeongezeka, huu tunaouzalisha sisi wenyewe unakwenda wapi hata ikawa huu uagiziaji haupungui?

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ningelijua hili ongezeko la mazao ya ndani kwa nini hayaonekani na takriban wakulima walio wengi wanaolima mpunga wanakula mpunga wao ule, wakati wa mavuno tu. Wakimaliza mavuno kwa wingi wanabakisha kile ambacho wameweka kwa ajili ya kupanda mwaka unaofuata.

Mhe. Spika, katika kipindi hiki juzi lilipoulizwa suala la mbegu za muhugo tukaambiwa kwamba kumefanywa utafiti mbegu nne, ilitoa Kizimbani kwengine sijui wapi lakini ni mbegu za aina nne ambazo zote zinafaa Unguja. Kwa hivyo, mimi napanda mihogo Sipweswe nije nichukue mbegu Unguja? Shamba langu liko kwetu Pemba lakini mbegu bora iliyofanyiwa utafiti ni hizi ambazo zote ziko huku Unguja, nijitwike mzigo wa mbegu niupeleke Pemba. Je, kule Pemba hakuna mbegu ambazo Idara hii ya Kilimo imefanya utafiti na kuona kwamba mbegu hii na hii ndio bora.

Mhe. Spika, kule kuna mbegu zinaitwa mwari; ina muhogo mtamu sana na mzuri. Kwa hiyo, ningeomba kama mbegu ile haijafanyiwa utafiti wangelifanya utafiti na kuona ni kiasi gani wanaweza kuiboresha. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Mheshimiwa mimi ni mkulima eti umesema mbegu gani?

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Naam!

Mhe. Spika: Mimi ni mkulima mbegu gani umesema ili nikaiombe na mimi.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mwari!

Mhe. Spika: Ewaah! (*Makofi*)

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Muhogo wake ni mzuri sana Mhe. Spika, kwa kweli unawiva na ni mtamu, unapokula ikibishwa hodi huwezi kuitikia kwa sababu una bumbwi mdomoni. Kwa hiyo, Idara hii ya Kilimo imechukua jitihada gani yakuweza kufanya utafiti na kuiendeleza mbegu hii. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nichangie kidogo vile vile katika Idara ya Misitu ambapo katika kitabu hiki kibovu…

Mhe. Spika: Bado dakika tano.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Niongeze japo kidogo kwa sababu hiki kitabu kimejipangua. Katika kitabu hiki ambacho kimepanguka chote iko ukurasa wa 32, hapa kuna uoteshaji wa miche milioni moja ya mikarafuu. Nawapongeza sana idara hii na wizara kwa ujumla kwa kila mwaka wanaongeza idadi ya uoteshaji wa miche ya mikarafuu, ili kuongeza pato la Taifa. Na pia wamewaruhusu watu binafsi kufungua vitalu vya mikarafuu na watu wanaotesha hatimae idara inanunua na halafu inawagaia wakulima bure. Lakini mara hii katika jimbo langu kijiji cha Mjimbini sio kitalu hiki, Wizara ya Kilimo baada ya watu kufanya kazi kubwa wameshindwa kununua miche yao ya mikarafuu.

Mhe. Kaimu Waziri ningeomba kujua ni sababu zipi za msingi zilizofanya miche ile isinunuliwe ambao huu ni wito wa Mhe. Rais kuwa watu waongeze uzalishaji wa mikarafuu, ili kuongeza mikarafuu katika nchi. Lakini Mhe. Spika, kabla ya huko nyuma kidogo ilikuwa mazao yetu makuu yalikuwa ni matatu; karafuu, nazi na pilipili hoho. Leo nazi licha yakuwa ni zao la kibiashara hata kwa kupikia kwa kule Pemba haiko tena. Kuna jitihada zipi za msingi ambazo wizara itachukua kuifanya nazi irudi katika *position* yake yakuwa ni zao la biashara? Pia watachukua hatua zipi kiungo hiki cha pilipili hoho kukirudisha katika *position* yake kuwa ni zao la biashara.

Mhe. Spika, wizara hii haya mazao yote badala yakuyaendeleza wameyadumaza kwa sababu polepole pilipili inapotea, nazi tayari imepotea wakati ambao tulikuwa tuna viwanda vya mafuta ya nazi hapa Zanzibar. Tulikuwa tuna kiwanda cha usumba hapa Zanzibar. Kwa hivyo, yote hayo sasa hivi yametoweka kwa sababu hiyo nazi wenyewe haipo hata kuwa na kumbi la kufanyiwa usumba.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ningeomba wizara hii itilie maanani kama walivyotilia maanani uoteshaji wa miche ya mikarafuu, pia watie maanani uoteshaji wa miche ya minazi ili kutufanya watu wa Zanzibar tutumie nazi zaidi kuliko mafuta ya viwandani, ambayo yanatuletea madhara kadhaa wa kadhaa.

Mhe. Spika, wengi walio humu wameathirika na kwa njia moja au nyengine na vyakula vya viwandani ambavyo tunaviona ni bora lakini kwa kupikia nazi Mhe. Spika, haijashindwa.

Mhe. Spika: Haya ahsante sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu mwingi wa rehma kwa kutujaalia leo mchana huu kuchangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ya Wizara ya Kilimo.

Mhe. Spika, pia napenda nimpongeze Mhe. Kaimu Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote wa wizara hii kwa jitihada zao wanazozichukua katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Spika, napenda kuanza kwa kusema kwamba sote tunaelewa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa nchi yetu. Mhe. Spika, napenda kusema kwamba serikali bado inaonekana haijawa tayari kutoa kipaumbele kwa wizara hii kutokana na bajeti yao kuwa finyu na kupelekea kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mhe. Spika, sambamba na hilo na kuwakatisha tamaa wananchi ambao wanategemea sekta hii kwa huduma mbali mbali. Mhe. Spika, wananchi wanahitajia pembejeo, mbolea na vitu vyengine ambavyo vinategemea wizara hii, lakini kutokana na ufinyu wa bajeti hiyo wizara inashindwa kutekeleza kwa sababu bajeti haitoshi na kuwapa shida wananchi wetu.

Mhe. Spika, pia napenda kusema kwamba inapendeza kwamba pamoja na uingizaji mdogo wa fedha za wizara hii, lakini Mhe. Spika naomba niwapongeze kwa dhati kabisa watendaji wa wizara hii kutokana na kazi zao kubwa wanazozifanya za kizalendo kutokana na ukusanyaji wao mkubwa wa mapato kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kwamba wamevuka lengo la makadirio hadi kufikia asilimia 114. Mhe. Spika, naomba niwapongeze sana watendaji hawa na niwaombe waongeze bidii na wazidi kufanya kazi vizuri na Mwenyezi Mungu, *inshaallah* atawalipa.

Mhe. Spika, nikiendelea napenda kumjulisha Mhe. Waziri kwamba katika maeneo yetu ya kilimo kuna matatizo makubwa sana ya upungufu ya mabibishamba na mabwanashamba, hali ambayo inasababisha wakulima wetu kukosa kulima kwa utaalamu na kuendelea kulima kwa mazoea, jambo ambalo linasababisha kutumia nguvu nyingi lakini mapato yao yanakuwa madogo.

Mhe. Spika, hapo hapo katika suala la kilimo nilikuwa napenda kumuuliza Mhe. Waziri tunaelewa kwamba katika kijiji cha Makunduchi ilikuwa ni kijiji kikame sana, watu wa Kusini au niseme Makunduchi walikuwa chakula chao kama ndizi, muhogo wanategemea sana kutoka Wilaya ya Kati. Lakini sasa hivi Mhe. Spika, wenzetu wa Makunduchi wamevumbua kilimo hiki cha umwagiliaji wa ndizi; kilimo ambacho kinawapatia tija sana wananchi wa Makunduchi.

Mhe. Spika, naiomba serikali kama ingelikuwa imejipanga vizuri katika kuwasambaza hawa mabibishamba na mabwanashamba, ili kuwapa utaalamu wananchi wa Makunduchi katika kilimo cha migomba. Nadhani sasa hivi kilimo hicho kingekuwa kikubwa na Wazanzibari wote tungefaidika sana na ndizi za Makunduchi, na tusingetegemea tena ndizi za kutoka kwa kina Maalim Saleh ndugu yangu. Kwa hivyo, naomba sana serikali iwaone wakulima wa ndizi wa Kijiji cha Makunduchi wapewe utaalamu ikiwezekana ziboreshwe hizi skuli za wakulima isiwe tu kwa vile vikundi vya SSP vya ule mradi, lakini pia wasaidiwe wote wananchi, ili haya mafunzo na utaalamu wapatiwe wananchi wote waweze kufaidika zaidi na kilimo hiki.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kulizungumza ni tatizo la mtaro wa wakulima wa Cheju na Jendele. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri nafahamu kwamba suala hili analielewa vizuri sana la tatizo la mtaro wa Cheju na Jendele kule katika kilimo chao cha mpunga wa umwagiliaji maji. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Naibu Waziri *solution* ya tatizo hili sio kulichomokea, *solution* ya tatizo hili ni kulipatia ufumbuzi na nadhani atakuwa analijua kwa sababu najua kama anatembelea sana. Kwa hiyo asilichomekee isipokuwa alitafutie ufumbuzi, ili wananchi wale waweze kufaidika na kilimo kile na yale maji wapate kuyatumia vizuri, ili kilimo chao cha umwagiliaji waweze kukiendeleza na kiweze kuwapatia tija zaidi.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba Mhe. Kaimu Waziri nadhani hili suala limeshazungumzwa na watu wengi lakini na mimi pia nataka kulisisitiza. Mhe. Waziri naomba sana lile deni la wakulima wa mbegu limalizwe, kwa sababu wakulima wale ni wanyonge sana na wao wanategemea kwamba wanalima, ili waiuzie mbegu serikali wakitegemea kwamba watapata mafanikio. Lakini inasikitisha kwamba mpaka sasa lile deni halijamalizwa kwa hiyo Mhe. Waziri nakuomba sana hili deni lao wale wananchi limalizwe ili waweze kuzifaidi nguvu zao.

Mhe. Spika, jambo jengine ninalotaka kulizungumza ni kuhusu wizi wa mazao. Mhe. Spika, wizi wa mazao ni kero kubwa sana kwa wakulima wetu. Mhe. Spika, wakulima wetu wanakuwa wanalima kwa malengo wakitegemea kwamba kilimo kile kiwasaidie wao na familia zao kwa mambo yao tofauti tofauti. Mhe. Waziri mkulima anapolima anategemea kwamba analima kwa kutegemea labda anaweza kusema anaweka mazao yake kipindi cha Ramadhani au cha sikukuu yamsaidie kwa ajili ya futari, pia na kilimo cha biashara kimsaidie katika kufanikisha shughuli zake za sikukuu na familia yake.

Mhe. Spika, malengo ya wakulima yanakatishwa na wizi wa mazao; wizi wanawaathiri sana, wizi wanatoka usiku wanakwenda kuvuna kama wamelima pamoja. Mkulima anapokwenda asubuhi shambani kwake kweupe na mwizi tayari ameshapeleka mazao yale sokoni, anakwenda kuuza na anafaidika yeye. Kwa hiyo, Mhe. Waziri naomba kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Sheria itayarishwe sheria kali yakuwadhibiti hawa wezi wa mazao ambao wanaathiri wakulima wetu.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 76 katika kiambatanisho kile cha programu ya lishe bora inasema kwamba lengo kuu la programu hii ni kuchangia katika hatua za kitaifa za kupunguza umasikini wa chakula na kipato. Kukabiliana na hali ngumu ya kutokuwa na uhakika wa chakula na lishe katika ngazi ya taifa, jamii na kaya na kushajihisha ushiriki katika jamii katika hatua ya kuongeza kipato. Mhe. Spika, hili ni lengo zuri naweza kusema, lakini lengo hili halitafikiwa kama hatutaweza kuwadhibiti vizuri hawa wizi wa mazao, kwa sababu hata tukipanga haya lakini wananchi wanapotaka kutekeleza hili na wizi nao wanajitayarisha kwa ajili ya kuwaharibia mipango yao wakulima. Kwa hiyo, Mhe. Waziri naomba sana suala hili la wizi wa mazao ulifikirie vizuri na lipangiwe mikakati.

Mhe. Spika, mwisho kabisa namalizia kwa wakulima wa midimu. Mhe. Spika, nalichangia suala hili; kwanza mimi naomba nilete ujumbe hasa wa hii jumuiya ya wakulima wa midimu wa Jimbo la Chwaka; jumuiya yao inaitwa JUAMIJICHWA.

Mhe. Spika, suala hili sina uhakika na mimi kama la kilimo ama la Wizara ya Biashara, lakini Mhe. Spika, wakulima hawa wa jumuiya hii ya JUAMIJICHWA wana kilio kikubwa sana cha soko la ndimu zao. Mhe. Spika, wananchi wa Chwaka wa jumuiya hii ukienda kuangalia mikono yao utawaonea huruma, kwa sababu ndimu hazina soko na ndimu wanazo nyingi sana. Wanachofanya sasa hivi ni kuzikamua na mikono yote imeshafanya kinyanya kwa ndimu.Walichokuwa wanategemea kuna wafanyabiashara Wakomoro walikuwa wanakuja na wanakwenda kuzinunua ndimu zao, lakini sasa hivi Wakomoro wale wamekatisha na ndimu wanazo nyingi na baada ya kuona kwamba mwani hauna soko ndio waliamua kujiingiza katika kilimo hicho cha midimu, na kilimo cha midimu sasa hivi imekuwa pia hakina soko inakuwa matatizo. Kwa hivyo, bado wananchi wa jumuiya ya JUAMIJICHWA wanapenda kujikomboa.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri suala hili kama ni la kwake basi naomba lipatiwe ufumbuzi, lakini kama si la kwake pia naomba nipate jibu ili itapokuja Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko niweze kulichangia.

Mhe. Spika, mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi na nitakuwa sina mengi ya kuchangia. Naunga mkono hoja, nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru sana kunipa nafasi hii kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Kilimo na Maliasili. Kabla ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) aliyenijaalia kuwa katika hali ya uzima na afya inayoniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kuwahudumia wananchi wetu.

Mhe. Spika, vile vile nimpongeze Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili pamoja na Naibu Waziri na watendaji wao wote wa wizara hii kwa utendaji wao wa kazi, tunawapongeza sana kwa ushirikiano wao.

Mhe. Spika, nikianza na mchango wangu naomba niende moja kwa moja katika ukurasa wa 3, hapa inaelezwa ukuaji na mchango wa Sekta ya Kilimo katika pato la Taifa. Nimesema kilimo kuwa ni uti wa mgongo vile vile kinatuletea pato katika taifa letu, lakini ukiangalia kilimo kimepewa kipaumbele na kama kimepewa kipaumbele basi tunadhani usimamizi wake utakuwa mzuri ili kufikia hayo maendeleo ambayo yamepewa kipaumbele.

Tumeambiwa uzalishaji umekua, ni kweli kwa wastani lakini ukiangalia mkulima mimi nadhani ni yule anayelima akapata chakula chake na akapata mazao mengine akauza kwa kupata mahitaji mengine, huyo ndiye mkulima, lakini kuna wengine hawa ni waganga njaa, mtu analima hata kula yake ya mara moja inamshinda, basi huyu hali yake inakuwa sio nzuri.

Mhe. Spika, nchi yetu na ardhi yetu ni ndogo lakini ikiwa na usimamizi mzuri basi mahitaji ya kilimo yanapatikana sana. Hapa tumesema kama uoteshaji wa mikarafuu umesimamiwa vizuri na wakulima wengi wa mikarafuu sasa hivi wamepanda mikarafuu mingi, baada ya miaka kama mitano hivi tutaona manufaa ya mikarafuu hiyo lakini mambo mengine yako chini.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nakwenda katika Idara ya Kilimo katika ukurasa wa 20 imepewa majukumu ya kusimamia hiki kilimo, lakini tuulize usimamizi huu upo? Kama upo vipi uzalishaji wake. Mimi niseme tu kama usimamizi wa idara hii ni mdogo sana, naomba ninukuu katika ukurasa wa 20.

Kifungu 5.1 kinasema kwamba;

> "Mhe. Spika, idara hii ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, upatikanaji na usambazaji wa huduma za pembejeo na zana za kilimo kwa ukulima, uhifadhi na ukaguzi wa mazao na kutoa mafunzo kwa wazalishaji".

Idara hii imepewa jukumu hilo kusimamia na kuleta maendeleo ya uzalishaji, lakini mimi nasema hao mabwanashamba hatuwaoni kupita kama ilivyokuwa zamani, maana ukisema unasimamia unakaa ofisini sio usimamizi, lakini kama utatembea utaona mahitaji ya wakulima wanataka nini, wasaidiwe nini na waelekezwe kitu gani, hapo utajua kama kuna matatizo na unaweza kuchukua hatua ukayatekeleza, lakini kama utakuja kuripoti kwenye makaratasi, basi mafanikio hakuna kabisa. Tunaomba kama imekusudiwa Mapinduzi ya Kilimo

kweli basi lazima mabwanashamba na mabibishamba wafanye kazi ya ziada pamoja na wataalamu wetu, hapo ndio tutafikia malengo ya kilimo.

Mhe. Spika, tumeambiwa hapa kuhusu Kilimo cha Maweni. Pamoja na jitihada zinazofanyika lakini bado hali imekuwa ngumu katika uzalishaji. Ni kweli lakini niseme hii inatokana na huo usimamizi mbovu, bado nizungumzie kutoka ukanda wa Micheweni unakuja zako mpaka Kojani Kisiwani, unakwenda zako Ng'ambwa, Vitongoji, Kangagani kote huko ni sehemu moja. Mheshimiwa usimamizi wa kilimo cha maweni kama utashughulikiwa bado uzalishaji utakuwepo. Naomba nitoe mfano.

Mwaka 1972 na 1974 kilimo cha maweni kilisimamiwa vizuri na nadhani Kisiwa cha Kojani kulivunwa mtama mpaka ukashinda katika mashamba, itakumbukwa lakini kulikuwa na usimamizi mzuri kweli kweli. Sisi ni watu wa dago lakini ilikuwa huruhusiwi kwenda dago kama hujalima, watu wakajipanga kwa vikundi na walilima mtama na mawele ulivunwa kweli kweli.

Sasa mimi nadhani usimamizi ule umeondoka na nasema usimamizi katika kilimo cha maweni hauna kazi, nathubutu kusema mpaka leo upandaji wa uwele Kojani kisiwani bado unanawiri vibaya sana haushughulikiwi tu, tena sio uwele tu na mtama pamoja na mazao mengine kama *water melon* yananawiri vizuri. Hiyo sehemu niliyoitaja ya Ng'ambwa watu wanavuna sana lakini usimamizi sio mzuri. Matango pia yananawiri, tungule unavuna mpaka ndoo inauzwa shilingi 1,500 katika msimu wa uvunaji.

Sasa tunawaomba hawa wanaofanya utafiti waende na sehemu kama hizo wakafanye utafiti wa kutosha, wakienda watagundua mambo mengi. Ilikuwa ikifika Mwezi wa Ramadhani ukitembea Zanzibar katika mitaa unasikia harufu za viungo zinavyopendeza, lakini sasa wapi hayashughulikiwi hili ni tatizo. Sasa tusiseme kwa kuimba tu Mapinduzi ya Kilimo, Mapinduzi ya Kilimo, au tunafanya Mapinduzi ya Kilimo kukiua kile kilimo? Tunataka kujua. Hebu Mhe. Waziri tuambiwe Mapinduzi ya Kilimo hayo tunataka kukiua kile kilimo au tunataka kije juu? Kama tunataka kije juu basi lazima kuwe na mbinu mbadala na maelekezo na wataalamu wetu wapite katika mashamba ili kuwaelekeza wananchi, tutakuwa na mavuno mengi sana.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende katika Idara ya Umwagiliaji. Idara hii ina majukumu ya kuwaelekeza wananchi katika kilimo cha umwagiliaji na kilimo hiki ndio kilimo cha sasa. Kwa kweli tukiwa na kilimo hiki basi hata ndani ya mwaka unaweza kuvuna mara tatu, lakini kwa kusubiri msimu wa mvua ni wa mwaka mmoja tu, tunaomba wazingatie sana suala la umwagiliaji na kuwa na miundombinu mizuri ya kuweza kuwafikia hao wakulima ili kuwapa mahitaji ya kufikia kile kilimo cha umwagiliaji.

Wenzetu wa Tanzania Bara hivi ndivyo wanavyotumia; na tunawaona mchele wao mzuri, mtamu kutoka sehemu za Mbeya na Iringa ni hapa hapa Tanzania na sisi hapa tunaweza tukawa tusihitaji chakula kutoka nje, lakini kutokana na ukulima wetu huu basi ni wa kuganga njaa tu chakula chako cha siku moja hata mbegu uliyoipanda hairudi.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu utakuwa ni mdogo sana, lakini mwisho niende katika Idara ya Misitu na Maliasili. Idara hii ina majukumu ya kusimamia misitu na kuimarisha, lakini nataka niseme kwamba hili limekuwa janga kubwa sana, misitu inakatwa ovyo ovyo, miti yote inakatwa bila ya kujali chochote hasa minazi imepotea kabisa. Sasa hivi minazi imekuwa ndio inayochongwa mbao za kuezekea, milango na kila kitu, watu hawa hawajali kama kuna matumizi mengine ya kisheria.

Halafu tulikuwa na ile sera ya *kata mti panda mti* hatuoni miti kuoteshwa, watu wanakata tu miembe yote inakatwa, miembe sakua pia inakatwa, miti yote imepotea. Ilikuwa katika msitu wa Mtambwe kule kwa Mhe. Salim Abdalla Hamad ni mzuri sana lakini miti yote imekwenda na maji hakuna msitu hata mmoja ulioimarika, tena hata ukienda ni jangwa tu.

Sasa hali kama hii ndio hayo mabadiliko ya tabia nchi. Tuangalie tunasema wakati wa baridi hapa ni joto mpaka leo haya ni matatizo. Sasa ile miti ina hewa pekee alizungumza Mhe. Saleh Nassor Juma, lakini sasa miti tunaikata ovyo hatuwezi kufikia malengo. Kwa hivyo, tunawaambia wanaosimamia idara hii lazima wawe wakali kweli, miti inapotea na baadae nchi itakuwa jangwa.

Mhe. Spika, mimi kwa siku ya leo naomba niishie hapa na tunaomba sana wataalamu wetu katika kilimo cha maweni waende wakafanye utafiti wa kutosha bado mazao yanastawi, wakienda kule tutapata mavuno mazuri sana. Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Kilimo na Maliasili. Kwanza nichangie ukurasa wa 5 kuhusu kilimo cha maweni.

Mhe. Spika, kwa kweli Wizara ya Kilimo na Maliasili hivi sasa haikipi kipaumbele kilimo cha maweni kwa sababu kilimo hiki hivi sasa kimeshuka sana, wakati tunajua kilimo hiki ni cha hasara sana. Kilimo cha maweni tukiangalia hakina matatizo makubwa ya kuweza kuipa ugumu serikali kwa kuweza kupata trekta ama kupeleka mbolea nyingi katika kilimo hiki.

Tukiangalia kilimo hiki hasa vilimo vilivyotajwa humu kama pilipili hoho, mtama, choroko pamoja na mbaazi; utashangaa sana Mheshimiwa kwamba tunaagiza vitu hivi nchi jirani na nchini mwetu vinakuja vizuri bila ya hata mbolea nyingi.

Kusema kweli ni kwamba sisi katika Jimbo la Koani hatuhitaji hata mbolea katika kilimo chetu cha mbaazi ama pilipili hoho au mtama, lakini kwa kweli hukuti mabwanashamba kupitia katika sehemu hizo angalau kuwaelekeza wananchi namna gani waendelee na kilimo hicho na kwa wakati gani, tunalima kwa kutumia akili ya kichwa bila ya ujuzi kutoka kwa mabwanashamba.

Namuomba Mhe. Waziri akija aniambie kwamba Jimbo la Koani hivi sasa kuna mabwanashamba wangapi ambao wanahamasisha vilimo vya maweni na utakuta vilimo hivyo vinalimwa sana.

Mhe. Spika, nikiangalia kilimo cha pilipili hoho ni kilimo ambacho hakibwagi katika nchi yetu, kwa sababu nchi nyingi za nje sasa hivi zinahitaji sana pilipili hoho na ni zao ambalo linatoka katika Jimbo la Koani, lakini wananchi hawahamasishwi angalau wakilima pilipili hoho zikaushwe ili wauze kwa bei nzuri kama inavyotangazwa bei ya karafuu. Nina hakika wananchi wangehamasishwa kwamba watauza bei gani kwa kilo ingelikuwa zao hili limekuwa kama lilivyokuwa mwaka 1961 na 1962.

Mimi mwenyewe nilikuwa mchumaji mzuri sana wa pilipili hoho na tulikuwa tunachuma tunajua inavyouzwa wakati huo hamna kilo kuna kibaba, tunajua kibaba kiasi gani na tulikuwa tunaendesha maisha yetu na tukaweza kuishi kwa zao hilo. Leo pilipili hizi zimetupwa na ndio zinahitajika, hakuna nchi duniani ambayo haina vita, hakuna nchi ambayo haihitaji kurushiwa watu maji ya pilipili ama mabomu ya pilipili, tuna hakika ni kitu ambacho kinahamasisha nchi yetu na inawezekana zikatajirisha nchi kuliko hata karafuu.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri akija anihakikishie kwamba kilimo cha pilipili hoho watakitilia nguvu wakishirikiana na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko watanunua bei gani pindi wananchi wetu watapozilima kwa wingi pamoja na mbaazi ambazo ziko nyingi sana katika jimbo letu.

Mwezi huu wa Ramadhani watu wengi wanataka wapate mbaazi kwa ajili ya futari, naona ajabu kwamba hivi sasa mtu anaagiza mbaazi kutoka nchi jirani wakati nchi yetu inazalisha sana mbaazi pamoja na mtama wa kupikia uji.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri akija anambie kwamba wananchi wetu watapata angalau majembe na mapanga kwa wingi ili tuingie porini kuweza kuhakikisha kilimo cha porini kinaendelea na kuweza kupata kuhamasishwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, nataka nichangie ukurasa wa 20 kifungu cha 5 Idara ya Kilimo. Kwa kweli nchi yetu mara nyingi inahamasika sana na kilimo cha mpunga, lakini hivi sasa Wizara ya Kilimo na Maliasili inaumiza sana wananchi wetu kwa sababu wanalima kwa vijembe vya kawaida badala ya kupatiwa matrekta yakalima kwa wakati. Wananchi wanaweza kutoa pesa zao kwa wizawa wakalimiwe kwa wakati, na wakati ule matrekta yapo mengi kumbe matrekta yale Waziri wa Kilimo na Maliasili hakuyafanyia uchunguzi kama ni mazima au mabovu,

utakuta wakati wa kilimo tayari matrekta yaende kwenye kilimo basi hayawezi kwenda na yako pale pale na wananchi wametoa pesa zao na wakati huo huo wananchi wale hawalipwi pesa zile.

Namuomba Mhe. Waziri watu wa mabondeni kama vile Kilombero, Koani pamoja na mabonde mengine wananchi wengi wanadai pesa zao kwenye wizara hii na mpaka leo hawajalipwa. Hivyo Mhe. Waziri ahakikishe kwamba wananchi wale wanalipwa pesa zao ili wafidie, walime kwa vilimo wanavyoweza wenyewe kwa sababu Mhe. Waziri mpaka sasa hajawapa pesa zao wananchi wanalalamika, wametoa pesa zao wakati wa kilimo umepita matrekta hayakwenda kulima kwa wakati.

Mhe. Spika, wananchi wanajitahidi sana kulima cha mpunga lakini mbolea haifiki kwa wakati na hata ikifika inauzwa bei ya juu, tena bei ya kuruka ambayo ya kupita kwa chini ili uliwe rushwa ndio uweze kupata mbolea.

Kwa kweli inasikitisha sana kwamba wizara yetu haiuzi mbolea wenyewe wanawapa wananchi wengine wanauza kwa njia za panya na hapo mbolea inakuwa bei mbaya, na wananchi wanashindwa kulima na mazao waliyohitaji. Wananchi wanalima lakini vilimo vingi hawapati mbolea na utakuta mpunga unaharibika.

Mhe. Spika, matatizo hayo ni mengi sana nchini kwetu na namuomba Mhe. Waziri anihakikishie kwamba bei ya mbolea awatangazie wananchi mbele ya Baraza lako, mbolea inauzwa bei gani kwa kilo tukiacha wananchi wanavyouziwa. Mwananchi akiuziwa bei hiyo amkamate muhusika anayeuza mbolea hiyo kwa bei ya juu.

Mhe. Spika, wananchi wetu wana matatizo sana ya kuweza kupata mbegu za mpunga. Hivi sasa mbegu hazipatikani, na hata zikipatikana hawapewi kama ilivyotegemea Serikali; wananunua, hata ukinunua unauziwa bei ya juu sana ili uweze kupata mbegu. Wananchi wana hamu sana ya kulima hasa katika mabonde ya Koani lakini wanashindwa kupata mbegu pamoja na mbolea kwa wakati.

Mhe. Spika, tatizo kubwa zaidi katika bonde langu la Koani hivi sasa limeshatayarisha kila kitu lakini halijaweza kufanyiwa mabonde yale kuweza kupata kulimiwa kumwagia maji kwa ukamilifu. Utakuta bonde lipo tayari, kisima kimeshachimbwa tayari, lakini utakuta mitaro bado haijatengenezwa kuweza kuhakikisha kwamba wanapata kumwagilia maji kwa wakati. Tunajua mpunga wa kumwagilia tunaweza kupata mara tatu kwa mwaka, na hivi sasa utaona tunategemea mvua wakati uwezo wa kumwagilia upo lakini haipatikani.

Mhe. Spika, nizungumzie matatizo ya maliasili kuhusu misitu yetu. Mhe. Spika, misitu yetu inakatwa bila ya mpango, lakini hao askari ambao wanawekwa kulinda misitu hawalindi ipasavyo. Kama mfano askari wa KMKM anayelinda bahari ukamkuta analinda pori, ni sawasawa na askari wa misitu utamkuta anangoja kukamata gari sio kule porini kunakokatwa miti. Anakamata gari ya mizigo ya kuni lakini kwenda porini akamkamata mhalifu ambaye anakata wakati huo hana.

Namuomba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba askari wa maliasili waende kwenye sehemu zao na wamkamate mtu na mti ambao ulikatwa. Sio anakuja kukamata gari ambayo ina kuni hajui kuni zile zimekatwa muda gani na utakuta zimeshakuwa kavu, na kuni zikiwa kavu ni wajibu kukatwa, lakini anamkamata mwananchi na kumdhalilisha na kuni zake wakati kwenda porini akakamata mti mbichi ambao umekatwa hamfuati.

Kwa hivyo, mimi naona askari ambaye amempeleka mtu na kuni kavu aanze kukamatwa yeye hakufanya jukumu lake. Kwa sababu jukumu lake ni kumkamata mtu anayekata kuni porini, kuni zile zikawa mbichi, na sio kuni zile zipo kwenye gari ama zimewekwa ndani ya nyumba yeye akaanza kuingia kupekua nyumba. Kazi ya kupekua nyumba ni ya askari polisi sio askari wa misitu.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri akija anihakikishie masuala haya yatatekelezwa katika bajeti yake hii ya fedha. Kama hakuweza kujibu masuala haya nitaondoa shilingi katika mchango wa bajeti hii kwa sababu wizara hii haichukui majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Spika, sitakuwa na mchango mkubwa isipokuwa namsubiri Mhe. Waziri akija atujibu masuala ya matatizo ya nchi yetu, wakati uwezo tunao wa kujihakikishia chakula katika nchi hii acha kuagiza nchi za nje. Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa na afya njema.

Pili, naomba kukushukuru wewe Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia na kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kuichangia vizuri Hotuba ya Wizara ya Kilimo na Maliasili. Napenda kuwahakikishia kuwa michango yao, maelekezo na ushauri wao tumeyapokea na tutayafanyia kazi wakati wa utekelezaji wa majukumu yetu ya Wizara.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa michango na maelekezo yao wakati walipowasilisha maoni ya Kamati. Tunaahidi kwamba Wizara itayafanyia kazi maelekezo na ushauri waliotupa.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kujibu hoja za Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kama ifuatavyo:

Suala la Pembejeo. Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba suala la pembejeo linahitaji kuangalia kwa uhalisia wake. Inawezekana kama Waheshimiwa Wajumbe walivyochangia kwenye pembejeo, wameeleza wasi wasi wao uhaba wa pembejeo. Kwa upande mmoja inawezekana ikawa hivyo.

Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe wakumbuke kwamba katika Baraza hili hili, wakati Wizara ilipowasilisha hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2010/2011, Wizara kwa wakati huo iliagiza tani 88.62 za mbegu bora za mpunga, kununua matrekta mapya 10, kuagizia tani 260 za mbolea na kununua lita 12,000 za dawa ya magugu.

Mhe. Spika, hivi tayari Wizara imeshafikia kununua na kusambaza mbegu bora ya mpunga inayofikia tani 650 kwa mwaka, mbolea ilinunuliwa na kusambazwa na wakulima kufikia tani 1,500, dawa ya magugu lita 30,000 na kununua matrekta mapya 33.

Mhe. Spika, hata hivyo, kutokana na kuongezeka kwa wakulima wetu, kuhamasishika na kutambua umuhimu wa mbegu bora na pembejeo, mahitaji ya pembejeo yameongezeka sana.

Mhe. Spika, naomba kumuarifu Mhe. Bikame Yussuf Hamad kwamba mbolea ya *TSP* haijatoweka na ipo katika vituo vya mauzo ya huduma za pembejeo (Matangatuani na Wingwi), na katika juhudi za kuziweka pembejeo karibu kwa wakulima utaratibu maalumu unafanyika pale bonde/Shehia inapohitaji kukusanya pesa zao na kupeleka kwa viongozi wa wakulima wa Shehia husika. Mfano Shehia ya Sizini, Konde, Msuka Mashariki, Msuka Magharibi na Kinowe. Ndani ya msimu huu wa masika wakulima walihitaji wapelekewe mbolea ya *Urea* katika Shehia zao na Wizara ilifanya hivyo. Vile vile mabonde ya umwagiliaji maji ya Weni na Mangwena, Tungamaa na Dobi walipelekewa huduma hizo.

Mhe. Spika, pia naomba kumuarifu Mhe. Ali Salum Haji kuwa Serikali haijawabagua wakulima wa maweni na inatambua mchango wao katika Sekta ya Kilimo na ndio maana huwapatia mbegu bora za mazao kama mtama, fiwi na viazi vikuu.

Mhe. Spika, suala la fedha za wakulima wa walioikopesha Wizara mpunga, Wizara tayari imeshawalipa wakulima pesa zao zote ambazo walikuwa wanaidai kutokana na kukopesha mbegu za mpunga.

Mhe. Spika, tumewalipa wakulima nakumbuka siku ya tarehe 11 ambayo niliondoka mimi hapa kwenda kuhakikisha katika vituo ambavyo vilikuwa vinadaiwa Cheju na pesa zao hawa wote wameshalipwa. Kwa hivyo, Wizara haina deni katika suala hili. Pia Wizara tayari imeshanunua mabomba matatu yenye ujazo wa lita

ishirini (20) kila moja. Wizara pia imechukua hatua ya kuyapima na kutengeneza hati miliki baadhi ya mabonde makubwa ya mpunga kama vile bonde la Kibondemzungu.

Mhe. Spika, kuhusu eneo hilo limechukuliwa kwa kazi maalum ya mradi wa kuzalisha mbegu ya nafaka hasa mpunga kwa msaada wa *USAID* na eneo hilo ni la Serikali, hivyo hakuna mpango wa kuwafidia.

Mhe. Spika, Wizara kupitia vituo vyake vya kuzalisha mbegu na zile zinazozalishwa na wakulima kwa njia ya mkataba, huzalisha mbegu zinazostahamili ukame na zenye sifa za ziada za kustahamili wadudu na maradhi. Wizara huwapatia wakulima huduma ya kuwapigia dawa bure pale inapotokea uharibifu wa wadudu. Mfano mwaka huu wadudu waliharibu eka 400 za mpunga katika Wilaya ya kati na Kaskazini 'B'. Pia dawa ya kuzuia nzi waharibifu wa matunda hutolewa bure.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Panya Ali Abdalla kwamba Wizara inachukua hatua na juhudi kubwa kuwapatia wakulima hao mafunzo juu ya elimu ya kilimo bora cha uzalishaji wa mboga na udhibiti wa wadudu waharibifu.

Mabwanashamba ni washauri wa kanuni bora za kilimo kwa wakulima. Hivyo huripoti kazi kwa uongozi wa Shehia waliyoitembelea na kuwasilisha kitabu cha mahudhurio ya kazi kwa kusainiwa na kugongewa muhuri wa uthibitisho wa kufika kazini siku hiyo.

Suala la Uhakika wa Chakula na Lishe. Mhe. Spika, kuhusu suala la uanzishwaji wa hifadhi ya chakula ambalo limechangiwa na Wajumbe watatu akiwemo Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Salma Mohammed Ali na Mhe. Panya Ali Abdalla.

Napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika uanzishwaji wa hifadhi ya chakula bado ipo. Katika utekelezaji wa azma hii kutakuwa na maghala mawili ya akiba; moja Unguja na jengine Pemba yenye uwezo wa kuhifadhi tani 12,000 na 24,000 za mchele. Naomba kuwahakikishia Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba kazi hii itatekelezwa mara baada ya fedha ya kazi hiyo kupatikana.

Mhe. Spika, Wizara inakubaliana na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo na Mhe. Suleiman Hemed Khamis katika kuendeleza utafiti wa mazao ya kilimo ikiwa ni pamoja na kukiendeleza Kituo cha Utafiti cha Matangatuani ili kiweze kuendeleza kazi za utafiti.

Napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba kwa mwaka wa fedha 2014/15 Wizara imetenga fedha kwa ajili ya kujenga uwezo wa watafiti pamoja na kukifanyia matengenezo Kituo cha Utafiti Matangatuani.

Suala la Utengenezaji wa Chumvi.Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya jitihada kubwa katika kuwaendeleza watengenezaji wa chumvi kupitia Taasisi za Serikali. Kwa upande wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imewapatia elimu na baadhi ya nyenzo za kufanyia kazi. Wizara ya Kilimo na Maliasili imewapatia kituo cha Jumuiya ya Kutengeneza Chumvi kilichopo Machomanne.

Suala la ukulima wa chumvi kwa muda mrefu halikuwa likiratibiwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili. Kwa bahati nzuri kuanzia mwaka 2014 kazi ya ukulima wa chumvi itaanza kuratibiwa rasmi na Wizara ya Kilimo na Maliasili. Hivyo, kazi za mwanzo za msingi zitakazofanyika ni pamoja na kufanya tathmini ya maeneo yote ya utengenezaji wa chumvi na kuangalia mustakbali wa utengenezaji wa chumvi na hali halisi ya utunzaji wa mazingira yetu.

Upandaji wa Miti wa Miti kwenye Mashimo ya Mchanga. Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili tayari imeanza kulifanyia kazi suala la upandaji wa miti katika maeneo yaliyochimbwa mchanga na kuweka utaratibu maalum wa kisheria kurekebisha maeneo ambayo yamechimbwa mchanga. Hatua ambazo zinaendelea ni kupanda miti katika maeneo hayo kwa kushirikiana na wananchi wanaohusika. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 jumla ya hekta 27 za miti zimepandwa katika mashimo ya mchanga. Hatua ya pili Wizara ya Kilimo

na Maliasili imelizingatia suala hilo katika mapitio ya Sheria na Sera mpya ya Misitu ambayo ipo katika hatua za mwisho ya matayarisho.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Nam. 10 ya mwaka 1996, maliasili zote za misitu zinahitaji kibali cha ukataji na usafirishaji pale mwananchi anapotaka kukata au kusafirisha maliasili hizo. Maliasili zinazokamatwa na kubainika kuwa hazina vibali hivyo, basi mtu huwa amefanya kosa kisheria. Mtu huyo hupelekwa Mahkamani au anahukumiwa au anachukuliwa hatua na Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka kwa mujibu wa kifungu nambari 98(1) cha Sheria Nam. 10 ya mwaka 1996. Mali iliyokamatwa na mtenda kosa huyo hushughulikiwa kwa mujibu wa kifungu nambari 98(2) cha Sheria Nam. 10 ya mwaka 1996 ambapo mali hiyo hutaifishwa na kuuzwa na fedha kuingizwa katika mfuko wa Serikali.

Uajiri wa Wahitimu wa Chuo cha Kilimo.Mhe. Spika, kuhusu suala la kuwaajiri wanafunzi wanaomaliza masomo katika Chuo cha Kilimo Kizimbani, Wizara inahakikisha kwamba inawaajiri wanafunzi wote wanaohitimu masomo yao katika Chuo cha Kilimo Kizimbani pale tu Serikali itakapokuwa na uwezo wa kuwaajiri wakati fedha zitakapoingizwa. Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara imeajiri wafanyakazi 60 wakiwemo mabwana/mabibishamba 45.

Mhe. Spika, kuhusu suala la Uvamizi wa Mabonde. Wizara ya Kilimo na Maliasili inashirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati inaendelea na kuyapima na kuyapatia hati miliki mabonde na maeneo yote ya kilimo yaliyo chini ya Wizara. Jumla ya maeneo 23, zikiwemo nyumba 10 na mashamba 13 yameshapatiwa hatimiliki, na maeneo 19 yameshapimwa na kupatiwa michoro na yanasubiri hatimiliki. Hata hivyo, naomba kutoa wito kwa viongozi wa Mikoa, Wilaya na Shehia kwa kushirikiana na Wizara katika kusimamia Sheria na kanuni zilizowekwa ili kuepuka uvamizi na uhifadhi wa maeneo yaliyotengwa kwa kazi za kilimo.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii napenda kumjibu Mhe. Ali Salum Haji kuhusu ongezeko la kifungu nambari 221008 cha huduma za utunzaji wa misitu kutoka 51,100,000 mwaka 2013/2014 hadi kufikia 80,310,000.

Mhe. Spika, hichi ni kifungu mama kinachojumuisha vipengele vifuatavyo:

- Uoteshaji wa miche ya matunda na misitu
- Ujenzi wa vitalu
- Vifaa vya vitalu
- Ununuzi wa mbegu
- Huduma za kujikinga na moto
- Upandaji wa miti
- Kazi za doria

Aidha, masuala ya kujikinga na majanga ya moto, uoteshaji wa miche na huduma za ulinzi wa misitu ni huduma za msingi na zinahitaji fedha nyingi. Ndio maana Mhe. Ali Salum Haji ukaona vifungu hivyo vimenona.

Mhe. Spika, kuhusu kifungu nambari 220100 kinachohusu huduma za mawasiliano na nambari 220301 safari za ndani, nambari 220302 safari za nje, nambari 220400 gharama za mafuta na vilainishaji.

Mhe. Spika, kufuatia muundo mpya wa wizara za serikali kwa viongozi wote wa wizara wanaratibiwa katika Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Vifungu hivi vilikuwa vinaratibiwa na Idara ya Sera, Mipango na Utafiti na hivi sasa vinaratibiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi kama uratibu unavyotaka.

Mhe. Spika, ninapenda kumfahamisha Mhe. Ali Salum kuwa wafanyakazi waliopo masomoni ni wa aina mbili. Wale wanaoendelea na wale walioanza masomo mwaka 2013/2014. Kwa jumla idadi ya wafanyakazi wanaolipiwa gharama za mafunzo ni 129, kati yao wafanyakazi 62 wanaendelea na masomo na wafanyakazi 67 wameanza masomo katika mwaka 2013/2014.

Katika ngazi za cheti, stashahada, shahada ya kwanza na ya pili na ya tatu. Mwaka 2014/2015, wizara inategemea kufundisha jumla ya wanafunzi 20 katika ngazi ya cheti, stashahada, shahada ya kwanza, ya pili na ya tatu.

Suala la umwagiliaji maji Mhe. Spika, katika bonde la Kinyakuzi, miundombinu ya umwagiliaji maji hivi ipo katika hali nzuri kufuatilia ujenzi wa misingi na umwagiliaji wa maji wa saruji uliofanyika kwa kutumia fedha za *TASAF*.

Aidha, bwawa la kuhifadhia maji ya kumwagilia limefanyiwa ukarabati kwa fedha za SMZ. Hivi sasa mpunga upo shambani na unasubiri kuvunwa.

Mhe. Spika, ama katika bonde la Saninga, ninapenda nikiri kwamba kumejitokeza hitilafu katika mfumo wa umwagiliaji kutokana na kuvunjika kwa bwawa linalomwagiliwa katika hekta kumi na sita (16). Napenda nimuhakikishie Mhe. Bikame Yussuf Hamad kwamba bwawa hili tutalifanyia matengenezo ili kuweza kumwagilia eneo hilo.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kumuomba Mhe. Bikame atusaidie kuwahamasisha wakulima wa Saninga ili wakitumie kisima kiliopo na miundombinu ya umwagiliaji iliopo katika eneo lililobakia, kwani hivi sasa wananchi wamesita kabisa kulima katika eneo hilo kwa kujishughulisha na ukulima wa mwani na hata huthubutu kusema kwamba ikiwa matrekta yanapumzika, kwa nini nao wasipumzike.

Mhe. Spika, aidha msingi wa kuzuia mafuriko kwa kawaida huwa tabia ya kujifukia kutokana kupotea maji mengi yaliyojaa mchanga kutoka kwenye maeneo ya miinuko. Ninapenda kuliarifu Baraza lako Tukufu Mhe. Spika, kwamba suala la kuondoa mchanga ni jukumu la wakulima kuhakikisha kwamba misingi hii inasafishwa ili kufanya kazi yake na kupunguza mafuriko katika mabonde husika.

Mhe. Spika, napenda kutoa taarifa kwamba sehemu ya Kilombero na Pangeni imo katika mradi mkuu unaoendeshwa kwa mkopo kutoka *Exim Bank* ya Korea, kufuatana na mradi huu wa Kilombero na Pangeni, kujengwa bwawa, mitaro ya kumwagilia maji, mitaro ya kutoa maji, njia za mashambani na kutayarisha eneo lenye ukubwa wa hekta mia mbili thalathini (230).

Mhe. Spika, hivi sasa kazi ya utayarishaji michoro imeanza. Kazi hii inafanywa kwa mashirikiano ya wataalamu wa kigeni wa Kampuni ya KRC na DASAN na wataalamu wa ndani. Aidha, kupitia mradi wa nafaka unaofadhiliwa na *USAID* tayari kwa msimu huu umewezesha wakulima 50 wa Pangeni na wakulima 50 wa Kilombero kwa mafunzo ya vitendo kuhusiana na mbinu bora za kilimo cha mpunga.

Mhe. Spika, kwanza ninapenda nikubaliane na Mhe. Salma kwamba mwanzo wa miaka 1990 wakulima wa bonde la Kwapweza walikuwa wanapata mavuno makubwa ya mpunga kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji.

Kwa wakati ule chemchemu ya Kwapweza ndio iliyokuwa chanzo kikuu cha maji ya kumwagilia, lakini kufuatia uamuzi wa serikali wa kutumia chemchemu hii kama chanzo cha maji kwa matumizi ya jamii kwa ajili ya mji wa Chake Chake na vitongoji vyake. Kutokana na hali hiyo, maji ya kumwagilia yalianza kupungua na kupelekea bonde hilo litumike kama bonde la mpunga wa kutegemea mvua hadi hivi sasa.

Mhe. Spika, kwa kuwa bonde la Kwapweza limo katika orodha ya mabonde yanayofaa kumwagilia katika Kisiwa cha Pemba kama yalivyoainishwa katika mpango mkuu wa umwagiliaji maji. Serikali itafanya jitihada za kulirejesha katika hali yake ya asili ya umwagiliaji maji kadri ya uwezo wa kifedha itakaporuhusu.

Mhe. Spika, baada ya kutoa ufafanuzi huu, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru tena wachangiaji wote na kuwashukuru watendaji wangu wote kwa kazi ambayo nzuri iliyofanyika, hasa ninapenda kumshukuru Katibu Mkuu kwa mashirikiano yake mazuri pamoja na Naibu Katibu Mkuu Maliasili, Katibu Mkuu wa Kilimo, maafisa mbali mbali, Afisa Mdhamini, Wakurugenzi wote kwa mashirikiano mazuri ambayo tunayopeana na kuweza kupata mafanikio katika wizara yetu hii. (*Makofi*).

Mhe. Spika, pia nitakuwa mkosefu wa fadhila kama sikumshukuru sana Kaimu Waziri wangu ambaye ananipa mashirikiano makubwa wakati wote unapofika wa kupitisha miswada, wakati wa kuweka sheria mbali mbali tunakuwa tupo karibu. Kwa hivyo ninawashukuru sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waipitishe bajeti ya wizara hii ili tuweze kupata afya, kama hatukuweza kula basi tutakuwa hatuna afya. Tukiipitisha tutapata kulima vizuri, tutapata kula na wagonjwa hospitali watapungua.

Mhe. Spika, baada ya hayo, naunga mkono bajeti yetu hii ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri tunakushukuru. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Kaimu Waziri wa Kilimo wa Maliasili.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kukuomba kwamba uwaruhusu wataalamu wa kilimo washuke chini wakati mimi ninafanya *windup.*

Mhe. Spika: Ruhusa. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia tangu jana kuwa na afya njema na kuweza kukabiliana na kuwasilisha hotuba hii ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa niaba ya mwenzangu Mhe. Suleiman Othman Nyanga; ambaye angependa kuwa pamoja na sisi sasa hivi, lakini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na kudra yake ambapo kama Waislamu tunatakiwa tukubali ameshindwa kusimama hapa mbele ya Baraza hili na kuzungumzia bajeti ya wizara yake. Ninajua kwamba ni mtu mwenye hamu sana ya kufanya hivyo.

Mhe. Spika, masuala mengi yamezungumzwa kuhusu nafasi yangu kukaimu. Kwa hivyo ninasema kabla sijakwenda katika majibu ya hoja mbali mbali zilizotolewa na Wajumbe, ninapenda kusema kwamba sio kama Mhe. Suleiman Othman Nyanga hafanyi kazi katika hii wizara yake, anafanya na anakwenda ofisini na anatatua anayoyakuta pale juu ya meza, ikitokea barua anaandika, ikitokea hoja mbali ambali anajibu. Hii shughuli anaifanya lakini shughuli nzito nzito ambazo katika mazingira kama ya hapa kwa afya yake ya baridi iliomo humu ndani hawezi kustahamili kukaa muda mrefu hapa.

Kwa sababu hiyo ndio maana ninamsaidia mimi. Hata kwenye Baraza la Mapinduzi vile vile kwa mazingira ya hali ya hewa ya mule ndani, hawezi kukaa kwa muda mrefu mule, anaweza kukaa pengine kwa muda wa saa moja au saa mbili halafu baadae inabidi aondoke na aende akapumzike nyumbani. Hiyo ndio hali halisi kusema kweli. Kwa hivyo, popote alipokuwa ana dharura, mimi huwa nakaimu katika wizara hii tunakwenda pamoja, na pahala popote ambapo anaweza kufanya kazi anakwenda na anafanya kazi na wizara inakwenda, anashauriana na maafisa wake hawa, wanapanga pamoja mambo yao mbali mbali ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Kusema kweli wizara inakwenda. Tumuombe basi kama walivyosema baadhi ya Wajumbe kwamba Mwenyezi Mungu amjaalie apate afya njema ili ashirikiane na sisi katika kila kitu. Hilo ndio suala muhimu kabisa la kumuombea. Mwenyezi Mungu atujaalie afya yetu na sisi iendelee kuwa nzuri tuweze kuzifanya kazi zetu, kwa sababu ni mtihani wa Mwenyezi Mungu huwezi kujiamini ukasema mimi ni *hundred percent*, huyu mwenzangu yeye ndio kapungua na nini, haiwezekani. Mwenyezi Mungu ndiye anayejua hatma yako wewe utakuwa vipi kesho na keshokutwa utakuwa vipi.

Mhe. Spika, ninawashukuru sana Wajumbe wote waliotoa michango yao katika Wizara hii ya Kilimo na Maliasili. Ninapenda niwatambue kwamba ni:

1. Mhe. Viwe Khamis Abdalla -Kaimu Mwenyekiti
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Ali Salum Haji
4. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
5. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
6. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mahamedali
7. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
8. Mhe. Salma Mohammed Ali
9. Mhe. Asha Abdu Haji
10. Mhe. Panya Ali Abdalla
11. Mhe. Saleh Nassor Juma
12. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
13. Mhe. Mbwana Mohammed Hamad
14. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
15. Mhe. Salim Abdalla Hamad
16. Mhe. Mgeni Hassan Juma
17. Mhe. Mohammed Haji Khalid
18. Mhe. Salma Mussa Bilali
19. Mhe. Hassan Hamad Omar
20. Mhe. Mussa Ali Hassan

Mhe. Spika, hawa walizungumza kabisa katika Baraza hili.

Lakini Mhe. Spika, kuna wengine walichangia kwa maandishi, nao ni:-

1. Mhe. Farida Amour Mohammed
2. Mhe. Fatma Mbarouk Said
3. Mhe. Marina Joel Thomas
4. Mhe. Raya Suleiman Hamad
5. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman

Hawa Mhe. Spika, wamechangia kwa maandishi.

Mhe. Spika, ninapenda nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa wizara hii. Kusema kweli kama walivyompongeza wenzangu na mimi ninachukua nafasi hii kumpongeza sana. Mhe. Spika, mimi

unaponipa mtoto kulea basi huwa sipendi kumuingilia ingilia katika kazi, hupenda afanye kazi ili azizoee kazi, asiwe tena anadeka tu mabegani, hili siliwezi hapana, afanye kazi. (*Makofi*).

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Waziri Mhe. Spika, na wewe ndio shahidi. Mhe. Naibu Waziri huwa ninamuachia afanye kazi. Huko wizarani kwao sipendi anione kila mara aone aah! kumbe kuna mtu, hapana. Ninamwambia hao ni maafisa wako na wewe ni Waziri, fanya nao kazi hawa na anafanya kazi na watu wamesema hapa, anafanya kazi na anapata uzoefu kweli kweli katika kufanya kazi zake Mhe. Spika. Hivyo ndivyo tunavyofanya.

Mhe. Spika, baada ya kuwataja hawa, mimi katika majibu yangu hivi sasa sitotaja majina ya mtu kasema nini na huyu kasema nini. Naomba radhi sana Wajumbe wanikubalie. Kama alivyofanya Mhe. Naibu Waziri kuyazungumza maneno ambayo yamezungumzwa humu na kutoa majibu yake, ndivyo nitapoendelea kufanya mimi, kwa sababu kila mtu atajua hoja yake ni ipi katika hizi hoja ambazo zimezungumzwa hapa. Hichi ndicho nitakachokifanya. Naomba radhi sana na nawaomba sana Wajumbe wanistahamilie katika hili.

Mhe. Spika, vile vile ninapenda kulifahamisha Baraza lako Tukufu kuwa serikali iliwahi kununua miche kutoka vitalu vya wakulima na kuigawa kwa wakulima bila ya malipo mwaka 2012/2013. Miche hiyo ilinunuliwa kwa kuwa wizara ilipata pesa kutoka Shirika la Kununua Karafuu (*ZSTC*) kwa wakati huo.

Kwa mwaka 2014, wizara haikuahidi kununua miche hiyo ya mikarafuu lakini ilishajihisha wakulima wapate soko la kuuzia miche hiyo. Mpaka mwezi wa Mei, jumla ya miche 26,640 ya watu binafsi imeuzwa kwa bei ya shilingi elfu moja (1000) mpaka elfu moja mia tano (1500) kwa miche na hivyo kupata jumla ya shilingi arobaini na mbili milioni laki tisa na sitini elfu(42,660,000). Miche hiyo ilinunuliwa kutoka vitalu 33 vya watu binafsi.

Mhe. Spika, ninapenda kumuhakikishia Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuwa Wizara ya Kilimo na Maliasili imeliona suala la ukataji wa miti katika maeneo ya vyanzo vya maji. Suala ambalo kwa kiasi kikubwa linaathiri upatikanaji wa maji kwa shughuli za matumizi ya wananchi kwa ujumla. Wizara imechukua hatua mbali mbali za kuhifadhi vianzio hivyo vya maji.

Miongoni mwa juhudi hizo ni pamoja na kushirikiana na wanavikundi vya mazingira vya maeneo husika ikiwemo eneo la Bububu, Mwanyanya na Kianga kwa kuwapatia taaluma ya uhifadhi wa mazingira. Wizara pia imewapatia miche kwa ajili ya kupandwa katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, wizara pia inaendelea kuhifadhi misitu ya Masingini ambacho ndicho chanzo kikuu cha maji katika mito hiyo. Aidha, wizara imeongeza doria pamoja na kuwakamata na kuwachukulia hatua wahalifu wanaohusika na ukataji wa miti bila ya kuwa na vibali kama utaratibu wa sheria unavyotaka. Wizara pia imeongeza udhibiti wa matumizi ya misumeno ya moto.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili tayari imeorodhesha vifaa vyote chakavu na kuwasilisha orodha hiyo Wizara ya Fedha. Aidha, ninapenda kulijuulisha Baraza lako Tukufu kwamba kazi ya kuviuza vifaa hivyo kwa mnada tayari imeanza na itaendelea katika mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, pia ninapenda kulijuulisha Baraza lako Tukufu kuwa wizara kwa kuona umuhimu wa zao la karafuu hapa Zanzibar, imehamasisha jamii upandaji wa mikarafuu kwa kuanzisha skuli za wakulima wa mikarafuu 21, kwa Unguja 8 na Pemba 13. Jumla ya wakulima 412 wanashiriki katika skuli hizo, kwa wastani ya wakulima 20 kwa kila kikundi.

Mhe. Spika, Shehia zilizoanzishwa skuli hizo ni hizi zifuatazo:-

Unguja;

-Kizimbani

-Koani

-Donge Vijibweni

-Donge Karange

-Selem

-Kitope

-Kidimni na;

-Mwakaje

Pemba;

-Gando

-Zabibu

-Shumbageni

-Mjimbini

-Kukuu

-Ziwani

-Kwale

-Shungi

-Chanjamjawiri

Mhe. Spika, katika skuli hizo wanavikundi wamepata elimu ya kuotesha miche ya karafuu vitaluni na jinsi ya kupanda mashambani, ikiwa ni pamoja na kuekewa mazingira mazuri ya kuilea mikarafuu hiyo huko mashambani. Pia wanavikundi hao wamepata faida ya kuuza miche kwa wakulima wa mikarafuu na kujipatia kipato. Aidha, vikundi kadhaa vilivyokuwa nje ya skuli hizo vimemega maendeleo yaliyopatikana na vikundi hivyo.

Mhe. Spika, ninapenda kulijuulisha Baraza lako Tukufu kuwa mpaka sasa wizara imeshayapima maeneo 14; Unguja 11 na Pemba 3. Mashamba ya Unguja ni Kizimbani, Selem, Kijichi, Bambi na mashamba matatu Mwera, Miwani, Makunduchi, Ndijani na Bondemzungu.

Kwa upande wa Pemba ni Matangatuani, Weni na Wesha.

Mhe. Spika, ninachukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mbarouk Wadi Mussa kuwa ni kweli mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi ya Zabuni hayakufanyika kama yalivyopangwa katika bajeti ya mwaka 2013/2014, kutokana na ukosefu wa fedha kutoka serikalini. Hata hivyo, wizara ilifanya juhudi za ziada za kutafuta chanzo chengine ambapo kwa msaada wa fedha kutoka *IFAD* kupitia Programu ya *MIVARF*, wizara ilifanikiwa kuwapeleka wajumbe wote wa Bodi ya Zabuni pamoja na kitengo cha manunuzi huko Dar es salaam, kwa muda wa wiki moja kwa mafunzo hayo mara baada ya kutayarishwa kwa kitabu cha bajeti na ndio maana taarifa hiyo haikuweza kuingizwa katika kitabu cha bajeti 2014/2015.

Mhe. Spika, napenda kueleza kuwa kwa mujibu wa Sheria za Ardhi za Zanzibar, taasisi inayohusika na utoaji wa hatimiliki kwa ardhi zote yakiwemo mashamba ni Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Hivyo basi, naomba ieleweke kwamba utoaji wa hatimiliki za mashamba umegawika katika hali kuu mbili, yaani mashamba ya serikali na mashamba ya watu binafsi. Kwa upande wa mashamba ya serikali vigezo vinavyotumika katika utoaji huo wa hatimiliki ni:

- Kutuma maombi ya kuhitaji matumizi ya shamba husika kwa wizara ya ardhi
- Baada ya wizara kuyapitia maombi, muhusika kulipa gharama za upimaji wa shamba hilo na hatimaye kupatiwa hatimiliki kwa ajili ya matumizi ya shamba hilo.

Mhe. Spika, kwa kuwa Wizara ya Kilimo na Maliasili siyo inayohusika na kazi hiyo, itakuwa ni vigumu kuelezea utaratibu unaotumika kwa upande wa mashamba ya watu binafsi.

Mhe. Spika, kwa kuwa mimi ndiye ninayehusika na suala hili, basi napenda kusema kwamba mtu yeyote mwenye shamba lake, nadhani sasa umefika wakati wa kuuacha ule utaratibu wa kutumia mibono au mifursadi kuwa ni mipaka ya shamba. Ni vizuri mtu aje Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati katika sehemu ya Idara ya Upimaji, aombe kupimiwa shamba lake. Kuna watu wengi wameshaelewa juu ya suala hili, huwa wanakuja na wanaomba kupimiwa, anatozwa ada fulani, kwa ajili ya wale wanaokwenda kufanya kazi ile ya upimaji. Huwa wanampimia halafu wanatengeneza *site plan*, halafu *site plan* inawekwa katika utaratibu maalum wa kisheria na inatayarishwa hati maalum na inayoeleza madhumuni ya matumizi ya eneo lile, kama ni kilimo, kama ni uwekezaji au chengine basi inaelezwa pale, na Waziri anapelekewa anatia saini. Huo ndio utaratibu unaotumika katika masuala hayo ya upimaji wa ardhi.

Mhe. Spika, napenda kulifahamisha Baraza lako Tukufu kuwa katika kukabiliana na tabia nchi hali ambayo inaathiri uzalishaji wa mazao, wizara inafanya jitihada nyingi ya kupata njia na mbegu mbadala za mazao. Jitihada hizo ni pamoja na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji lakini pia kutafuta na kuhimiza matumizi ya mbegu bora za muda mfupi zinazostahamili ukame. Kwa mfano, mbegu za muhogo, viazi vikuu, mbegu za mpunga aina ya *Nerica*, lakini pia mazao ya mtama, uwele na mengine yanayostahamili ukame.

Mhe. Spika, kuhusu mbegu bora za zao la muhogo, muhogo ni zao lililoathiriwa sana na maradhi ya virusi. Hata hivyo, wizara ilifanya utafiti na kupata mbegu bora nne zikiwemo mbegu ya Kizimbani na Machui. Utafiti huo ulifanywa Unguja na Pemba na mbegu hizo zinapatikana katika maeneo mengi ya visiwa hivi ikiwemo Matangatuani, Wesha, Pembeni, Chake Chake, Machui, Bambi, Kizimbani na maeneo mengine.

Mhe. Spika, aina ya mbegu ya mwari pia ilifanyiwa utafiti na kweli ni nzuri, lakini inaathiriwa sana na maradhi haya ya mihogo katika baadhi ya maeneo. Mhe. Mohammed Haji Khalid jibu hilo.

Mhe. Spika, napenda kulifahamisha Baraza lako Tukufu kuwa moja kati ya majukumu ya mabwana na mabibishamba ni kutathmini mavuno ya mazao kwa wakulima. Kazi hii inafanyika kila mwaka katika kila zao ndani ya kila Shehia, kwa kushirikiana na wakulima wa mazao hayo. Katika kufanikisha zoezi hili wataalamu hao huwatembelea wakulima, mazao huvunwa na kupimwa uzito wake na wastani wa mavuno wa kila zao uliopatikana kutoka kila Shehia ndio hutumika kutoa makisio ya mavuno.

Mhe. Spika, napenda kulifahamisha Baraza lako Tukufu kuwa katika Bonde la Machigini umeme bado haujawekwa, ambao gharama zake ni Tsh. 60,000,000/= hii inatokana na ukweli kwamba fedha kwa ajili ya kazi hii hazikupatikana katika mwaka wa fedha wa 2013/2014. Ili kuhakikisha kwamba bonde la Machigini linapatiwa umeme, wizara itahakikisha kwamba suala hili linapatiwa ufumbuzi katika mwaka huu wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, kuhusu suala la fidia ya mazao. Napenda nikiri kwamba baadhi ya wakulima wa bonde la Makombeni wanaidai serikali karibu shilingi milioni 6,000,000, kutokana na kukatiwa vipando vyao wakati wa uvutaji umeme na sio wakati wa ujenzi wa barabara. Wizara itafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba deni hili linalipwa katika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Spika, napenda kujibu swali la Mhe. Mohammed Haji Khalid, pamoja na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, kuhusu vyanzo vya mapato na kuvuka kwa malengo ya ukusanyaji mapato, pamoja na makisio mapya ya ukusanyaji wa mapato kama ifuatavyo;

Mhe. Spika, ni kweli kwa miaka mitatu mfululizo Wizara ya Kilimo na Maliasili, imekuwa ikivuka lengo la makusanyo ya fedha ambayo ni sehemu ya mapato ya serikali. Vyanzo vikuu ya mapato hayo ni pamoja na mapato yanayotokana na ada na mauzo mbali mbali ya mazao ya kilimo na maliasili, ikiwemo uuzaji wa miche, ukodishwaji wa mikarafuu katika mashamba ya serikali pamoja na ada ya usafirishaji wa maliasili zisizorejesheka kama mchanga, mawe na kadhalika.

Sababu kubwa zilizopelekea kuongezeka kwa mapato ni kuongezeka kwa ufuatiliaji na msisitizo katika ukusanyaji wa mapato, pamoja na uzalishaji mkubwa wa karafuu katika mwaka 2013/2014. Aidha, Mhe. Spika, kuhusu kushuka kwa kiasi kidogo cha makisio kwa mwaka 2014/2015, kulinganishwa na mapato ya mwaka 2013/2014, kumetokana na tathmini ya makisio ya karafuu za mwaka, ambayo yameonekana kushuka kulinganisha na mwaka uliopita.

Mhe. Spika, napenda kulieleza Baraza lako Tukufu kwamba ukodishwaji wa karafuu kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili pia umesababisha kuongezeka kwa karafuu zinazouzwa Shirika la Biashara la Taifa ZSTC, mapato ya serikali pia yanaongezeka.

Mhe. Mgeni Hassan Juma, alitaka kujua kuhusu mashamba ya serikali kiwilaya. Mashamba ya serikali kwa Unguja kiwilaya ni kama ifuatavyo. Kaskazini A kuna Mto wa Maji, Kipange, Kibokwa, Kilombero na Upenja. Kaskazini B kuna Mahonda, Chechele, Mchangani, Pangeni, Donge Mchangani. Wilaya ya Kati kuna Kiboje Mkwajuni, Uzini, Kisima Mchanga, Koani, Ubago, Kidimni na Cheju. Wilaya ya Kusini kuna Mtende, Muyuni, Makunduchi na Wilaya ya Magharibi ni Kianga, Mtwango, Kibonde Mzungu, Mwera, Kijito Upele, Kwarara, Chuini, Melinane, Bumbwisudi na Kizimbani.

Mashamba ya serikali kwa Pemba kiwilaya, Wilaya ya Mkoani ni Kuyuni, Chambani na Fufuni. Wilaya ya Micheweni ni Matangatuani, Makuwe, Chwaka Tumbe, Maziwa Ng'ombe, Ngezi na Msitu Mkuu. Wilaya ya Chake Chake ni Pujini, Wesha na Mtambile. Wilaya ya Wete ni Gando, Daya, Ole Dodeani, Fundo, Weni na Msaani.

Kwa nini utalii wetu hatuufanyi kwa kuwatangaza wanyama pori wa Zanzibar ambao wanahifadhiwa ndani ya misiti yetu?

Mhe. Spika, jibu kwa Mhe. Mgeni Hassan Juma. Mhe. Spika, wizara yangu inaupa kipaumbele utalii wa kimazingira ambao unajumuisha wanyama pori ambao wanapatikana hapa ndani. Suala la kuendeleza utalii endelevu limewekwa kuwa ni miongoni mwa malengo ya wizara. Mipango yote ya kuhifadhi misitu ya wizara inajumuisha na uhifadhi wa wanyama pori, mipango shirikishi ya wanajamii, lengo lake kuu ni kuhifadhi rasilimali za misitu na wanyama pori. Wizara imeweza kushirikisha sekta binafsi.

Kwa mfano *Zanzibar World Life Safari* katika kutangaza utalii huo wa wanyama pori. Kwa mfano katika wiki iliyopita, tuliweza kuuza kiutalii Paa Nunga mmoja kwa dola za Kimarekani 4,900, Kigombo kwa dola 30. Hivi Wajumbe mnamjua Kigombo nyinyi, kakaa kama yule mnyama mkubwa asiyetajwa Makunduchi, Paa Chesi dola 300, Komba dola 300, Kima mweusi dola 100, Chindi dola 30, Ndege aina ya Kwembe dola 200 na Paa Suni dola 300.

Kutokana na wananchi wengi kushajihika katika uhifadhi wa maeneo yao hayo, wanyama kwa ajili ya utalii wa uwindaji, wananchi wa Mtende kwa kushirikiana na Mwekezaji binafsi wameanzisha kituo cha uzalishaji wa Paa Nunga pamoja na wanyama wengine.

Mhe. Spika, suala la ukataji wa miti na huduma zinazotolewa. Naomba kutoa maelezo kabla ya kujibu swali hilo. Suala la ukataji na usafirishaji wa maliasili bila ya kibali ni kinyume na sheria kwa mujibu wa kifungu namba 98 ya sheria ya misitu.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na wimbi la ukataji wa miti ovyo na uharibifu wa mazingira kwa mwaka 2014, jumla ya matokeo ya uhalifu 108 yamekamatwa na kufanyiwa kazi. Aidha, kati ya matukio hayo kesi 83 zimepelekwa Mahakamani kwa mujibu wa kifungu namba 98(1) ya sheria ya misitu na kesi 25 zimehukumiwa na idara kwa njia ya *compound* kwa mujibu wa kifungu namba 98(2) ya sheria ya misitu.

Mhe. Spika, kazi hiyo inayofanywa na Idara ya Misitu pamoja na kupunguza wimbi la waharibifu wa misitu, lakini kwa upande mwengine limeweza kusababisha wizara kuvuka lengo la makusanyo ya mapato hadi kufikia asilimia 95 ya mapato ya wizara yanayotokana na maliasili.

Mhe. Spika, napenda kujibu swali hilo kwamba fani zote za sehemu ya mapato ya serikali kwa mujibu wa sheria. Aidha, wizara kwa kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka, itaendelea kupiga vita ukataji wa miti ovyo na uharibifu wa mazingira kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, kuhusu taaluma ya umwagiliaji kwa njia ya matone, yaani *drop irrigation* tayari imeshatolewa katika wilaya za Unguja na Pemba. Wilaya ya Magharibi ni maeneo saba, Wilaya ya Kati ni maeneo matano, Wilaya ya Kusini na Wilaya ya Kaskazini B vile vile wamepewa mafunzo haya na Wilaya ya Micheweni Tumbe wamepewa mafunzo haya. Wilaya ya Wete Kangagani na Wilaya ya Mkoani Mjimbini.

Aidha, Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kupitia Idara ya Umwagiliaji Maji, inachukua juhudi za makusudi ili kueneza taaluma hii wakati wa sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi, kwa kuonesha taaluma hii Beit-el-ras, pamoja na ya magari ambapo umwagiliaji wa matone katika kilimo cha migomba na wananchi wengi waliangalia maonesho hayo.

Mhe. Spika, mradi wa Mpunga wa Umwagiliaji maji Muyuni tayari umeshaanza na kazi ambazo zimeshatekelezwa ni pamoja na kupeleka timu ya wataalamu wa Idara ya Umwagiliaji maji, kukutana na wakulima wa bonde hilo kwa lengo la kuelezea namna ya utekelezaji wa mradi huo. Aidha, kazi ya kumtafuta Mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu imeshaanza.

Haya Mhe. Jaku Hashim Ayoub, pengine yamejificha au yamefichwa na idara ndio huna habari nayo, lakini hatua hii imefika katika kiwango hicho, kwa hivyo ndio ninakupa taarifa, usitikishe kichwa, nakupa taarifa fuatilia wizarani watakueleza hatua zilizochukuliwa bila shaka.

Mhe. Spika, kuhusu kifungu namba 220701 kinahusiana na matengenezo madogo ya ofisi, ikijumuishwa ukarabati wa vyoo viwili katika jengo la Wizara ya Kilimo na Maliasili Darajani, pamoja na kufanyiwa ukarabati wa varanda inayovuja na sehemu ya kuweka mkonga wa taifa.

Aidha, kifungu cha 220702 kinahusiana na matengenezo makubwa, ambapo kwa mwaka 2014/2015, wizara imepanga kuanza maandalizi ya ujenzi wa jengo jipya la wizara; ambapo fedha ni za maandalizi ya ujenzi huo, ikiwemo kufanya usafi na kupima na kulipa hatimiliki, michoro, ramani ya jengo na kuandaa nyaraka za zabuni.

Kuhusu kifungu 21104 kinahusiana na masuala ya likizo kwa ajili ya kuwalipia wafanyakazi wote wanaokwenda likizo. Aidha, kifungu 211110 kinatumika kwa ajili ya kulipia maposho maalum yaliyomo ndani ya mishahara, kama posho la mafuta, wanasheria, masjala ya siri, simu na dhamana.

Mhe. Spika, kifungu 21116 kinatumika kugawa vikao vya Bodi ya Zabuni na vikao vya tathmini. Aina ya kifungu 21117 kinatumika kulipa posho la wahudumu kwa kupitia ndani ya mishahara yao.

Mhe. Spika, kuhusu kupungua kifungu 263167 kinachohusiana na huduma za kilimo, kutoka bilioni 3,450,000,000, kufikia bilioni 2,228,400,000. Kifungu hiki ndicho kikuu katika kutoa huduma za wakulima; kutoa mbegu, mbolea na madawa. Hii inatokana na kwamba mwaka 2013/2014 ilihusisha madeni ya pembejeo hizo yaliyotokana na mwaka 2013, pamoja na bajeti ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, kuhusu kutoa kipaumbele kwa kilimo cha umwagiliaji maji. Naomba kutoa taarifa wizara imetayarisha mpango mkuu wa umwagiliaji maji wa Zanzibar, ambapo maeneo 57 kwa Unguja na Pemba yameainishwa na kuingia katika mpango huu. Aidha, napenda kutoa taarifa kwamba mabonde matano yameingia katika mradi huu kwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji ya hekta 2,105 ya mabonde ya Cheju, Kilombero, Chaani Kibokwa, Mlemele na Makwararani. Kazi za mradi huo zimeshaanza kwa utayarishaji wa michoro.

Mhe. Spika, kuhusu suala la upelekaji wa huduma za matrekta mapema kwa wakulima. Wizara ya Kilimo na Maliasili imejipanga vyema katika kuwapatia huduma za matrekta, ikiwa ni pamoja na kununua matrekta mapya 20, pamoja na kufanya matengenezo ya matrekta 29 makongwe. Matrekta 19 Unguja na 10 Pemba, ambapo wizara itakuwa na jumla ya matrekta 49. Unguja matrekta 29 na 20 Pemba yatakayotoa huduma mara msimu wa kilimo utakapoanza. Tunategemea safari hii Mhe. Spika, kilimo kitaanza mapema sana kwa sababu tuna matrekta ya kutosha ya kufanya kazi hiyo.

Mhe. Spika, katika suala la kuzuia mtiririko wa maradhi ya wadudu waharibifu wa mimea. Wizara kwa kupitia kitengo cha utibabu wa mimea kwa kushirikiana na kitengo cha elimu kwa wakulima, vimepata ushauri na mafunzo juu ya mbinu bora za kuzuia na kudhibiti maradhi, ikiwa ni pamoja na kutumia mbegu zinazostahamili mashambulizi ya wadudu na maradhi, hususan kwa mazao ya juu kama mihogo, migomba na viazi.

Mhe. Spika, kuhusu wakulima wa bonde la Kwapweza ambalo Mhe. Naibu Waziri hapa keshalijibu. Mwanzoni mwa mwaka wa 1990 wakulima hawa walikuwa wanapata mavuno makubwa ya mpunga kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji maji, wakati ule chemchem ya Kwapweza ndio kilikuwa chanzo kikuu cha maji ya kumwagilia, lakini kufuatia uamuzi wa serikali wa kutumia chemchemu hii kama chanzo cha maji ya kunywa, kwa ajili ya mji wa Chake Chake. Maji ya kumwagilia yalianza kupungua na kupelekea bonde hilo litumike kama bonde la mpunga wa kutegemea mvua hadi hivi sasa.

Hata hivyo, kwa vile bonde la Kwapweza limo katika orodha ya mabonde ambayo yanafaa kumwagilia katika Kisiwa cha Pemba, kama ilivyoainishwa katika mpango mkuu wa umwagiliaji maji. Serikali itafanya jitihada zote za kulirejesha katika hali yake ya asili kwa umwagiliaji maji.

Mhe. Spika, kuna maswali hapa yalijichomoza. Kuna suala la Mhe, Mohammed Haji Khalid kuhusu sababu zipi zilizochangia kupungua kwa uzalishaji wa baadhi ya mazao?

Mhe. Spika, sababu zilizochangia kushuka kwa uzalishaji wa mazao na mengine kuongezeka ni hizi zifuatazo.

1. Hali mbaya ya hewa wakati huo zao lilipokuwa linazalishwa.
2. Wadudu na maradhi kwani wakati wa kiangazi uharibifu huwa mkubwa ukilinganisha na wakati wa mvua; na
3. Kuongezeka kwa baadhi ya mazao ni utaratibu huo huo niliouelezea.

Jengine ni lini Wizara italipa fidia kwa wakulima walioharibikiwa na mazao yao?

Mhe. Spika, mpaka sasa wizara haina utaratibu wa kulipa fidia kwa wakulima walioharibikiwa na mazao. Isipokuwa tatizo likiwa kubwa basi wizara huwa inaomba kutoka Jumuiya za Kimataifa kusaidia. Wakati fulani nakumbuka kwamba muhogo ulipoharibika hapa tulipata msaada wa mchele na ukasambazwa katika maeneo yote ambayo watu wameharibikiwa na muhogo wao.

Mhe. Spika, kuna suala hapa linahusu JUAMIJICHWA. Mhe Spika, zao la ndimu ndio zao lililochanguliwa na uongozi wa Wilaya ya Kati kufanyiwa kazi, kupitia programu ya miundombinu ya masoko, kuongeza thamani ya huduma za kifedha vijjini.

Programu hii tayari imeshamleta mshauri muelekezi kuwawezesha wazalishaji na kuwaunganisha na masoko wakulima wa ndimu kutoka Wilaya ya Kati, Mananasi kutoka Wilaya ya Kaskazini B, na wazalishaji wa mboga mboga kutoka Wilaya ya Magharibi.

Leo hii Mhe Spika mshauri muelekezi huyo anafanya majadiliano na timu za wilaya tulizozitaja na wawakilishi wa wakulima, kuhusu mnyororo wa thamani yaani *value chain* ya mazao hayo na namna watakavyoweza kutatua matatizo yao hasa ya soko.

Aidha jumuiya ya JUAMIJICHWA imepata fursa ya kupatiwa mtambo kupitia Programu ya *MIVARF*, kwa makubaliano kwamba wachangie gharama ya mtambo huo kwa asilimia 25. Kilichokwaza hadi sasa ni kupata sehemu muafaka ya kuweka mtambo huo kwa kuwa jengo lao halijakamilika na kufikia kiwango kinachostahiki cha kuweka mtambo huo.

Mhe. Spika, napenda kulifahamisha Baraza lako Tukufu kwamba hivi sasa kwa kutumia nguvu za wananchi, tayari tumeshaanza ujenzi wa mitaro kwa kiwango cha saruji, katika Jimbo la Koani kupitia mradi wa *GIACP*.

Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Fatma Mbarouk Said wa Jimbo la Amani, kuhusiana na Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe. Idara hii imeanzishwa mwaka 2010 kwa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe namba 5 mwaka 2011.

Mhe. Spika, kuhusiana na Zanzibar kujitosheleza na chakula. Naomba kueleza kwamba hivi sasa Zanzibar inajitosheleza kwa mazao ya aina ya mizizi ikiwemo muhogo, viazi, baadhi ya matunda na mboga mboga. Hata hivyo, bado hatujaweza kujitosheleza kwa zao la mpunga na hivyo bado tunategemea mchele kutoka nje ya nchi.

Aidha kuna mafanikio makubwa yamepatikana katika uzalishaji wa mpunga, kutokana na juhudi za serikali kupitia mpango wa ruzuku kwa wakulima. Uzalishaji wa ndani wa mpunga umeweza kukidhi mahitaji ya ndani kwa asilimia 30 kwa mwaka 2013 tukilinganisha na asilimia 16 mwaka 2010. Kwa hivyo, matumaini yetu ni kwamba uzalishaji wa mpunga utaongezeka zaidi na kuwa na uhakika pale ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji utakapokamilika.

Mhe. Mussa Ali Hassan, yeye alizungumzia kuhusu tatizo la ukataji miti mikubwa, hivyo anaiomba wizara ichukue jitihada katika kudhibiti hali hii. Mhe. Spika, suala la ukataji wa miti ni kilio kikubwa kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili, wizara kwa kushirikiana na jamii pamoja na taasisi za ulinzi imekuwa ikifanya doria za mara kwa mara, ili kupunguza wimbi la ukataji wa miti. Vile vile wahalifu wote wamekuwa wakichukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Misitu namba 10 mwaka 1996, wizara imeuchukua ushauri wao kwa ajili kulipunguza tatizo hili.

Mhe. Farida Amour Mohammed, yeye alizungumzia kuhusu uimarishaji wa kufufua zao la hiliki na pilipili manga. Mhe. Spika, wizara inaendelea kutoa elimu kwa wakulima wa Unguja na Pemba na mashamba kama ya Makuwe yanatumika kama Shamba Darasa kwa mazao hayo, pia kwa kuhifadhi mbegu za mazao hayo. Kwa mfano, hivi karibuni wakulima wa maeneo ya Michenzani Mkoani, Wawi Chakechake na Maweni Ngwachani wamepatiwa mbegu za hiliki kwa ajili ya kupanda mashambani mwao. *(Makofi)*

Vile vile hoja yake nyengine Mhe. Mjumbe ni kwamba anaomba maelezo kuhusu Shamba la Mikarafuu liliopo Matangatuani na usimamizi kuhusu uzalishaji wa mapato yake kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, kwanza napenda kumjuilisha Mhe. Mjumbe, kwamba shamba la mikarafuu liliopo chini ya Wizara ya Kilimo halipo Matangatuani, bali lipo Makuwe Mgogoni na mapato yake mwaka 2013/2014 ni shilingi milioni thalathini (30,000,000). Kati ya hizo, shilingi 6,300,000 kwa msimu mdogo na shilingi 23,000,000/= ni kwa msimu wa vuli (mkubwa). Shamba hilo lilikodishwa kwa njia ya mnada na fedha zote zimepelekwa serikalini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala la pilipili hoho na mbaazi alilouliza Mhe. Mussa Ali Hassan. Kwa kweli tunapokea kama ni rai ambayo nzuri sana ameitoa na tunategemea kwamba Wizara ya Kilimo na Maliasili itaifanyia kazi rai hiyo kwa ajili ya kukuza mazao hayo.

Mhe. Mjumbe, pia alitaka kujua bei ya soko, mbolea pamoja na dawa za magugu. Mhe. Spika, kuhusu dawa lita moja ni shilingi 25,000/=, mbolea ya TSP kilo 50 shilingi 85,000/= na urea kilo 50 shilingi 80,000/=. Sasa kuhusu ruzuku na inapokuja ruzuku bei inakuwa *TSP* shilingi 15,000/=, urea shilingi 10,000/= na dawa shilingi 20,000/=, kwa sababu kuna ruzuku serikali inafidia pale. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakubali kwamba hakuna mkamilifu, inaweza kuwa kuna hoja ambayo imezungumzwa lakini sikuijibu, naomba munistahamilie isipokuwa tushirikiane, ili tuwape nafasi wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, katika mwaka huu tumeshawahimiza vya kutosha hapa na wenyewe wapo na wamesikia maneno yetu na wameyaona, matumaini yetu kwamba tunataka nini tufanye.

Kwa kweli hichi kitendo cha Mapinduzi ya Kilimo kionekane kwa vitendo, nadhani ndipo walipojitahidi kwamba mwaka jana wakapata mpunga mwingi kuliko mwaka juzi, na mwaka huu wanategemea kupata mpunga mwingi zaidi, kwa sababu hali ilioko mabondeni ni nzuri sana. Vile vile tunategemea kwamba kilimo kitakachokuja mwakani kitalimwa vizuri sana, kwa sababu wanayo matrekta ya kutosha.

Mhe. Spika, milango ya Wizara ya Kilimo na Maliasili iko wazi, hivyo tunakuombeni mwende kwa ajili ya kupeleka rai zenu, watazipokea kwa manufaa na faida ya wakulima wetu, hivyo jambo hili lifanyeni na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatusaidia. *(Makofi)*

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili ahsante sana na hoja imetolewa. Sasa Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili. Sasa naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 20 - WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI

Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	300,000,000/=
Kifungu 0401	Idara ya Mipango na Sera	10,000,000/=
Kifungu 0701	Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka	485,000,000/=
Kifungu 1501	Idara ya Kilimo	15,000,000/=
Kifungu 1701	Taasisi ya Utafiti wa Kilimo	35,000,000/=
Jumla ya Fungu		**845,000,000/=**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na

Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Wakati nilipokuwa nikichangia nilinukuu vifungu vingi sana na kwa bahati nzuri nimshukuru Mhe. Naibu Waziri, kwa sababu yeye ndiye aliyekuwa akijibu vifungu vyao, lakini baadhi amevijibu na vyengine ameviacha.

Kwa mfano, nilinukuu ukurasa wa 59 kifungu 220500 na kifungu kidogo 220501 kuhusu vifaa vya kuandikia, sababu za msingi za kuongezeka maradufu kutoka shilingi 5,590,000 hadi 24,278,000 sikupata majibu kwa Mhe. Naibu Waziri. Hivyo, naomba anisaidie sababu za msingi kwa kuongezeka kiasi hichi mara tatu zaidi ya mwaka jana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, sina hakika kama suala hili hakulizungumza Mhe. Naibu Waziri, kwa sababu katika makabrasha ambayo ninayo mimi hakuwemo.

Lakini nategemea kwamba kuna ongezeko la mahitaji ya vifaa vya kufanyia kazi, kama vile karatasi za kutosha, wino wa *computer* pamoja na mambo mengine, ambapo hivi sasa tunaondoka katika ule utaratibu wa kutumia *typewriters* za kizamani na tunatumia *computer* ambapo wino wake ni ghali pamoja na mambo mengine, hii ndio itakuwa sababu iliyosababisha kupanda kwa gharama hizi za vifaa vya kuandikia kwa mwaka huu.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Kaimu Waziri sababu za msingi alizozitaja. Kwa kweli masuala ya kutumia *computer* hatujaanza mwaka huu tumeanza tokea miaka miwili au mitatu nyuma.

Sasa anaponiambia kwamba kuna baadhi ya vifaa vimeongezeka bado Mhe. Kaimu Waziri hajanitosheleza, naona amejibu kijumla na hivi nashindwa kufahamu sababu ya msingi, kwa sababu hata baadhi ya maeneo mengine vifaa vya kuandikia katika idara mbali mbali vipo, lakini huoni maongezeko, isipokuwa nimeyakuta hapa, na ninatumai hata hizo idara nyengine pia zinatumia *computer*.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tatizo lililosababisha hali hii karibu mara tano zaidi ni ipi sababu ya msingi, sasa anaponiambia vifaa vyengine pamoja na wino, bado sijamuelewa Mhe. Kaimu Waziri ananieleza nini.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, itabidi nieleze hali halisi ya pale ndani kwenye wizara kwa mwaka jana. Kwa kweli mwaka jana vilihaulishwa baadhi ya vifungu kwa ajili ya kukidhi mahitaji hasa ya upande wa kilimo, na wala hatukuvuka malengo ya matumizi, kwa sababu upatikanaji wa fedha haukuwa mzuri, kwa hiyo vifaa hivi hatukuvinunua vya kutosha. Kwa hivyo, mwaka huu tunataka tununue vya kutosha, ili kuweza kupata vifaa vya kutosha zaidi katika kuendesha shughuli zetu mbali mbali za kazi.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, kidogo nimemfahamu, ahsante tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nilimsikiliza Mhe. Kaimu Waziri kwa umakini kabisa wakati alipokuwa akimtetea Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili (Mhe. Suleiman Othman Nyanga), kweli hatukatai anaumwa na Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema, lakini jambo la kushangaa tulimuona kwenye Bunge la Katiba na kule kuna baridi kali, na huko tuachie sio hoja yangu.

Hoja yangu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilipokuwa na bajeti yake kabla ya siku tatu zile barabara tulizokuwa tukipiga kelele walizitengeneza kwa kuhofia bajeti. Je, wale wakulima wa Mtwango na Cheju wamelipwa wote au nusu, nataka kujua hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, ahsante naomba kumhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba fedha tulizokuwa tukidaiwa shilingi milioni 106,000,000/=, tumepiga mbio na tunaishukuru Wizara ya Fedha tulikuwa na hofu kwa kufika leo siku yetu ya bajeti fedha hizi bado hazijalipwa, lakini nataka kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba siku ya tarehe 11/06/2014 baada ya kupata taarifa kwamba fedha hizi zinalipwa sikukaa katika Baraza hili na niliondosha swali langu siku ile kwa sababu nilikuwa nijibu, kwa ajili ya

kupata uhakika kwamba kila mwenye kudai fedha zake analipwa na fedha zote zimelipwa Mhe. Mjumbe pamoja na Wahehimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ninamuamini Mhe. Naibu Waziri, kwa sababu ni Mchamungu na wala sina mashaka naye, pindipo kama ni Mjumbe wa kamati likatokezea tatizo mimi nitamtafuta yeye. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kama kuna jambo zaidi jambo lolote nadhani ni kuripoti kwa wizara kwa ajili ya kurekebishwa.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii, wakati nilipokuwa nikichangia jana kuhusu kilimo cha umwagiliaji maji; migomba Wilaya ya Kusini nilimuuliza Mhe. Waziri, kwamba katika Wilaya ya Kusini kuna kilimo cha umwagiliaji maji cha migomba, ni wakulima wangapi ambao amewatembelea angalau kwa kuwapa elimu?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Makunduchi kuna kilimo cha umwagiliaji maji wa migomba na mimi mwenyewe nimeshawahi kwenda kutembea na nimeshawaona wakulima hao kupitia wakufunzi wetu wa *Field Farmer School.*

Nina imani Makunduchi ndiko walikoinuka katika kilimo hichi na kupata taaluma hizo na bado wanaendelea kupewa taaluma hizo, ndio maana Makunduchi ikawa imeshajihika sana katika kilimo hichi cha umwagiliaji maji.

Vile vile tumefanya ziara pamoja na Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kwenda Makunduchi kuwatembelea wakulima hawa, ili kuona ufanisi wao na bado tutaendelea kuwapitia na kuwapa elimu, kwa sababu watu wa Makunduchi inaonesha wanao muamko mkubwa juu ya suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti, ni wakulima wangapi ambao wamewatembelea, maana yake amesema kwamba kuna wengi, na kweli wapo wengi, lakini wangapi ambao wamewatembelea?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli siku zote siwezi kusema neno la uongo, kwa sababu nilipotembelea sikuhesabu kama huyu Abubakar au Said ama Ali nikafanya hesabu, sikufanya hesabu hiyo, lakini katika ziara yangu nilipokwenda tayari ninajua kwamba hapa nimekwenda na kuwatembelea hawa na wale, kwa hiyo idadi sikuweka katika kichwa changu ni wakulima wangapi. Sasa kama analitaka hilo la idadi *inshaallah* katika kumbukumbu tutamletea kwa maandishi juu ya hao wakulima tuliowatembelea. *(Makofi)*

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu ya Mhe. Naibu Waziri, lakini hawa wakulima wanalalamika kwamba hawatembelewi na viongozi wa Wizara ya Kilimo na Maliasili kama vile hawawaoni mabwanashamba na wala maasifa wa wizara kwa ajili ya kuwapa ushauri. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo naomba tuendelee. *(Makofi)*

Kifungu 0401	Idara ya Mipango na Sera	377,129,000/=
Kifungu 0402	Chuo cha Kilimo Kizimbani	427,000,000/=
Kifungu 0701	Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka	

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kuna kifungu nilijaribu kukiulizia na nimshukuru Mhe. Naibu Waziri hichi alikijibu, lakini kidogo majibu yake hayajanitosheleza kifungu 221000 huduma za kilimo, hapa niliulizia sababu za msingi za kuongezeka kutoka shilingi 51,000,000 hadi 80,310,000.

Mhe. Naibu Waziri wakati akijibu maswali yangu hapa alisema tu kwamba hili eneo lina huduma nyingi, kama vile mambo ya uoteshaji pamoja na mambo mengine. Sasa nimejitosheleza na majibu yake juu ya hayo mahitaji mengi, lakini ninachotaka kukijua ni *specific area,* ni eneo gani ambalo lilisababisha kuongezeka kwa karibu

shilingi 30,000,000. Mhe. Mwenyekiti, masuala ya kwamba kuna kazi nyingi sijakataa, lakini ni eneo gani ambalo limesababisha mwaka huu kuongezeka karibuni milioni 30 kutoka 50 kwenda 80.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia haya maeneo yote ni maeneo mazito, ukija suala hasa la eneo kubwa ununuzi wa mbegu kama mlivyosikia hapa kama tulikuwa tuna deni karibu ya milioni mia mbili na juzi tumelipa milioni mia moja. Kwa hivyo, hili nalo ni suala mabalo nalo ni zito, ukija kuna huduma za kinga na janga la moto linapotokea, linakuwa si dogo, ulipoingia moto Jozani, serikali nzima ilitaharuki. Kwa hivyo, hili nalo ni eneo ambalo halina masihara, serikali nzima huhamia kule, halina masihara, vifaa vingi vya serikali na wananchi nao pia hujitolea kule.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, ni suala ambalo kwa kweli tunakuomba Mhe. Mwakilishi tuachie hizi fedha, si nyingi kiasi hicho unavyoziona nakuomba Mhe. Mwakilishi tuachie tukubalie na yote haya yana umuhimu, ukija kwamba suala jengine la hizi kazi za doria, haya maeneo yote yaliyotajwa kusema kweli yana umuhimu ukiacha hayo mambo mawili ununuzi wa mbegu, huduma za moto na haya mambo mengine yote matano yaliyotajwa nakuomba Mhe. Muwakilishi tukubalie kwa hili.

Mhe. Ali Salum Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, nimefahamu unajua Mhe. Naibu Waziri, mimi ni mkwe wangu na ndio maana hata anapojaribu kujibu maswali yangu, anajaribu sana kuniangalia mkwewe atafanya nini, lakini sina tatizo na hilo kuliachilia hilo fungu, lakini nilitaka kujua tu sababu mbili za msingi ambazo amezieleza hapa, hii sababu ya moto na sababu ya mbegu ambazo Mhe. Jaku Hashim, alikuwa akilalamika sana. Sasa hili suala la moto nataka kujua katika suala la moto, najua watu wa moto ni wa Zimamoto labda kama kuna fungu linaingia hapa watu wa Zimamoto, kuna fedha ambazo zinapelekwa wakati yanapoingia majanga ya moto hilo la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili, pamoja na jibu la suala la mbegu, nitakuwachia fungu, lakini nilitaka kujua tu, ukiachilia mbali wakulima ambao mmewalipa pesa zao za mbegu, lakini bado kuna kilio na jana nilizungumza hapa kwamba kuna wengine ambao wana mbegu zimo ndani na hazijenda kununuliwa na mbegu zile zinawatia umasikini, imefikia pahala mimi nimewashauri tu wajaribu kushauriana na Wizara ya Kilimo, ikiwezekana ile mbegu bora wale wenyewe ili wapate manufaa ya chakula, kuliko kuweka ndani Wizara ikawa haiendi kununua, sasa nataka unieleze Mhe. Waziri, nitakuachia fungu hili kwa sababu nina imani utakuwa unazo pesa, wale ambao wana mbegu ndani, muda gani utakwenda kumalizia matatizo yao ili waondokane na tatizo ndugu zetu? Kama kilivyozungumza kitabu jana moja ya sera zenu ni kuondosha umasikini, sasa kama watu wana mbegu ndani, umasikini hamjauondosha, nitakuwachia fungu, baada ya kuachia fungu, muda gani ambao mbegu ambazo zimo ndani ya majumba ya watu mtaenda kuzimaliza kuzinunua?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, mbegu tunazihitajia na ni kweli wananchi wetu na wakulima wetu wamelima kwa suala la kuondosha umasikini, kilio kikubwa kilichokuwepo ni kuwakopa, lakini pia, kukopa hatukukatazwa, Mtume anasema; "mwenye kukopesha anapata fungu la kumi", lakini pale pale pana kulipa na mbegu hizi, hata juzi nilipokwenda kulipa pesa hizi wakulima wakatwambia wana mbegu ndani, kweli wanazo na nilijaribu kuwambia, je, mukiuza nje na naomba wakulima wasinituhumu vibaya kwa hii lugha niliyoisema na walisema kwamba Mwakilishi yoyote atakayesema mbegu zao ziuzwe nje, zisiuzwe katika Wizara, basi watafanya maandamano, nikawahoji, kwa nini? Wakasema tukiuza kwenye Wizara, tunapata faida kubwa kuliko tukiziuza nje. Kwa hivyo, tutakapopata pesa, *Inshaallah* tutazinunua sisi mbegu kwa sababu tunazihitaji, wakulima wetu wamehamasika kulima.

Mhe. Ali Salum Ali: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0701 Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka- 1,605,448,000
Kifungu 1101 Idara ya Umwagiliaji Maji-

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nimesikiliza Mhe. Waziri, kwa makini kabisa, alinambia kule Muyuni tayari wataalamu wamekwenda, lakini alikuwa nae mtaalamu mmoja tu Bwana Mshenga, kwanza nimshukuru sana kwa kusimamia mradi huu na nimpongeze kwa dhati kabisa, lakini bado mimi ni muajiri wa wananchi wa Jimbo la Muyuni na hii kazi nafanya kutokana na jitihada za Mhe. Mbunge na Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni na kama sikusimamia kisawa sawa, nitakuwa sijafanya haki hata kwa Mwenyezi Mungu, nataka kujua tu, lini kazi hii itaendelea tena? Isiwe kwenda na kurudi, tunataka vitendo.

Mhe. Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ashukuru na afurahi na wananchi watafurahi kusikia kwamba bonde la Muyuni limeshachaguliwa kuingizwa katika mpango wa *Irrigation* hiyo, ni hatua ya mwanzo, unapotengeneza *Irrigation,* lazima kwanza uli-*save* bonde lote ili uone misingi yake, utaielekeza wapi, kisima kitakuwa wapi na uandike *Study* na *design* maalum, ukishaandika hiyo *design*, ndio tena uanze kuchukua zana, uanze kwenda kutengeneza hilo bonde kwa ajili ya *irrigation* inayotakiwa. Kwa hivyo, *irrigation* sio baada ya kuamka tu, itakuwa tayari kuna kazi ambazo lazima zifanywe na wataalamu wamesema kwamba tayari wameshapeleka mtu kwa ajili ya kulitizama lile bonde na kulitengenezea hizo *contour reading* zake, pamoja na mambo mengine kwa ajili ya kutengeneza hiyo ardhi kwa ajili ya kutengeneza hicho kipande cha *land development* kwa ajili ya *irrigation.*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, Mhe. Jaku, aendelee kuwa mstahamilivu na keshafanya kazi nzuri, kusema kweli kwa sababu suala kalipigia kelele muda mrefu sana, kwamba lile bonde litengenezwe kwa *irrigation* na Wizara ya Kilimo wamekubali kulifanya kuwa *irrigation* na litafanywa kuwa *irrigation* asiwe na wasi wasi na wananchi najua wanasikia huko, wawe wastahamilivu na wawe watulivu na *program* zinaendelea *Inshaallah.*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri Mkongwe sana katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, niendelee kumshukuru, tuendelee.

Kifungu 1101 Kifungu 1001	Idara ya Umwagiliaji Maji-	725,370,000

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru, mimi kidogo nilikua nataka maelezo ya ziada Mhe. Waziri, alitujibu hili suala, lakini mimi sikuwa nimemuelewa vizuri kwenye fungu 220700 Matengenezo ya Ofisi, nilikuwa nimezungumza kwenye suala hili la ujenzi matengenezo madogo ya Ofisi, nimemwambia sina matatizo sana kwenye matengenezo madogo, lakini hapa kwenye 220702 Matengenezo makubwa ya majengo, ametoa maelezo ya kwamba wanaandaa anaanda michoro, lakini ukiangalia katika miaka mitatu yote, hili fungu linachukua fedha, kuna milioni 20 mwaka juzi, mwaka jana milioni 29 na mwaka huu kuna 32 katika matengenezo hayo hayo, kwenye matengenezo madogo madogo, najua ni *repair* ndogo ndogo za Ofisi amezitolea maelezo kwa jengo lake lile.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hapa bado sijapata maelezo vizuri, kwa sababu hata huo ujenzi wa Ofisi za Serikali unasimamiwa na Wizara ya Fedha ukiangalia kule kwenye fungu tutakapokuja kuangalia Wizara ya Fedha, kule kuna fungu nono kabisa kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Serikali. Sasa kama ni jengo jipya la serikali usimamizi wake najua unakuwa unakwenda kule Wizara ya Fedha, sasa hapa sijui iko je, naona kuna fedha hizi, mimi nazihisi hazina matumizi, labda Mhe. Waziri, atusaidie maelezo ya ziada.

Mhe. Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, ataona kwamba mwaka juzi tulikuwa tuna milioni 20 pale kwa ajili ya matengenezo makubwa ya jengo letu la Wizara, lakini mwaka jana tumewekewa milioni 29, napenda kumpa taarifa kwamba pesa za mwaka jana milioni 29, hivi hatukuzipata, asisahau kwamba tulikuwa na upatu maridadi wa kununua meli. Kwa hivyo, pesa zile zimekwenda katika ununuzi wa meli, kila Wizara imetoa mafungu ambayo inaona yanaweza kuhamishika, wamepeleka kwa ajili ya ununuzi wa meli ambayo tumeshaambiwa na Wizara ya Mawasiliano na Wizara ya Fedha kwa jumla, sasa mwaka huu imekuwa fedha hizi pamoja na kuwa Wizara ya Fedha ndio itatulipa pesa za ujenzi, lakini matayarisho ya ujenzi mnafanya wenyewe Wizara mambo ya kutafuta ramani na mambo mengineyo mnafanya wenyewe, mnapoanza kazi Wizara ya Fedha inaingia kwa ajili ya kukulipeni hizo pesa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, majibu ya Mhe. Waziri, yanazongana kidogo kwa sababu ukiangalia matengenezo madogo, maana yake ni hizo *repair* ambazo amezungumza, zingefanyika kupitia hilo fungu 220701, ndio hayo matengenezo ya Ofisi, kwa sababu ni jengo limeshajengwa, lakini labda mnapiga rangi, mnagonga gonga, tunaita matengenezo madogo madogo, lakini bado huku chini kulikuwa na fungu, bado lilikuwa linaingia fedha na hizi ambazo anasema kwamba sasa anataka kutengenezea ramani, sijui na kitu gani. Mimi ndio napata shaka, kwa sababu kama ni matengenezo, hizi fedha zisingegawika katika mafungu haya, kuna matengenezo makubwa, maana yake huu ni ujenzi mpya anaouzungumza.

Mhe. Mwenyekiti, kama ni ujenzi mpya, basi huu unakuwa uko kwenye Wizara ya Fedha, sasa huku kuna fedha amechukua mwaka juzi na mwaka jana, katika matengenezo madogo madogo na kwenye matengenezo makubwa anakuwa anaomba tena, sasa anaomba mafungu yote mawili, anayaombeya katika kutengeneza kitu kimoja, mimi nimepata wasi wasi kwamba hizi fedha zitakuwa hazina matumizi hapa, kwa sababu hata huko Wizara ya Fedha ukiuliza wao, ndio wanaoshughulikia na mambo yote hayo, kwa sababu yale majengo ni mradi

wa serikali katika kujenga Ofisi mpya za serikali, ni mradi ule upo na tukija tukitizama Wizara ya Fedha, tutaukuta pale umetengewa pesa nyingi mwaka jana, ata sijui bilioni ngapi zile. Kwa hivyo, kila mwaka zipo fedha pale kwa ajili ya majengo ujenzi wa Ofisi za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hizi yeye Mhe. Waziri, ameshachukua huku kuna 14 katika matengenezo madogo madogo, mwaka jana alichukua 12 katika matengenezo madogo madogo na mwaka juzi ana 14 katika matengenezo madogo madogo jengo hilo hilo moja, ina maana kila mwaka linajengwa, sasa sijui kama ni bovu lote au vipi, lakini kwenye matengenezo makubwa pia anachukua tena, ukiangalia hii bajeti ingawa anasema huku kazichukua, sina uhakika kama kweli zilikwenda kwenye ujenzi wa meli, lakini ni fedha ambazo sisi tulishazitenga kwa ajili ya jambo fulani, hapa ameziombea kwa ajili ya ujenzi, sasa kama zilikwenda kwenye meli itakuwa umefanya uhaulishi huo sawa, watakavyokuwa wamefanya, lakini mimi nasema zimekwenda kwenye matumizi haya ambayo ameyaombeya hapa, huo ndio wasi wasi wangu.

Mhe. Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mtando, kwamba aondoe wasi wasi, haya majina yaliyomo katika vifungu ni majina ya kudumu ambayo yapo katika utaratibu wa bajeti wa Wizara ya Fedha, unapokuwa una tatizo unataka kulishughulikia, wao wanatizama tuweke wapi kifungu hichi, pesa zao tukuwekee wapi, sasa nakuwekea pale hilo moja. La pili, nataka afahamu Mhe. Mtando, upapopewa mwaka juzi milioni 14, kuna suala ulitiliwa hizo fedha au hukutiliwa, hilo ni suala jengine lipo, maana unaona namna ya uingizwaji wa hizo fedha, pengine hukutiliwa hizo fedha, lakini ndio zilizokuwa *located* mwaka juzi na mwaka jana ndio zile zile zilizowekwa 12 milioni, nakuja suala lile lile umetiliwa au hukutiliwa. Sasa fedha zinazoingizwa kwa nafasi siku zote ni fedha za mishahara kwa sababu huwezi kuwaweka watu na njaa, hizo ndio zinaingizwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini wakati mwengine linapotokea tatizo kama hilo nililolizungumza juzi la meli, vile vile na wewe unashauriwa utatoa pesa katika kifungu gani, sasa unajua kwamba kuna vifungu vinaingizwa, kuna vifungu haviingizwi, sasa na wewe unacheza mchezo wako, unawaambia Wizara ya Fedha chukueni kifungu fulani, maana hamna mtindo wa kukiingiza hichi, wanakichukuwa, kwa sababu zimesharuhusiwa zitumike, zile zinatumika na zinakwenda katika shughuli maalum.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sasa tunapotaka kwenda kwenye jengo jipya, maandalizi ya mwanzo ni ya Wizara yanyewe, ndio inayotengeneza yale maandalizi ya mwanzo ya *site plan*, mambo ya ramani na mambo mengineyo yanatengenezwa, unapokuwa tayari, sasa Wizara ya Fedha ndiyo inatekeleza mradi wa kujengeya, tayari una ramani mkononi na Wizara ya Fedha ndio wanatengeneza utaratibu wa kuendeleza ujenzi ule katika mradi ule wa fedha, ndivyo ninavyomjibu asiwe na wasi wasi, zikiingizwa unazitumia, lakini kuna vifungu vingapi ambavyo havikuingizwa kabisa kwa mwaka huu, hata kuna mengine nisije nikasema mengine mengi, *Inshaallah*, maana mengine hayaingizwi, itakuwa inajibomoa mwenyewe.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi namheshimu sana Mzee wangu huyu na maelezo yake haya anajibia kwa uzoefu wa kwamba yeye ni Mhe. Waziri, muda mrefu kama kasema hapo Mhe. Jaku, *long service* inasaidia anazungumzia uzoefu, lakini tukiangalia uhalisia hizi fedha wanaziomba kwa umuhimu na ndio maana wakaziwekea mafungu kwamba kifungu fulani cha matumizi kadhaa, kifungu fulani kwa matumizi kadhaa na ndio anaomba na sisi tunawaidhinishia kwa mujibu wa walivyoomba. Hawaji na maneno tu hapa kwamba tunaomba fedha hizi, basi ikawa ndio zote, ndio maana wanazichambua mafungu kwa mafungu na hapa tunapopitisha, tunapitisha kifungu kwa kifungu, tunazuia kifungu, hatupitishi maneno. Kwa hivyo, tunvyozitoa, ina maana zikatumike kama ambavyo zimeombewa, hata ile sheria ya fedha inasema hivyo hivyo unavyoziomba, ndio utakavyozitumia.

Mhe. Mwenyekiti, lakini mimi sina haja ya kutaka kumzuilia hili fungu Mhe. Waziri, nilikuwa nataka tu ufafanuzi zaidi, mimi naomba tuendelee.

Kifungu 0301 Idara ya Uendeshaji na Utumishi- 1,543,027,000

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Salum Ali, nilipokuwa naangalia angalia, nikaona kutupu, nikasema tumekwisha, sasa haya lete habari yako.

Mhe. Ali Salum Ali: Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji nilihoji vifungu vingi sana na Mhe. Naibu Waziri, wakati ananijibu alijaribu kunitolea ufafanuzi kwamba sababu ya kuongezeka haya mafungu, yaani kuondoka katika Idara nyengine na kuwa katika Idara ya Uendeshaji, nilikuwa nikichangia ukurasa wa 66 na 67, ukurasa wa 66 nilizungumzia fungu la 220101, Gharama za simu nikataka kujua kilichoongezeka kutoka

milioni 3,600,000/= mpaka milioni 15,200,00/=, karibuni mara nne zaidi, lakini pia, nilizungumzia habari ya safari za ndani na nje, ilikuwa katika kifungu cha 220300, Gharama za safari, jumla ya fungu kuu kutoka milioni 14,480,000/= mpaka milioni 87, lakini katika ukurasa wa 67, nilizungumzia gharama za mafuta fungu 220400 kutoka milioni kumi na mbili, ukiangalia magharama ya hapa kutoka 12,982,000/= mpaka milioni 52, hili la mafuta atanijibu, sijapata jawabu lake, lakini hili la safari jawabu aliyonieleza Mhe. Naibu Waziri, kwamba gharama za safari katika Idara zote zitakuwa zimeondoshwa na zimewekwa hapa, ndio ukaona hapa zipo pesa nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini baada ya kuwa ananijibu tu Mhe. Naibu Waziri, nilikuwa najaribu kupitia kila Idara, yaani Idara zake zote ya Maliasili, za Misitu, za nini na kila Idara ukija ukiangalia zote zimewekwa mafungu ya safari, sasa nilitaka kujua hilo jawabu ambalo amenipa kwamba wameondosha pesa kutoka maeneo mengine, wameleta hapa ni maeneo gani ambayo yameondoshwa hizo fedha, kwa sababu kama utaangalia kila Idara pesa hizi zipo za safari ziwe za ndani au ziwe za nje, sasa haya majibu kidogo hayajanitosheleza. Kwa hivyo, hili la safari atanipa majibu ya ziada, lakini kwa haya mafungu mengine mawili ya gharama za simu na gharama za *petrol*, atanipa sababu za kuongeza haya mafungu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, katika gharama za simu, fungu ambalo unasema limezidi, anajua kwamba mwaka uliopita 2000 au 2001 sio mwaka tunaokwenda, kila siku matatizo yanazidi au kila siku gharama zimezidi, umeme tulipiga hapa hapa kelele kwamba umeme siku hizi umepanda. Kwa hivyo, tuone kwamba kila kitu kinapanda, halafu isitoshe kwamba na kila mawasiliano katika Wizara kama zamani ilikuwa mna simu ipo katika sehemu ya Ofisi moja au Ofisi mbili, ina maana Ofisi zinapanuka. Kwa hivyo, kila Ofisi kunakuwa kuna simu. Kwa hivyo, gharama zitapungua zitaongezeka, ikiwa kulikuwa kuna Ofisi ya Waziri tu na ya Naibu Waziri hakuna, lakini na Naibu Waziri na yeye katiliwa simu gharama zitapungua au zitaongezeka. Kwa hivyo, hizi ndio sababu zinazofanya kwamba kuongezeka ikiwa kuna upanuzi wa kuongezeka maofisi ndani ya Wizara, bila shaka na gharama zitaongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, amezungumza habari ya safari za viongozi za Wizara na safari nazo pia ni hivyo hivyo, safari za Wizara katika Wizara yetu kuna safari ambazo zinawahusu Makatibu Wakuu, Manaibu, kuna Idara ya Utumishi ambazo kuna safari za lazima mtu ende na si kama anakwenda bure tu, kule anakokwenda, anakwenda kwa kutafuta ufanisi wa Wizara yetu ya Kilimo kama wanavyojua. Wizara ya Kilimo inataka mambo mengi na kufuatilia nje, mambo ya utafiti. Kwa hivyo, mimi naomba kwamba asione kuwa haya mafungu yamenona tu bure bure. Mafungu yamenona kwa kazi maalum na viongozi wanapokwenda katika hizi ziara kwa kwenda kutafuta ufanisi wa Wizara yetu.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, mimi sikatai kuongezeka, lakini tunachohitaji ni ufafanuzi kwa sababu hizi pesa ni za wananchi na tumekuwa tukipiga kelele, tunakuwa tunapata mashaka kuingizwa katika maeneo kwa kutokuelewa wakati kuna maeneo ambayo yanahitji *priority,* lakini hatuwekewi. Mhe. Naibu Waziri, anavyonijibu kwamba wameongeza kwa sababu ya Ofisi, unajua ninachopata mashaka huku, kwa sababu ya gharama.

Mhe. Mwenyekiti, karibuni miaka 3 nyuma kutoka 2011/2012 milioni tatu, 2011/2012 milioni tatu na elfu kumi, mwaka jana milioni tatu na laki sita. Miaka mitatu yote ukiangalia huu ndio ulikuwa wastani wa matumizi yao ya gharama ya simu, lakini mwaka huu imeongezeka karibuni mara 5 au mara 4. Sasa kama kuna Ofisi zimeongezeka, basi anambie kwamba kuna Ofisi au Idara fulani imeongezeka, ndio iliyosababisha kuongeza hii gharama, lakini katika hiyo miaka mitatu yote ya nyuma gharama yake wastani ni milioni tatu, safari hii imetoka kutoka milioni tatu mpaka milioni kumi na tano, sasa ongezeko ni kubwa maradufu na ndio maana nataka kujua limeongezeka wapi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, kama kuna Idara aieleze, mimi sina tatizo, lakini na jibu la pili katika masuala ya safari. Suala la safari sikatai kwamba tuna mahitaji ya Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Waziri, kusafiri sina tatizo, lakini jibu la mwanzo ilikuwa kwamba wameondosha katika baadhi ya Idara. Kwa hivyo, safari zote zimekuwa hapa na mimi nikajaribu kuangalia Idara zote juu ya safari zao. Idara moja baada ya moja, nilikuwa kila Idara naangalia kwamba hizi pesa zimetengwa na jawabu la mwanzo niliambiwa zimeondoshwa kule kwamba zimetengwa hapa, lakini pia, ukiangalia hiyo gharama ya ongezeko, basi kutoka milioni kumi na nne mpaka milioni thamanini na saba, karibuni milioni sabiini kutoka kumi na nne mpaka thamanini na saba. Sasa mimi sikatai sana.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho, sikujibiwa suala la mafuta kama wameongeza magari au vipi, Mhe. Naibu Waziri, hakulijibu kabisa, lakini najua tatizo, tatizo ni kwamba kichwa chenyewe hakipo.Tuendelee.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi nilipokuwa nachangia katika Idara hii ya Uendeshaji na Utumishi nilihoji kuhusu uajiri wa vijana ambao kuna vijana wamesoma miaka 3 mpaka 4 nyuma, lakini bado hawajaajiriwa. Mhe. Naibu Waziri, alinijibu kama Wizara itakapopata fedha inaweza ikaajiri na pia wana mpango wa kuajiri katika mwaka huu wa fedha. Nilitaka kujua katika uajiri huo, je, Wizara imezingatia kuwachukua wale waliosoma zamani au wanaajiriwa tu wale ambao wapya bado wale wakiendelea kubakia. Nilitaka kujua hilo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Panya, suala la uajiri siku zote tunasema liko tete ni kweli, lakini katika Wizara ya Kilimo, mara nyingi Wizara ya Kilimo inaposomesha wanafunzi wake mara nyingi hutoa ajira kwa wale wanafunzi wake wanaomaliza na kwamba wale wanaomaliza zamani, ndio wanaoajiriwa. Utaratibu ni wa kuajiri kwamba Utumishi inapotoa matangazo kuwa Wizara ya Kilimo na Maliasili, inataka kuajiri sifa hizi hizi, kila mmoja anapeleka barua yake Utumishi. Sasa katika kupeleka Utumishi, kila mmoja anasikiliza masikio yake kwamba mimi mwanafunzi tayari nataka ajira, Wizara ya Kilimo imetoa tangazo kwa uajiri ninapeleka barua yangu, anayebahatika mapema barua yake tayari ambaye aliyesoma mwanzo anaingia katika mkumbo ule na kuja *interview*, wanaajiriwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna wengine ambao kama kweli wapo ambao walisoma nyuma, anakuja watu wameshaajiriwa, lakini ndio analeta kwamba mimi sijasikia tangazo, watu wote wameshafanyiwa *interview*, kwa kweli yule mtu muda ule unakuwa ushapita, bado kama mimi Naibu Waziri wanakuja watu kama hao, nawaambia subiri litakapotoka tangazo tena, ili ukaombe upate ajira. Kwa hivyo, tunalifanya zinatokea kitu kama hicho kama ubinaadamu, kwamba mwengine anakuwa hakusikia hata tangazo, yuko maskini keshamaliza chuo anajishughulisha na mambo mengine, hata siku anapopata tangazo, watu wameshaajiriwa. Kwa hivyo, hili Mhe. Panya, linatokea, lakini na utaratibu tunaufuata *Inshaalah.*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri, lakini mimi nataka tu kumuuliza iwapo watajitokeza vijana ambao sifa wanazo na pengine walifata hizo taratibu, lakini ndio wakakosa kuingia katika huo mpango Mhe. Naibu Waziri, ikiwa mara hii watakuwa wamekosa kuingia na pengine mwakani mkawa mna uajiri mwengine utakuwa tayari tuwalete hao wanafunzi ili wakae tayari katika mpango kusubiri na ukafika wakati wa ajira tukaona wanapewa kipaumbele wanafunzi hao? Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo kuwa kazi ya uajiri inakuwa ya Tume ya Utumishi. Masuala ya uajiri kama tutayabeba sisi Wizara ya Kilimo, kwa kweli saa nyengine tutakuwa tunajitwika lawama. Kwa hivyo, kazi ya utumishi wakati hii ni kazi yao, mimi nina imani watafanya kazi vizur. Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Panya, suala la ajira mara nyingi hebu tulipelekeni Wizara ya Utumishi mtatusaidia kwa hilo.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru kwa majibu ya Mhe. Naibu Waziri, lakini tuelewe vijana wetu hawa wanakuwa wanyonge na huwa wanahitaji saa nyengine tuwakwamue. Kwa hivyo, mimi nashukuru na nitakuwa niko tayari kufuatana na Mhe. Naibu Waziri, zinapofika ajira ili tuone vijana tunawasaidia na wanafanikiwa.

Kifungu 1301 Idara ya Uendeshaji na Utumishi- 1,543,027,000
Kifungu 1401 Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe-

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, kwa kunipa fursa hii kwenye kifungu ambacho mimi nimechangia kwa maandishi na nilimpelekea Mhe. Kaimu Waziri na nikamuuliza kuhusu kifungu hiki, kwanza nilitaka kujua ile sheria ambayo ilianzishwa Idara hii mwaka gani na nilikuwa na sababu zangu kwamba nimeona katika majukumu, jukumu moja la Idara hii ni kuratibu kazi za uhakika wa chakula na kwa kweli nimeona kama kazi zake moja ni kuratibu mambo haya, nikaona kwamba sasa hivi Idara hii kazi itakuwa haina kazi. Kwa hivyo, nikaomba anijulishe kwamba ni sheria gani na mwaka gani na vile vile, katika *vote book* hii nimetizama katika kurasa zote sikuona hasa lile jukumu ambalo limepangiwa Idara hii ambayo ni *food reserve*, sikuliona na vile vile, nimetizama kwenye *vote book* hili ni kwamba ni gharma za vifaa, viburudishaji, gharama za safari, gharama za mafuta mengineyo, lakini hata hivyo, sikuona kifungu ambacho hasa kitakuwa na hili jukumu lilikuwemo humu.

Mhe. Mwenyekiti, unajua kwa kweli huwa ninauliza na mara nyingi husema sitaki kupiga buti, navipitisha vifungu vyote, lakini kutokana na hali nimeona kwamba inawezekana Idara hii ipo ipo tu, lakini yale majukumu

yake hasa hayapo. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri, anifafanulie vizuri na halafu sina haja ya kusimama tena isipokuwa akinijibu vizuri, basi naomba tuendelee.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Fatma, juu ya Idara hii kazi anayonipa, ni ya uchambuzi na nitajaribu kuichambua. Hii Idara ina mambo mawili; ina uhakika wa chakula na ina lishe. Katika upande wa uhakika wa chakula, hapo ndio tunazungumzia ununuzi wa chakula cha akiba, utayarishaji wa maghala ya kuwekea hicho chakula cha akiba, pamoja na ununuzi wake na muda wa kuweka chakula ghalani, ukimalizika kutoa taarifa kwamba sasa hivi chakula itabidi kiuzwe, kwa sababu hakiwezi kuendelea kungojea tena, kwa sababu hali ya nchi bado ingali amani kinunuliwe chengine kiwekwe, ndio unatafuta uhakika wa chakula.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, kutoa ushauri kuhusu kilimo chenyewe cha kulima na kwa ajili ya lishe, Idara hii ndio inasaidiwa ishughulikie masuala ya kuwaelimisha watu juu ya chakula bora ni nini katika kilimo, ili walime katika mashamba yao. Wenzetu nchi zilizoendelea wanafundishwa suala hili la lishe na wanalima mboga mboga mpaka katika penu za nyumba zao zinafanywa na Idara hii. Unalima karoti, tungule, pilipili boga na tomato pembeni pale kwenye nyumba, kwenye madoo na vipolo, pamoja na mengineyo kuondoa lile suala la kula tu mpaka tukashuka vitumbo, tukawa na *obesity* hii ambayo ni tatizo kubwa sana. Ni kazi ya Idara hii na anayewekwa hapa mara nyingi anakuwa ni mtaalam wa masuala hayo. Kwa hivyo, Idara sio ipo ipo, kazi inaendelea kufanya na Idara hii.

Mhe. Mwenyekiti, tulichokwama mpaka sasa hivi ni kwamba hatujapata fedha ya kulitengeneza lile ghala na kuanza kutoa ushauri wa ununuzi wa chakula ili pamoja na kuwa kuna michele inauzwa, lakini pale kuna mchele ndani unangojea kama tatizo litatokea na baada ya miezi 6, inabidi chakula kile kitolewe na kiuzwe na badala yake kinunuliwe chengine kiwekwe pale.Kwa hivyo, unakuwa unatia chakula unatoa, unatia chakula unatoa, ndio kazi za Idara hii. Kwa hivyo, hii Idara sio ipo ipo tu, hii Idara tukiongezwa wataalam, hii ndio Idara itakuwa mafunzo ya lishe, kilimo cha lishe na mambo mengineyo ili wananchi wawe na afya nzuri na wasiwe katika mambo tunayoendelea, sasa hivi vitumbo vitumbo na mambo mengineyo. Ahsante sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, kwa maelezo ya Mhe. Kaimu Waziri, naomba tuendelee.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, aliyoyatoa hapa mimi nilipokuwa nikichangia, niliomba kujua kuhusu suala la uhakika wa chakula na lishe. Ninachokiomba baada ya harakati zote ambazo tayari zinaendelea, pamoja na majibu mazuri ambayo Naibu Waziri, amejibu na Mhe. Waziri, sasa hivi pia amejibu, naomba mimi ufahamu tu, baada ya miaka 4 ambayo imepita ni muda gani zaidi tusubiri ili zoezi hili litakapokuwa limeanza rasmi, naomba jawabu katika hilo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kama baada ya kupitisha bajeti hii tutaletewa fedha kama tulivyoziomba tukiletewa kwa ajili ya kununua chakula, tutaanza kutengeneza ghala lile na kuanza kununua chakula kwa kukiweka. Chakula kile kama nilivyosema mwanzo sio kama kinakaa pale kungojea matatizo, ni chakula kinakaa kwa muda maalum. Mahindi yana muda wake, mchele una muda wake, sukari ina muda wake na inakuwa kila baada ya muda, muwe vitu hivi mnavitoa, mnaingiza vyengine, tukipata pesa, nadhani hata tukipata kwenye bajeti hii, basi ataona kuanza kuweka masuala hayo, lakini hatujapata hizo pesa, ndio tatizo letu.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi yote hayo ninayafahamu, yote ninayaelewa, lakini nasema kwa mujibu wa maelekezo na namna ambavyo utaratibu wa mradi huu ulivyoanza na maelekezo ambayo tulikwisha kupewa tokea mwanzo, mimi sina matatizo na yote ambayo Mhe. Waziri, anatueleza. Tunachotaka Mhe. Waziri, atuthibitishie katika Baraza hili yeye akiwa kama Kaimu Waziri, hili zoezi hasa la kuweza kuanza hiyo hoja yenyewe ni mwaka gani? Ikiwa mwaka huu atujibu, ikiwa mwakani au ikiwa mtondogoo, sisi tunataka mwaka tu atwambie kwamba hili suala litakuwa mwaka fulani limeanza.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, mwaka huu tukitiliwa pesa, nitalianza hili zoezi.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, bora tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ilikuwa ni hii hii sawa na Mhe. Mahmoud, kwa maana hiyo Mwenyezi Mungu asije akajaalia ikatokea ukame, mimi nataka kufahamu tu hiki kitengo kiko muda

mrefu. Kipo jina au kipo kivitendo kweli kweli. Nataka kufahamu kuna tani ngapi sasa hivi za akiba zilizokuwepo na chakula aina kilichokuwa ni akiba.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, nimejibu hatukuanza kwa sababu hatukuingiziwa pesa, hilo ndio tatizo, tukiingiziwa pesa, tutaanza. Hivi sasa tunashukuru sana wafanyabiashara wanajitahidi sana kuleta vyakula na hii ndio hali kidogo tunaona kwamba tunakwenda vizuri katika nchi hii, lakini ni vizuri kuwa na akiba ya chakula chetu tukakiweka, *in case* tuombe Mwenyezi Mungu usitokee ukame au lisitokee tatizo la chakula, lakini pia, kuna huu upande wa pili wa wananchi, sasa kuelimishwa juu ya suala la kutengeneza lishe na kutumia chakula cha lishe ni kitu muhimu sana kusema tulifanye vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nalo pia lina nafasi yake. Kwa hivyo, siwezi kumwambia kwamba tuna chakula ghalani kiasi gani, hatuna na wao wamekwenda Kamati wamekuta ghala halijafanyiwa matengenezo.Tulichokifanya sisi tumewaandikia barua waliokodi yale maghala kwamba waturejeshee maghala kwa ajili ya shughuli hii, lakini tumeshindwa kutumia nguvu kubwa kwa sababu hatuna hizo pesa za kuanzia hicho chakula chenyewe kununua, lakini tukianza kupata pesa wale wote waliokwenda maghalani watatukabidhi maghala yetu tutawatoa, kwa sababu tumewakodisha na wameshatokea wakati maalum kwamba sasa hivi tuweze kutulia. Tukipata tutaanza bila shaka hiyo kazi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hiki ni chombo cha wananchi na wananchi wanatusikiliza, kama serikali haijawa tayari, kwa nini wasisubiri mpaka itakapokuwa tayari wakajawakaleta hiki kitengo tukakipitisha, maana yake huu ni mwaka wa nne, hakuna dalili wala harufu yoyote nzuri, mimi naona tukiweke upande ili tuendelee mpaka serikali itakapokuwa tayari, tuje tena panapo uhai kama sikuja mimi, atakuja mwengine, ndio ushauri wangu huo tukiondoshe tukiweke upande.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, tusiiondoe tuiombe sisi Wizara Fedha itutilie pesa, hivyo ndivyo vitu muhimu ili tuanze hili zoezi, ndio kitu muhmu kusema kweli.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nadhani tukubaliane kwamba nia ni moja, Wizara wana nia hiyo na sisi Wajumbe tuna nia hiyo, kubwa ni kwamba tusimamie zipatikane fedha shughuli hiyo ianze. Nadhani tuendelee.

Kifungu 1401 Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe- 194,500,000
Kifungu 1401 Idara ya Kilimo-

Mhe. Panya Ali Abdallah: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, nilipokuwa nikichangia nilichangia kuhusu kilimo cha mboga mboga, nikaomba serikali kwa sasa naona kuna kilimo hiki cha *green house* kinachofanywa na kinaonesha kinaleta tija kubwa kwa sehemu ndogo ya ukulima. Kwa hiyo, nikaishauri wizara kwamba ina mpango gani wakuweza kushughulika na kilimo hiki ili wakulima wetu waweze kupata tija kwa kulima sehemu ndogo kuliko kuwa wanalima sehemu kubwa, lakini mavuno yanakuwa kidogo. Serikali imejiandaa vipi kuhusu kulifanyia utafiti jambo hilo?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kumfahamisha Mhe. Panya Ali Abdalla, sote tunataka kuendeleza kilimo kwa sababu tunajua kwamba kilimo ni uti wa mgongo na Wizara ya Kilimo inafanya utafiti njia mbali mbali ili kuboresha kilimo. Suala la *green house* hili ni suala ambalo wizara ishafanya utafiti sana, lakini kilimo hiki lile jumba lake moja ni milioni nane, ni suala ambalo tunaweza kusema kwamba ni ghali sana. Pia, tumejaribu kupita kila pahala kwenda kutizama na kwenda kukagua hata hapa Kisauni nishawahi kwenda na tushaona kina tija.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kutokana na gharama mkulima kuweza kumudu gharama zile ni nyinyi.Waheshimiwa mtakuja kulia hapa hapa, Waheshimiwa wenye majimbo watataka wakulima wafanyiwe lile. Hivyo, mtakuja kulia hapa hapa. Kwa hivyo, tunapenda sana kwamba tuone tunaimarisha kilimo na bado tutaendelea kufanya utafiti juu ya suala hilo. Itakapowezekana hali itakapokuwa nzuri, basi hakuna tatizo, sisi wakulima wetu tunataka wapate tija na serikali ipate tija.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, nashukuru kwa majibu ya Mhe. Naibu Waziri, basi haya naomba tuendelee na uhakika wa chakula na lishe ili tuwe na uhakika nacho chakula kiwepo na haya mengine tutafanya wakati mwengine Mwenyezi Mungu atakapotujaalia.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, hapa nilikuwa nina hoja katika mabonde ya mpunga na Mhe. Naibu Waziri, wakati akinijibu alinielezea kwamba kuna mabonde ya mpunga kweli yamevamiwa, amekiri hilo na akasema wamo mbioni kutoa hatimiliki ya baadhi ya maeneo, lakini aliwataka Wakuu wa Wilaya pamoja na taasisi nyengine husika zisimamie haya mabonde ili yasivamiwe. Haya ndio majibu ya kila siku ambayo tumeyazoea, lakini siku kila zikiendelea mabonde haya yanamalizika, kulikuwa na mabonde kama manne tu, bonde la Ziwamaboga, Melinne Kijitoupele, Mwera, Melitano na Chuwini, nyumba zinakaribia kufikia katikati ya mabonde. Sasa Mhe. Naibu Waziri, anapotwambia kwamba labda taasisi husika, sisi hizo taasisi nyengine zinazohusika, sisi tuna mashaka makubwa kwamba wao wenyewe wanahusika na kuruhusu ujenzi, kwa sababu kama hawahusiki mwananchi wa kawaida hawezi akenda akajenga kwenye bonde pasipo na kupata kibali cha ujenzi, pasipo na kuomba lile eneo. Sasa kama unatwambia taasisi nyengine zichukue hatua ni taasisi gani?

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri Kaimu Waziri wa Kilimo ndio Mhe. Waziri wa Ardhi, mimi nataka anieleze hapa na nataka nipate kauli, ni lini pamoja na kwamba anawataka watu wa jiji na anataka taasisi zifuatilie kwa sababu Wizara ya Kilimo nyie ndio wenye eneo na kama eneo lenu linachukuliwa linajengwa mnasubiri taasisi nyengine isimamie hapa ni tatizo. Kwa hiyo, nataka niambiwe suala la kusimamia ni sawa, lakini wale ambao wameshajengwa nataka kujua Wizara ya Ardhi tunaona mifano kwa wenzetu kwa kina, Mama Anna Tibaijuka wanabomoa majumba mpaka ya mawaziri, lini wale ambao wameshajenga mejengo yataenda kuondoshwa ili yale mabonde yanufaishe wakulima, ili waweze kuondokana na umasikini ni lini?

Mhe. Mwenyekiti, jengine nilizungumzia suala la shamba la Kibondemzungu, hili sikupata ufafanuzi wake na nilitoa *document* ya wananchi karibu 198 ambao wamejiorodhesha wameitwa kwa Mkuu wa Wilaya kuzungumziwa juu ya suala la shamba la Kibondemzungu kwamba limo ndani ya utafiti kuna mambo mapya yanataka kufanyika, lakini wao yale mashamba wametakiwa wayarejeshe. Nikanukuu kitabu cha Mhe. Waziri, moja katika sera zao kwamba wanataka kuondosha umasikini, kama hii kuwanyang'anya kuja kuwapa watu wengine, ndio kuondosha umasikini, wanataka kutekeleza Ilani, kama hivi kuwanyang'anya wale ndugu zetu wana CCM wa Kijitoupele, ndio kutekeleza Ilani. Mhe. Waziri, naomba nipate majibu ya kutosha katika hoja hizi mbili.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Salum Haji, amezungumza suala zito na mbinu zake za kuchukua hatua ni nzito na linaweza likasababisha hata *instability* katika nchi. Pia, amejaribu kusema kwamba wanaohusika ni serikali peke yake, lakini tunapoichambua serikali, basi nadhani kwa sababu mimi nimeingia katika Wizara hii ya ardhi, nimeshajifunza na nimeshaona mambo haya yanavyotendeka, ni vizuri nieleze. Ardhi ya bonde la mpunga asi-*rule out*, akasema kwamba waliojenga katika mabonde ya mpunga wamepewa vibali, sio kweli, hawakupewa vibali wote wale, lakini jambo linatokea katika shehia, Sheha yupo ukifuatilia suala lile, utakuta kwamba kibali pale kimetoka kwa Shehe, maana kuna baadhi ya Masheha wanatoa vibali na ushahidi ninao kwenye Ofisi yangu, lakini sasa tunataka viongozi sote tuhusike katika suala hili la kuzuia kuvamia mabonde haya ya mpunga.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka wakati fulani Mhe. Hamza Hassan Juma, alijitahidi sana kuona anajaribu kuzuia suala hili, lakini lilikuwa zito na gumu sana, kwa sababu wewe umekaa nyumbani kwako, mtu kule anajenga usiku usiku na ujenzi mara nyingi wanaanza usiku usiku, sasa siku ya pili unapata taarifa kwamba hapa kuna mtu kaanza kujenga na ukimuendea yule aliyejenga anakwambia, mimi nishapewa ruhusa hii hapa, nimepewa na Sheha au Diwani nijenge hapa, unakuja kukuta nyumba imeshasimama, ndio unakuja kugundua wewe kama pale kumesimama nyumba na watu wako pale wanaona hawasemi wananyamaza kimya.

Mhe. Mwenyekiti, sasa unataka kuingia kutafuta *bulldozer* ili uyavunje yale majumba, ni suala la lazima uwe na uamuzi wa kisasa mkubwa sana, uamue na mukubaliane katika suala hilo. Mimi sioni uzito katika kutekeleza suala hilo hata kidogo, lakini tukubaliane na wenzangu kwamba tunabomoa majumba yaliyomo katika mabonde ya mpunga, hiyo kazi tutaitekeleza tena kwa siku moja tu, tutazibomoa zote, kwa sababu sheria pale imevunjwa, mtu kajenga hakupewa ruhusa, kapewa ruhusa na mtendaji wa pale pale, ni tatizo kubwa sana, kusema kweli si jepesi kiasi hicho.

Mhe. Mwenyekiti, wakati fulani unachukua hatua unapokuweko pale, ukiondoka, anakuja mwengine, anaruhusu ujenzi unaendelea, matokeo yake nyumba zinasimama. Kwa kweli mimi labda nitumie nafasi katika kipindi hiki kuwambia watu, ni kosa kwa mtu yeyote kujenga nyumba, bila ya kibali rasmi yakupewa matumizi ya ardhi katika eneo lile, ni kosa na sheria inaruhusu moja kwa moja kuja kuchukuliwa hatua ya kisheria. Wananchi wote wanaojenga katika maeneo, wajue kwamba wanavunja sheria, wanapojenga katika maeneo yale na ukiendelea, wanataka kuligeuza suala hilo la kisiasa, lakini si suala la kisiasa, ni suala la kisheria hili tatizo lipo. Nategemea

Masheha watakuwa wamenisikia sasa hivi, Madiwani watakuwa wamenisikia sasa hivi, Wakuu wa Wilaya watakuwa wamenisikia sasa hivi, wote watajua kwamba ni jukumu lao. Ni jukumu la Sheha wa mahala pale kuhakikisha kwamba anaona kuwa ardhi ya kilimo haivamiwi, ni jukumu, si suala la kwamba ni hiari yake Sheha, ni jukumu lake, kwa sababu lazima tupate mahala mwa kulima.

Mhe. Mwenyekiti, hayo ndio matatizo yaliyotokea na hasa katika Wilaya ya Magharibi, ndio uvamizi huo umekuwa mkubwa sana kusema kweli. Hilo suala lipo. Kwa hiyo, sijui nimjibu nini Shekhe Ali katika suala hili, lakini katika picha alizorusha kwamba tukavunje kisiasa kabisa na wanasiasa tuko madhubuti katika hilo. tutatekeleza tu mara moja, hakuna shida juu ya hilo, zimeshawahi kuvunjwa nyumba ngapi hapa, huko Tomondo kushawahi kuvunjwa majumba na maneno yakawa mengi hapa, watu wakapiga makelele na nini, hilo si tatizo hata kidogo, tukishaamua, tunatekeleza, basi tutatekeleza, tuko pamoja kusema kweli.

Mhe. Mwenyekiti, hilo suala limenishtua sana, kwa sababu ndio linanipa shida sana, hata pale Mwera sasa hivi utaona kwamba lile bonde kidogo tayari linaanza kunyofolewa nyofolewa pale na watu walivyokuwa wajanja wanajaribu kuanza kujenga msikiti, maana Muislamu kavunja msikiti, utaonekana ni mtu wa ajabu kweli kweli, unaanza kujenga msikiti pale, hilo ndio tatizo ambalo linatokezea. La pili, Shekhe Ali Salum lilikuwa suala gani? Hebu nikumbushe.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, suala la Kibondemzungu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, suala la Kibondemzungu kwa kweli itabidi atupe ruhusa tulifuatilie kwa Mkuu wa Wilaya alikusudia nini katika kutoa barua hiyo, kwa sababu mimi sina habari nimewapeleka maafisa wangu na wao hawana habari. Kwa hiyo, itabidi atuache tufuatilie kwa Mkuu wa Wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, unakumbuka wakati fulani Mhe. Rais, alipokuwa akifanya ziara alisema masuala ya migogoro ya ardhi iliyoko huku inasababishwa na nyie mlioko huku, itatueni migogoro yenu, hili alitwambia kwamba watatue wenyewe kabla yeye hajaingia kutatua. Hivyo, basi watatua wenyewe. Kusema kweli hili suala lipo limeshatolewa katika maeneo mbali mbali. Kwa hivyo, hili Shekhe Ali tupe nafasi. Namuomba Shekhe Ali atupe nafasi katika hili tulifuatilie kwa Mkuu wa Wilaya, alikusudia nini barua zile, maana mimi sina habari nalo na watu wangu wa Wizara ya Kilimo hawakunijibu, nadhani na wao hawana habari nalo. Kwa hiyo, tutalifuatilia na tutampatia jibu bila shaka.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia vizuri Mhe. Kaimu Waziri, alipokuwa akijibu hoja zangu, hili la pili la Kibondemzungu wakati amekiri kulifuatilia, mimi huwa sina tatizo sana, lakini na mimi ninataka kumtosheleza, kadhia hii imefika juzi usiku na watu walikuwa wako katika maandalizi yakwenda kumuona Makamu wa Pili wa Rais, juu ya suala hili kwa bahati kabla hawajafika huko, ndio nikakutana nao na mimi nikawaambia nitalifanyia kazi na jawabu mtalipata.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru Mhe. Waziri, kwa kulichukua na namuomba alifanyie kazi haraka sana, lakini katika ile hoja ya mwanzo ambapo Mhe. Waziri, alikuwa ana hofu zaidi suala la kwenda kuvunja nyumba kwa shughuli za kisiasa. Mimi nafikiri tukianza kuogopa sheria kwa kuogopa siasa, sijui tutafika wapi, kama tunatunga sheria na tunatakiwa tuzisimamie sheria na watu wanatakiwa wazifuate sheria, lakini wanavunja sheria tukianza kuwaogopa kwa kuogopa shughuli za kisiasa, hii nchi itaangamia, tunatakiwa tuwe makini kuzisimamia sheria za nchi na yule ambaye amevunja sheria za nchi, basi hatua za kisheria ziwe zinachukulia.

Mhe. Mwenyekiti, majibu mengi ambayo Mhe. Waziri, amenijibu katika hoja hii, hayakuwa na uzito, amenijibu kwamba nyumba zinajengwa usiku. Hapa tunapitisha bajeti na ndani ya bajeti kuna watu, sisi tunawapitishia pesa hapa, kama ni wafanyakazi, haya mabonde imani yangu kwamba kila bonde sio kama litakuwa halina Ofisa wa Kilimo hata siku moja. Sasa anaposema kwamba nyumba zinajengwa usiku inabidi wao wenyewe haya mabonde Ofisa wa Kilimo hakuna, wasimamizi wa wizara au watendaji wakuu hawapiti kwenye mabonde yao kuyatizama, yaani mpaka nyumba inajengwa, wao hawapiti, nyumba hiyo ikijengwa usiku, asubuhi kwani inakuwa imeshahamiwa? Hakuna inaonekana hata mzunguko wa utendaji wa kazi hauko vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia, nilitoa *option* mbili juu ya mabonde haya, nilimwambia Mhe. Waziri, kama atakuwa anakumbuka na *Hansard* aje aangalie. Nilimwambia aidha tukavunje majengo, kama hawawezi kuvunja majengo, atoe vibali vile vipande vilivyobakia bakia, watu wajenge ili tumalize yale mabonde yawe maeneo ya kujengwa. Hizo ndio *option* mbili nilizozitoa, aidha, tukayavunje majengo au atoe vibali vya ujenzi ili yale maeneo yapimwe ili tuwape wananchi wajenge kwa sababu inakuwa ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi Mhe. Waziri, hili namuachilia, kwa sababu nafikiri yote ni mambo yakwenda kukaa na kutafakari mambo mazito. Hivyo, namuachilia aende akatafakari kuona namna gani anaweza akaisaidia jamii wale wanyonge wa Mwenyezi Mungu ambao wanakuwa wanategemea rizki zao katika mabonde yale na matajiri kwenda kuzichukua zile ardhi na kuanza kujenga na ndio maana nilipomuuliza tunataka kuondosha umasikini au tunataka kuuongeza, tunatekeleza Ilani au tunaiharibu Ilani. Tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Kabla yakuendelea maelezo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, hapana iko haja yakumshukuru sana Shekhe Ali Salum kwa kauli hii aliyoitoa hapa na ameitoa mahala pazuri na wananchi wamesikia, nadhani sasa hivi Wizara ya Kilimo italazimika kuorodhesha majumba yote yaliyojengwa katika maeneo ya mabonde ya mpunga. Kwa hiyo, tukae kitako na Wakuu wa Wilaya, tufikirie tutachukua hatua wakati gani, lakini tuchukue hatua. Kwa hiyo, maneno uliyoyasema ni mazuri, Wizara ya Kilimo waanze kuorodhesha majengo yaliyojengwa katika mabonde ya mpunga, Wakuu wa Wilaya wawe tayari tukutane wanachukua hatua gani katika mabonde ya mpunga na tutachukua hatua. (*Makofi*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, usione nasimama mara kwa mara, mimi ni Mjumbe wa Kamati hii na kama hana watetezi, nilitaka kujua sababu gani Chuo cha Kizimbani kutoka milioni 90,000,000 wakapewa milioni 10,000,000 hiki ni kilio cha Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, la pili, ni kwamba likizo zao hawalipwi ni sababu gani wizara kutokuwalipa likizo zao, haya si maneno yangu, ni maneno ya Wajumbe wa Kamati tuliokaa nao.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, kwani hii Idara ya Kilimo tumeshaimaliza?

Mhe. Mwenyekiti: Inaonekana hoja hiyo sio pahala pake, Mhe. Jaku Hashim, hiyo sio sehemu yake.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, nilipokuwa nikichangia niliomba Mhe. Waziri, anisaidie maelezo umuhimu katika Wizara ya Kilimo ni kitu gani? Ni suala la Santuri na mambo mengine au ni ununuzi wa mbegu za utafiti, mbolea, pamoja na madawa ya kuulia wadudu, kwa sababu eneo hili naona halikutiliwa pesa lina sifuri. Sasa nilimuomba Mhe. Waziri, aniambia, je, madawa wanayo mengi ndani wanaendelea kutumia au wameona kwamba waelekee katika Santuri na mambo mengine. Nilikuwa naomba majibu katika eneo hili.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, sijui Mjumbe amekusudia kifungu gani, hebu anisaidie.

Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, fungu nililokusudia katika ukurasa wa 73, Idara ya Kilimo, fungu kuhusu huduma za kilimo 22 1000, ndipo nilipo-*raise concern* yangu hapo wakati nilipokuwa nikichangia.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, katika sehemu hii si kama hatuhitaji huduma za mbolea, tunahitaji huduma za mbolea, lakini huduma hii hapa tulikuwa hatukuingiziwa pesa, bado mpaka leo ilikuwa haijafika hiyo mbolea yenyewe hapa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuthibitisha kweli. Hii mbolea ya kupandia kwa sababu ya rutba ya nchi yetu, ukiweka mbegu yoyote tu inaota. Sasa wakulima wengi wanaona kama wanapata hasara. Kwa hivyo, ni ukweli kabisa watu hawaitumii, lakini ipo na inasaidia. Tunasaidia taaluma tu, lakini kweli wakulima tokea miaka na miaka inakaa ghalani tu nyingi kabisa. Unajua wakati wetu huo nathibitisha ni kweli.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu hayo ya kuambiwa kuwa mbolea hii ipo, lakini pia, nawaambia kuwa mbolea kama zipo tusiwekewe mbali na vituo vyetu tunamolimia, kwa sababu bonde letu la Saninga tuna banda letu na ghala ipo, mbolea tuwekewe pale. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, hili pia nimemjibu aliliuliza. Kuna utaratibu wa mbolea kupeleka katika vituo na kwa mwaka huu nilisema nilipomjibu hapa wakulima wametaka wenyewe

wasogezewe hiyo mbolea katika hicho kituo chao na wamesogezewa. Kwa hivyo, hayo pia tunayakubali tutachukua ushauri wake.

Kifungu 1705 - Idara ya Uendeshaji na Utumishi Pemba- 2,409,853,000
Kifungu 1706 - Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe Pemba- 42,000,000
Kifungu 1707 - Idara ya Kilimo Pemba-

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nilipokuwa nikichangia katika sehemu hii, nilisema katika ukanda huu tuanze Kaskazini Micheweni mpaka kufika Vitongoji. Katika kilimo cha maweni ametoa mfano kama mwaka 1972-1974, ilikuwa kuna kipando hichi cha kilimo cha maweni, mtama na mawele yalikuwa yanavunwa sana, lakini ilikuwa kuna usimamizi mzuri. Ametoa mfano kama siku ya watu kwenda dago, lakini ilikuwa kama hujalima huendi dago na mara hiyo ukapandwa mtama kwa kushirikiana kwa vikundi vya ushirika na mtama ulivunwa mpaka ukabaki kwenye mashamba. Nasema nataka kujua Mhe. Waziri, usimamizi ule au umepotea.

Mhe. Mwenyekiti, halafu nikasema katika mabwanashamba na mabibishamba wanabaki tu maofisini, hawatembelei wakulima ili kujua kero zao ni zipi na kunafanyika nini. Hapa Mhe. Waziri, naomba jawabu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, suala la mabibishamba na mabwanashamba kwamba hawatembei na wanabaki ofisini. Mimi nasema kwamba bado mabibishamba na mabwanashamba wanafanya shughuli zao, lakini juzi nilijibu hapa swali ambalo siku zote linazungumzwa. Katika majibu hapa nilisema inawezekana kwamba hawa mabibishamba na mabwanashamba hata humo sehemu nyengine wakulima hawajui tofauti ya bibishamba na Afisa ni yupi. Hili linatokea na tumeshalikuta. Kwa hivyo, ndio inapokuja kwamba hata wale wakulima tulikwenda katika ziara moja, wanasema hivi hivi mbele ya Makamu wa Kwanza wa Rais, sisi bibishamba na bwanashamba hawajafika. Wakaulizwa huyu nani? Huyu anakuja siku zote hapa, kumbe ndio bwanashamba.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nina imani, mimi hizi kelele za kila siku bibishamba hafiki, bwanashamba hawawajui. Bila shaka tutakaa wizara kuwaelimisha wakulima nani bwanashamba na nani bibishamba, tufanye hivi, lakini nina imani mabibishamba na mabwanashamba wanafanya kazi zao. Nikasema pia kutokana na upungufu wa mabibishamba na mabwanashamba inawezekana kweli wengine hawafiki, kwa sababu bwanashamba mmoja amepewa shehia sita, anaweza akazitumia shehia mbili au tatu shehia nyengine hajafika, lakini tatizo hili nikasema litaondoka baada ya kupata uajiri ambao utaziba pengo juu ya haya matatizo tuliyokuwanayo. Kwa hivyo, naomba suala hili tutajitahidi na hawa mabibishamba na mabwanashamba tukitafuta Ofisi zao, zipo mabondeni, hawana Ofisi.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, amenijibu bwanashamba tu, ukulima huko maweni hajanijibu na usimamizi mzuri, mtu kulima ni hiari yake, lakini kunakuwa na usimamizi na nikasema mazao haya yaliyopatikana kulikuwa na usimamizi mzuri na nikasema bado yanastawi mazao yale. Nikatoa mifano matikiti maji yanalimwa sana, matango, uwele na mtama hasa kisiwani Kojani. Mfano sisi tunaongoza kwa kulima mtama, lakini usimamizi sio mzuri hajanijibu. Naomba jawabu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, namwambia Mhe. Mwakilishi, kwamba tutajitahidi kuboresha suala la usimamizi. Nakubaliana na yeye kwamba unapokuwa usimamizi mzuri na mafanikio yanakuwa mazuri. Kwa hivyo, mimi nachukua ushauri wake kwamba tutaboresha suala la usimamizi ili tupate ufanisi wa kilimo.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Naibu Waziri, lakini nitafurahi sana akija kutembea kisiwani Kojani na akija Kojani avuke Kojani, halafu avuke aende ng'ambo aone hizo sehemu za kilimo. Avuke mara mbili na mimi tukijaaliwa kama utanialika nitashiriki nitakuvusha utaona. Kama ni hivyo, tuendelee.

Kifungu 1707 - Idara ya Kilimo Pemba- 99,000,000
Kifungu 1708 - Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Pemba- 66,000,000
Jumla ya Fungu- **13,758,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 20 - Wizara ya Kilimo na Maliasili-

Kifungu 0401 -

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu inakuja kwenye kasma 610014, Programu ya kuendeleza sekta ya kilimo. Hapa pana msaada, nataka kujua Kituo cha Kizimbani kitapata msaada huu? Maana yake kulikuwa na kilio nilichokisimamia. Mwaka jana iliomba milioni 90, ikaingiziwa milioni 10 kama yatima. Je, msaada huu watakaopata hapa watanufaika kwa jicho la huruma Kituo hichi cha Kizimbani kutokana na bajeti yao kuwa ndogo? Na hichi ni kituo kimoja muhimu sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, huu mradi umeandikwa hapa wa *ASDP*, lakini kwa ajili ya sekta ya kilimo kwa ujumla. Labda liwe lake kama ni ombi kusema kwamba katika msaada huu, zipelekwe pia katika Kituo cha Kilimo Kizimbani. Hiyo wizara itakaa kitako kulifikiria suala hilo baada ya kujua hasa huu mradi umetegemewa kufanya nini na nini. Sasa mimi siwezi kumjibu *off-hand* hapa kwamba mradi wa *ASDP* na *ASDP- I* kuwa ndio utakwenda Kizimbani moja kwa moja. Hilo siwezi kumjibu mpaka ionekane ile *component* ya mradi wenyewe unazungumzia mambo gani katika hayo. Aliweke kama ombi ikionekana kuna *possibility* watekeleze watu wa Idara ya Kilimo, siwezi kujibu hapa. Najua Chuo cha Kilimo Kizimbani kina mradi wake 610020.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, wakae walifikirie badala ya milioni 90 mwaka jana wakawapa milioni 10 na kama kulifikiria walifikirie wao. Hichi chuo ni muhimu. Mimi nimuombe tu awatizame kwa jicho la huruma.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, nimesema kama ni ombi, ndio tunalipokea, kwa sababu kila mradi una mambo yake yaliyokwisha kupangwa. Kwa hivyo, tulichukue kama ni ombi tu. Kila mtu ana mambo yake yaliyokwisha kupangwa ya kufanya.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, maana yake leo mimi kidogo naumwa sioni vizuri, kumbe pana kifungu chake hapa. Hii hapa miundombinu ya Chuo cha Kilimo Kizimbani, hicho kifungu kidogo 610020, bahati kimo Chuo cha Kizimbani. Hoja yangu kifikiriwe tu bado hichi chuo.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja yako hasa ni nini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hichi chuo mwaka jana kiliahidiwa milioni 90, kikapewa milioni 10. Sasa nikaona labda wafadhili hawa watakifikiria hichi chuo kilivyo, kutokana na hali yake kilivyo ambacho ni muhimu sana na bahati kumbe kimo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, nimemwambia kwamba kila mradi unakuwa na utaratibu wake na wale wanaotoa pesa wafadhili au mkopo wanakuwa wameshajua kitu gani kitashughulikiwa katika mradi ule. Sasa hapa tuna miradi mingi, kuna mradi huu aliouzungumza yeye wa 376 ambao 610014 unaoshughulikia kuendeleza sekta ya kilimo na mifugo *ASDP* na hii *ASDP- I* ya chini yake pale *development program* hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kuna mradi mwengine hapa, programu ya utafiti wa kilimo na maliasili nao pia una kazi yake. Pengine huu kwa sababu ni utafiti unaweza ukawa ndio huo uliokusudiwa katika Kituo cha Utafiti, maana Kizimbani kuna Kituo cha Utafiti na Chuo cha Kilimo. Vitu viwili mbali mbali hivyo ambapo utakuta kuna Chuo cha Kilimo kwenye 610020, hicho ni Chuo cha Kilimo Kizimbani.

Mhe. Mwenyekiti, sasa labda hii iliopo hapa tuichukulie, lakini mimi siwezi kuijibu hii. Wataalamu ndio wanaojua miradi wameipanga vipi, lakini nasema aliweke kama ombi ili wataalamu washughulikie suala hilo, ikibidi kama hakuna. Kama ipo ndio hii, itakuwa ndio imeshakuwepo kwa ajili ya Kituo cha Utafiti *(Agricultural Research)* iliopo hapa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Kaimu Waziri, lakini Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kumbe alikusudia kukiombea Chuo cha Kizimbani sio kituo na chuo kina fungu lake hapa ambazo ni milioni 278. Kwa hivyo, hiyo hoja yake nafikiri Mhe. Jaku, ameshaiondoa, kwa sababu alichokusudia ni chuo, sio kituo. Mwanzo alitamka kituo, mimi nikamuuliza unakusudia kituo au chuo? Akasema chuo, chuo kina fedha zake hapa, milioni 278 ni kubwa zaidi kuliko hizo milioni 90 ambazo ziliidhinishwa mwaka jana. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, labda atwambie tu kwamba hoja anaondoa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, aliyoyazungumza Mhe. Waziri, ni sawa sawa, lakini naomba kuhakikishiwa tu hiki chuo, hizo pesa kama watazipata. Nihakikishiwe hilo tu basi. Hoja ya Mhe. Haji Omar Kheri, pale ilikuwa ni sahihi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti: Kuna maelezo zaidi hapo Mheshimiwa. Anauliza hiyo fedha itapatikana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, wakati hizi pesa zipo, basi tutazipata.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, mimi hapa sina kuzuia fungu, isipokuwa nilikuwa naomba tu ufafanuzi kidogo. Kule mwaka jana katika eneo lile la uhakika wa chakula na lishe kuliombwa milioni 160 ikawa hazijapatikana. Zimeombwa tena katika bajeti hii, lakini na hapa sasa katika miradi ya maendeleo pana fungu la milioni 50. Tunaiomba serikali fedha hizi nazo izifanyie utaratibu ili kitengo hichi fedha izipate kwa ajili ya kufikia malengo yao ambayo walikuwa wamejiwekea. Maombi yangu yalikuwa ni hayo. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana nae.

Kifungu 0401 - Idara ya Mipango na Sera-	9,611,002,000
Jumla ya Fungu-	**9,611,002,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Wizara ya Kilimo na Maliasili bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na makadirio hayo ya Wizara hii ya Kilimo na Maliasili wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana kwa kazi kubwa mliyoifanya leo siku ya Jumamosi ambayo mlipaswa mpumzike na mmeifanya kwa ufanisi mkubwa sana. Nakushukuruni sana, lakini pili Waheshimiwa Wajumbe, kwa taarifa ambayo tumeipokea punde inaonekana kwamba siku ya Jumatatu ilipangwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuwasilisha hotuba yake, lakini kwa makubaliano ya Mawaziri kwa taarifa niliyoipata punde inaonekana siku hiyo itakuwa ni Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kwa hivyo, tuwe tunajua hivyo na watendaji watarekebisha hiyo ratiba kwa mtazamo huo.

Waheshimiwa Wajumbe, kuna taarifa mbili; Taarifa ya kwanza, ni maombi ambayo yametokana na sisi. Hii ni taarifa ya Wajumbe kuombwa tukubali tufanyiwe semina ambayo asili yake tuliomba sisi wenyewe Wajumbe kupitia Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi, kwamba Kamisheni ya Wakfu na Mali Amana iandae semina kwa ajili ya Waheshimiwa Wajumbe, ili kutoa taaluma kwa Waheshimiwa Wajumbe, inayohusiana na masuala ya zakka, mirathi, wakfu na hizo mali zenyewe za amana. Pia, kuhusiana na masuala ya kutoa uzoefu wao juu ya utaratibu ambao utawawezesha Wajumbe pengine na wananchi kumudu kufanya ibada ya hija. Hilo ombi kwa taarifa ambayo Katibu Mtendaji amenileta lilipelekwa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wakati wakiuliza shughuli za taasisi hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa Katibu Mtendaji ametueleza kwamba kimsingi yeye hana fedha kwa ajili ya kufanya semina hiyo, kwa sababu fedha aliyonayo yeye ni ile fedha ya amana, hiyo fedha ya wakfu ambayo ina

utaratibu wake maalum wa kutumia na hairuhusiki kutumika vyenginevyo. Sasa akatuomba tukubali, basi wao waje watoe taaluma kwetu, Ofisi kwa sasa nayo ina tatizo kidogo, nitalijadili kwa kina, lakini umuhimu wa taaluma hii kwa maombi tuliyopeleka kwa Katibu Mtendaji upo. Mkikubali kwamba semina hii ifanyike, yeye yupo tayari kuja kutoa hiyo taaluma tumuarifu tu na tulipanga ile siku ya mwisho mara baada ya kufunga shughuli zetu tarehe 28, basi tupande hapo juu kidogo watupe taaluma ambayo itatusaidia katika maeneo haya ambayo huwa yanatuletea vikwazo vikubwa.

Waheshimiwa Wajumbe, Katibu tulizungumza akaniambia kwamba vitu kama chai na vitafunio vyengine vinaweza kupatikana. Sasa tukikubaliana kwamba semina hiyo ifanyike, basi Katibu Mtendaji atatayarisha taaluma hiyo aje atupe siku ya tarehe 28. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru. Kwa hivyo, nitampa taarifa kwamba Wajumbe wanakubali semina hiyo ifanyike katika hali hiyo ambayo tunayo. Jambo la pili, nimepokea maombi mengi kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe wa upande wa CUF ambao wana shughuli ya Mkutano Mkuu Dar-es-salaam, hivi tunavyoendelea katika mchakato wa mambo mbali mbali na baadhi yao wameomba kugombea nafasi ya kushika nafasi humo ndani ya chama cha CUF, lakini kipindi hichi pia tuna shughuli hizi za Baraza na mambo yote hayo mawili ni muhimu. Sasa Mnadhimu alikuja akanipa ombi la jumla juu ya jambo hili, lakini sisi tulikubaliana kwamba shughuli yetu hapa iendelee isivurugike, maana wakitoka Wajumbe wote hao nayo haitapendeza machoni mwa wananchi kwamba shughuli hiyo inaendeshwa na Wajumbe wa upande mmoja, lakini pili, kuna hatari ya kukosa *quorum* na shughuli hizi zikawa zisiendelee.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa hivyo, tulichokubaliana ni kwamba wale Wajumbe ambao hawana maombi ya kugombea nafasi mbali mbali tuendelee na shughuli hii na wale ambao wanahisi wao wanapita bila ya kupingwa kwamba Mwenyekiti wa Mkutano atawaombea kura na wakapita bila ya kupingwa, wakapata hiyo nafasi waliyoomba. Basi nitapenda pia washirikiane nasi hapa ili shughuli zetu ziendelee bila ya kukwama.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa hayo ndio kati ya mambo ambayo Mnadhimu Mhe. Abdalla Juma Abdalla, tulikubaliana, yeye bahati mbaya hayupo, yupo Pemba anauguliwa na mzee wake, lakini kimsingi kama hakukupeni taarifa hiyo Waheshimiwa Wajumbe wa upande wa CUF, nakupeni hiyo taarifa ili iende sambamba na shughuli zetu ziwe zinakwenda vizuri. Pamoja na hawa wagombea mbali mbali wajaaliwe wapate hizo nafasi ambazo wameomba.

Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana kwa kunisikiliza. Nirudie tena kuwashukuru kwa kazi nzuri mliyofanya na mashirikiano makubwa mliyotupa. Sasa tuahirishe shughuli zetu hizi hadi siku ya Jumatatu tarehe 23/06/2014 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 8:05 mchana Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 23/06/2014 saa 3:00 asubuhi)